**2 SEPTEMBA, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Sita — Tarehe 2 Septemba, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika Mkutano wetu wa Nne, Kikao cha Sita.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. *ENG*. MSHAMU A. MUNDE):**

Majibu na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2025.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.02) Bill, 2026)*.

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.02) Bill, 2026)*.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na maswali na swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa ninamwita Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Kuteuliwa, aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 74

**Kima cha Chini Kubagua Kiwango cha Mishahara Kati ya Kampuni za Kigeni na za Kizawa**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. ABDULLAH ALI MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni inatengeneza tabaka kwa kanuni za mishahara ya kima cha chini kubagua kiwango cha mishahara kati ya kampuni za kigeni na za kizawa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya Kima cha Chini cha Mshahara inawekwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300. Sheria hiyo imeunda bodi za kima cha chini cha mshahara za kisekta kwa maana ya sekta ya umma na binafsi. Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi ina jukumu la kufanya utafiti na kumshauri Waziri mwenye dhamana na masuala ya kazi kupanga na kutangaza kima cha chini cha mshahara katika sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi nchini kinawekwa kwa kuzingatia sekta za kiuchumi. Aidha, upangaji wake unazingatia vigezo mbalimbali vilivyowekwa kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa na sheria za nchi zinazojumuisha uwezo wa waajiri kufanya biashara na kulipa ujira pamoja na gharama za maisha. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, maswali ya nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba anapambania maslahi ya watumishi na jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akifanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba maslahi ya watumishi kwenye nchi yetu yanakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake Mheshimiwa Rais ndipo ambapo tumeona ongezeko kubwa la mishahara, lakini pia kulipwa kwa fedha ambazo zimekuwa zikidaiwa na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja tu Mheshimiwa Waziri. Ukipita kwenye viwanda mbalimbali ambavyo vipo ndani ya nchi yetu kumekuwa na malalamiko makubwa ya vijana kuhusu maslahi yao. Kwanza, kwamba *local content* hailindwi; kazi ambazo zinatakiwa zifanywe na Watanzania wazawa zinafanywa na watu ambao ni wa nje, kazi ambazo vijana wetu wangeweza kuzifanya. Ni upi mkakati wa Serikali katika kusaidia vijana hawa waweze kupata hizo kazi ili maslahi yao yaweze kukua?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Festo Sanga, amekuwa ni mpiganaji hodari kufuatilia maslahi ya vijana wa Kitanzania; lakini ninamhakikishia kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipambanua wazi kwamba inajali maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika mwaka 2025 Mheshimiwa Rais aliona kuna haja ya kupandisha kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi katika sekta ya umma ambapo kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii ongezeko la kima cha chini cha mshahara ilikuwa kwa wastani wa 35.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais akaona jambo hilo hilo pia lifanyike kwenye sekta binafsi ambapo kupitia Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara na kwa kushirikisha wadau kwa maana ya vyama vya wafanyakazi, Chama cha Waajiri *(ATE)* na Serikali tulikaa pamoja na kufanya mapitio na kuja na kima cha chini cha mshahara ambacho kwenye sekta binafsi sasa ni ongezeko la 33.4%. Utekelezaji wake ulianza tarehe Mosi, Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Festo Sanga, tumekuwa tukifanya ukaguzi na *compliance level* ipo kwa kiasi kikubwa. Zaidi ya waajiri 90% wame-*comply* na hakuna mwajiri yoyote aliyekuja Ofisi ya Waziri kuomba *waiver* ya kulipa kima cha

chini cha mshahara. Hii maana yake ni kuwa, waajiri wamekubaliana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kulinda dhana nzima ya *local content*, tumeweka utaratibu maalum wa kutoa vibali kwa kazi zenye ujuzi maalum tu na zile kazi ambazo zinafanywa na Watanzania hatutoi kibali. Tumekuwa *strict* katika hili na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais; kuhakikisha kwamba tunapoanza utekelezaji wa Dira 2050 ambapo tunalinda uwezo wa nguvukazi na kuwawezesha Watanzania kupata ajira, tunahakikisha kwamba kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania zinaenda kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuhakikishia kwamba jambo hili tutalisimamia na tutahakikisha tunaendelea kufanya kaguzi. Hata wale wanaopita kwa njia za panya na kufanya kazi za Watanzania tutahakikisha hatua stahiki zinachukuliwa. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 75

**Haki za Wafanyakazi Wanaotoka kwenye Kampuni zenye Kazi za Kandarasi na Serikali**

**MHE. MARIAM A. MUNGULA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi wanaotoka kwenye kampuni zenye kazi za kandarasi na Serikali?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Mungula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kusimamia haki za wafanyakazi nchini kupitia Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura 366 ambayo pamoja na mambo mengine imeainisha haki mbalimbali za wafanyakazi wakiwemo wafanyakazi wanaofanya kazi katika kandarasi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utekelezaji wa sheria, Serikali imeendelea kufanya ukaguzi na kutoa elimu katika maeneo ya kazi ikiwemo kandarasi za Serikali. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026, jumla ya kaguzi za kazi 13,731 zilifanyika kwa waajiri mbalimbali ambapo katika kaguzi hizo 722 ni za wakandarasi wakiwemo wenye kandarasi za Serikali. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Mungula, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM A. MUNGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; ninaomba kufahamu ni hatua gani zinachukuliwa kwa wale wakandarasi ambao wanakiuka sheria na haki za wafanyakazi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; ninaomba kufahamu pia je, Serikali ina mfumo au utaratibu gani wa kupokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi wanaofanya kazi na kandarasi za Serikali kabla ya malalamiko yale hayajageuka kuwa ni migogoro ya kisheria? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mariam, akiwa ni mwakilishi wa wafanyakazi ameendelea kutimiza jukumu lake na wajibu wake

kama mwakilishi wa wafanyakazi kwa vitendo. Nimeshuhudia mara nyingi akifika ofisini kwangu kuleta changamoto zinazowahusu wafanyakazi wote katika sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake nitayajibu kwa pamoja. Serikali imekuwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa kwa wale wanaokiuka sheria za kazi. Kwanza, tunafanya *administrative procedure,* kwa maana ya utaratibu wa kiutawala kuwaita waajiri ambao hawatimizi jukumu hili. Pale wanaposhindwa kutekeleza hayo maelekezo tunakutana kwenye meza ya pamoja na tunawapa amri ya utekelezaji kwa maana ya *compliance order.* Asipotekeleza ndani ya siku 30 tunachukua hatua ya kumpeleka Mahakamani mwajiri huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 katika kaguzi hizi 13,731 waajiri wapatao 428 tuliwapa *compliance order* na kati ya hao, 11 tuliwafikisha Mahakamani kwa kutokutekeleza amri ya utekelezaji. Katika waajiri wale wanaochangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambao hawakufikisha michango ya waajiriwa wao, tuliwaita katika meza ya mazungumzo, lakini zaidi ya hapo tulihakikisha kwamba kama hawaja-*comply* tunawapeleka Mahakamani. Waajiri takribani 104 ambao hawafikishi michango kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tuliwafikisha Mahakamani kwa ajili ya hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni namna gani tunapokea malalamiko kutoka kwa waajiri na wafanyakazi; kwanza, tumeunda mfumo wa majadiliano ya pamoja, tunafanya *social dialogue* kwa maana ya waajiri kupitia chama chao cha waajiri na wafanyakazi kupitia vyama vya wafanyakazi *(TUCTA)* na Serikali. Tunafanya *social dialogue,* katika meza ya pamoja katika utatu tunajadili changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano pia tuna *social media platform* ya kupokea malalamiko ya wafanyakazi na tumekuwa tukiyafanyia kazi. Pia, kupitia mfumo wa Serikali kuna e-Mrejesho, hii imekuwa ni *platform*

nzuri ya kutuletea changamoto za wafanyakazi na tumekuwa tukizishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, hawa wamekuwa wadau wakubwa wa kupokea kero za wafanyakazi na kutufikishia kupitia Ofisi za Maafisa Wafawidhi wa Kazi katika mikoa yote 29 ya kikazi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kufanya kaguzi mbalimbali na waajiri ambao hawatazingatia sheria za kazi, hatua stahiki zitachukuliwa. Ninatoa wito kwa waajiri wote wa wafanyakazi ambao wana changamoto mbalimbali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano tupo tayari muda wote na ndiyo kazi tuliyonayo ya kusikiliza kero za wafanyakazi na kuweza kuzitatua kwa wakati. Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Sasa ninamwita Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Busega, aweze kuuliza swali lake.

Na. 76

**Ujenzi wa Soko Kata ya Lamadi – Busega**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa soko la kisasa katika Kata ya Lamadi, Busega?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Busega iliibua Miradi miwili ya Kimkakati ambayo ni Ujenzi wa Soko la Lamadi na stendi ya Nyashimo ambayo kwa ujumla ilikuwa ina gharama ya shilingi 9,000,000,000, yaani soko shilingi 5,000,000,000 na stendi shilingi 4,000,000,000. Baada ya uchambuzi wa maandiko hayo, Serikali iliishauri Halmashauri ya Busega kuanza na mradi mmoja wa kipaumbele zaidi kwa sababu za kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Busega ilichagua kuanza ujenzi wa Stendi ya Mabasi Nyashimo kama mradi wa kipaumbele ambapo Serikali katika mwaka wa fedha 2026/2027 imetenga shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi hiyo. Hadi sasa halmashauri inaendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Soko la Lamadi unatarajiwa kugharimu takribani shilingi 5,000,000,000 na utaanza mara baada ya ujenzi wa stendi kukamilika ambao ni mradi wa kipaumbele uliochaguliwa na halmashauri husika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Songe, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Nianze kwanza kwa kuipongeza sana Serikali kwa kutenga shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi katika Kata yetu ya Nyashimo. Pamoja na hayo nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ujenzi wa stendi Nyashimo ni mahitaji makubwa ya wananchi wa Wilaya ya Busega na tumekuwa tukihitaji muda mrefu na Mheshimiwa Rais aliahidi kuanza mara moja ujenzi huu wa stendi katika Kata yetu ya Nyashimo. Je,

Serikali sasa haioni umuhimu wa kufanya haraka taratibu za kumpata mkandarasi ili ujenzi huu uanze mara moja na wananchi wa Jimbo la Busega wanufaike na stendi hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kwa ufuatiliaji wake makini sana kuhusiana na ujenzi wa stendi katika eneo la Nyashimo, Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafahamu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa ziara zake alitoa ahadi na maelekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuanza ujenzi wa stendi katika eneo la Nyashimo na ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha tayari tumetenga shilingi 1,000,000,000 na taratibu za manunuzi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Busega kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tunatarajia kumpata mkandarasi, lakini pia tunaanza hatua za ujenzi wa awali wa stendi hiyo ya Nyashimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric James Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Soko la Nyakaliro ni la muhimu sana kwa wavuvi na wananchi wa Jimbo la Buchosa na Serikali imekwishapeleka fedha kwa miaka nane mfululizo na soko lile halikamiliki; na kwa kuwa, Halmashauri yetu ya Buchosa imeshatoa fedha za ndani kukamilisha soko, lakini imeshindikana na inapungua shilingi 100,000,000 tu soko likamilike. Je, Serikali ipo tayari kutoa shilingi 100,000,000 hizi ili soko hili liweze kukamilika na wananchi waweze kulitumia?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ukamilishaji wa ujenzi wa soko hilo ambalo kama maelezo yake linahitaji takribani shilingi 100,000,000 ili kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wa Buchosa wanapata soko hilo bora na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutashirikiana na Halmashauri ya Buchosa kuhakikisha kwamba tunakamilisha fedha hiyo, shilingi 100,000,000, ili tuweze kukamilisha ujenzi wa soko hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Halmashauri ya Wilaya ya Chemba tuliandika barua ya maombi ya ujenzi wa soko na Wizara ya TAMISEMI wakatupa maelekezo tutafute eneo na likishakuwa tayari watatuma wataalamu kwa ajili ya kuja kufanya upembuzi yakinifu ili waweze kutupatia fedha za ujenzi wa soko hilo. Je, ni lini sasa Wizara watatutumia wataalamu kwa ajili ya kuja kuhakiki eneo hilo na hatimaye waweze kutupatia fedha tuweze kujenga soko letu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Jimbo la Chemba, amefuatilia mara kadhaa na nimefanya ziara kule na Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara na Mheshimiwa Kunti alilisemea hitaji la soko la kisasa katika Halmashauri ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwanza ninawapongeza Halmashauri ya Chemba kwa kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa soko, vilevile ninawapongeza kwa hatua za awali za tathmini. Ninamhakikishia tu kwamba tutawatuma wataalamu Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kushirikiana na halmashauri, kufanya ukaguzi na tathmini ya eneo hilo, ili tuanze taratibu za kibajeti kwa ajili ya kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu, swali la nyongeza.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa soko kuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, maarufu kama Soko la Azimio, lipo katika hali mbaya sana kwa kiwango ambacho wakati wa masika linavuja na ni dogo na halitoshi kwa mazingira ya sasa ya ukuaji wa uchumi wa Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeonyesha nia kwa kutuma wataalamu hivi karibuni ili wakae na wataalamu wetu na kufanya uchambuzi wa namna Tunduru itapata soko jipya la kimkakati. Je, ni lini sasa ujenzi wa soko la kisasa la kimkakati katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Ado Shaibu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini. Ninamhakikishia tu kwamba tunatambua kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ni moja ya halmashauri kongwe na ni kweli kwamba Soko la Tunduru maarufu kwa jina la Azimio ni soko kongwe, lakini ni hitaji la wananchi kulikarabati. Ndiyo maana Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeshirikiana kwa karibu na Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri

ya Tunduru kupeleka wataalamu. Tayari tunayo taarifa ya mahitaji ya ujenzi na ukarabati wa Soko la Azimio pale Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea na taratibu za mwisho za tathmini pamoja na taratibu za kibajeti ili twende kulikarabati soko lile la Tunduru pale Azimio. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mecktridis Mdaku, swali la nyongeza.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa wananchi wa Malinyi wamekuwa wakipata shida sana na wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu kuanza kwa ujenzi wa soko la kisasa la Wilaya ya Malinyi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo kama inavyoeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2025 – 2030? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Malinyi kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara. Ni kweli kwamba halmashauri mpya nyingi kama Halmashauri ya Malinyi bado hazijajengewa masoko ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali, kwanza tumefanya mkakati wa kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa masoko katika halmashauri zote mpya, lakini na halmashauri zile ambazo hazina masoko. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Malinyi kwamba, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kuhakikisha kwamba tunaanza ujenzi wa soko katika Halmashauri ya Malinyi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Timoth Geofrey, Mbunge wa Kawe aulize swali lake.

Na. 77

**Ukarabati wa Soko la Tegeta Nyuki**

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati Soko la Tegeta Nyuki ambalo miundombinu yake imechakaa sana na wafanyabiashara na wateja wanafanya shughuli katika mazingira magumu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Timoth Geofrey Anyosisye, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Tegeta Nyuki ni muhimu kwa wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Kwa sasa soko hili ni chakavu, hali inayoathiri ufanisi wa shughuli za kibiashara. Ili kutatua changamoto hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2026/27 imeliweka kwenye mpango wa uboreshaji kupitia Mradi wa Uboreshaji Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, Awamu ya Pili (*DMDPII*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa mradi upo katika hatua ya ununuzi ya kutangaza zabuni ya kuwapata wataalamu washauri *(consultants*), watakaofanya usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Tayari taarifa ya tathmini ya tamko la nia (*expression of interest*) imekwishawasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuidhinishwa ili kuendelea na hatua inayofuata. Usanifu unatarajiwa kukamilika Disemba, 2026 ili hatua za ujenzi ziweze kuendelea. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timoth Geofrey, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Wanakawe ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa changamoto hii ya uchakavu ni ya muda mrefu, ninaomba Mheshimiwa Waziri atueleze, je, ni lini sasa yuko tayari kuongozana na mimi kwenda sokoni tukawaone wale wafanyabiashara na kuwapatia majibu haya mazuri ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; mwanzoni mwa mwaka huu sisi Wanakawe tulibahatika, tulitembelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kadha wa kadha, ikiwa ni pamoja na kuzitaka taasisi mbalimbali zinazohusika kukaa na kuona namna ambavyo daladala zinazotoka nje ya Dar es Salaam, kama Bagamoyo na Kibaha, zitakuwa zinaishia kwenye Soko la Bunju B. Maelekezo mengine aliyotoa ni pamoja na ujenzi wa barabara na shule. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu ujenzi wa shule, majibu tumepatiwa...

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa, uliza swali.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanakawe wanataka kujua, je, ni lini utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya magari kuishia Soko la Bunju B yatatekelezwa? Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninatumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Timoth Geofrey Anyosisye, Mbunge wa Jimbo la Kawe kwa namna ambavyo amekuwa msemaji na mfuatiliaji mahiri kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari mimi na yeye kuambatana baada ya kumaliza Bunge hili. Tutakaa pamoja tupange tarehe mwafaka ili tuweze kwenda kulitembelea Soko hili la Tegeta Nyuki na pia kuongea na wafanyabiashara na wananchi katika eneo hilo, ili kuwahakikishia kwamba Serikali sikivu ina mpango madhubuti wa kulikarabati soko lile ili kuwawezesha kufanya biashara katika mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusiana na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuboresha miundombinu yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tayari tumeanza kufanya tathmini na kuandaa taratibu za kibajeti, na pia kufanya usanifu katika baadhi ya maeneo ili kuhakikisha maelekezo hayo yanatekelezwa lakini pia miundombinu hii inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kawe kwamba, Serikali itakwenda kutekeleza ahadi yake na kuhakikisha kwamba mazingira ya biashara yanazidi kuwa bora zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Temeke ni jimbo ambalo linakua kiuchumi na Soko Kuu la Temeke ni Soko la *Temeke Stereo*. Soko hilo lina muda mrefu linafanyiwa ukarabati mdogo mdogo tu. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha wanalijenga soko la kisasa pale *Temeke Stereo*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE:)** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mama yangu Mheshimiwa Mariam

Kisangi, Mbunge wa Temeke amekuwa akifuatilia mara kadhaa kuhusu maendeleo na maboresho ya miundombinu mbalimbali katika Jimbo la Temeke. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mama Kisangi kwa ufuatiliaji wake makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeendelea kwa awamu, kwanza kutambua masoko yote kongwe na chakavu, kuyafanyia tathmini ya mahitaji ya gharama za ukarabati na kuweka mipango kwa awamu kwa ajili ya kuendelea na ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke aweze kwenda kufanya tathmini ya uchakavu wa soko lile, tuwe na taarifa rasmi ya mahitaji na makadirio ya gharama zinazohitajika, ili kwa pamoja Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na kwa mapato ya ndani ya Manispaa ya Temeke, tuone namna ya kuanza kufanya ukarabati kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Manispaa ya Shinyanga ni mojawapo ya manispaa ambayo ina soko kongwe, soko ambalo ndilo kichocheo kikubwa cha mapato ya Mkoa wa Shinyanga na manispaa yetu kwa ujumla. Mradi huu uliibuliwa na halmashauri ya manispaa, ulikuwa na gharama ya shilingi 4,000,000,000. Halmashauri hadi sasa tumeshatekeleza mradi huu kwa shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sasa TAMISEMI na Serikali ione haja ya kutumalizia shilingi bilioni 2.5 ili tuweze kukamilisha soko hili ambalo ni kichocheo kikubwa cha uchumi kwenye manispaa yetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mwanahamisi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga, kwa ufuatiliaji wake. Ninafahamu kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ni miongoni mwa halmashauri ambazo zina miradi mikubwa kupitia Mradi wa *TACTIC*. Pia ninafahamu kwamba uko mpango ambao unaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa soko la Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza halmashauri kwa kutenga zaidi ya shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi huo. Serikali inatambua kwamba bado soko halijakamilika. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu, kwanza za mapato ya ndani ya halmashauri, lakini pia kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ili kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa Soko la Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Khambay, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Halmashauri ya Mji wa Babati ni mji ambao unakua kwa kasi na soko tulilonalo kwa sasa halikidhi mahitaji. Halmashauri ya mji imekwishatenga eneo. Je, ni lini Serikali itatupatia shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya kujenga soko jipya la kisasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Mji wa Babati ni moja ya halmashauri ambazo zina uhitaji mkubwa wa soko na nimefanya ziara pale mara kadhaa na nimekagua soko lile, ni kweli ni chakavu lakini pia ni finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa Serikali, kwanza tunaendelea na utekelezaji wa Mradi mkubwa wa *TACTIC* katika Halmashauri ya Mji wa Babati; pili tunaendelea na taratibu za kibajeti katika kuhakikisha kwamba tunaboresha na kujenga soko la Babati. Kwa hiyo, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Emmanuel Khambay na ninampongeza kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara. Serikali hii kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba tunakarabati na kujenga soko katika Halmashauri ya Mji wa Babati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Samira Khalifani Amour, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 78

**Kuongeza Mabweni na Walimu katika Shule za Sekondari Mkoani Kagera**

**MHE. SAMIRA K. AMOUR** auliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mabweni na walimu katika shule za sekondari Mkoani Kagera ili kupunguza changamoto ya umbali na kuongeza ufaulu?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Samira Khalifani Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga mabweni katika shule zenye uhitaji kwa kadri ya sera, hasa kipaumbele kikiwa ni shule za kidato cha tano na sita, ili kuongeza

idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari ya juu. Vilevile, Serikali imekuwa ikiajiri walimu kila mwaka ili kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu nchini kote, ikiwemo Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilitoa shilingi bilioni 2.13 kwa ajili ya kujenga mabweni 19 katika shule 14 za sekondari na kuajiri walimu 1,176 waliopangiwa vituo katika shule za sekondari za Mkoa wa Kagera zilizokuwa na mahitaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga mabweni katika shule zenye uhitaji kadri ya sera inavyoelekeza na kuajiri walimu, ili kupunguza changamoto ya umbali kwa wanafunzi na kuongeza ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samira Khalifani Amour swali la nyongeza.

**MHE. SAMIRA K. AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyonipatia. Swali langu la kwanza, ninapenda kujua Serikali ina mkakati gani wa kuongeza mabweni hasa katika Mkoa wangu wa Kagera, ukizingatia wanafunzi bado wanatembea umbali mrefu sana kwenda shuleni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; ninapenda kujua mkakati wa Serikali wa kuongeza walimu katika shule zetu, hasa Mkoa wa Kagera, ili kuendana na idadi ya wanafunzi wengi waliopo katika shule zetu hivi sasa.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Samira Khalifani Amour, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kagera, kwa ufuatiliaji wake wa mara kwa mara. Ninamhakikishia tu kwamba, Serikali kupitia mipango mbalimbali, kwanza kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na kupitia miradi kama *SEQUIP;* tumeweka mkakati endelevu wa kuhakikisha kwanza tunatambua shule zote ambazo ziko katika mazingira hatarishi ambazo zinahitaji ujenzi wa mabweni na shule za kidato cha tano na sita na tumeendelea kujenga mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kutenga fedha na tutaendelea kujenga mabweni katika shule za Mkoa wa Kagera, ili kupunguza umbali wa wanafunzi kwenda masomoni na pia kuongeza ufanisi wa masomo katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tunafahamu kwamba kuna changamoto ya upungufu wa walimu katika baadhi ya shule kote nchini, ikiwemo katika Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa ambayo tumeiainisha katika mikoa 10 ya mwanzo yenye upungufu mkubwa zaidi wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika ajira za siku 100 za kwanza za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, walimu 7,000 waliajiriwa na walimu walipelekwa pia katika Mkoa wa Kagera na kupelekwa kwenye vituo vyenye upungufu mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Samira kwamba, tutaendelea kuwapa kipaumbele cha walimu kila ajira zinapojitokeza, ili Mkoa wa Kagera pia uweze kuwa na ahueni ya upungufu wa Walimu katika shule za sekondari. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yohana Msita, swali la nyongeza.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa

kuwa, Jimbo la Itigi lina shule 15 za sekondari na mimi kama Mbunge nimezitembelea zote, lakini ziko shule mbili ambazo kwa kweli zina changamoto kubwa sana ya mabweni. Shule hizi za sekondari ziko barabara kuu, kiasi kwamba watoto wa kike wanapata athari kubwa sana kulingana na idadi kubwa ya magari makubwa yanavyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kuiuliza Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kutujengea mabweni katika Shule ya Sekondari ya Kitaraka pamoja na Shule ya Sekondari Kamenyanga, ambazo ziko barabara kuu ambazo kwa kweli watoto wa kike wanapata athari kubwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Itigi. Ninakumbuka wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbunge alilisemea suala la uhitaji wa mabweni katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu kwamba, Serikali inayo sera na utaratibu. Kwanza tunatoa kipaumbele kwenye ujenzi wa mabweni kwenye shule za kidato cha tano na sita, pili, shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum na tatu shule ambazo ziko katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi kutuma wataalamu wake kwenda kufanya tathmini rasmi na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ili kuona uhatarishi wa shule hizo na kuona kama zinakidhi vigezo kwa ajili ya kujenga mabweni, ili Serikali ianze kujenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa suala hili linafanana kabisa ...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kupata nafasi ...

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Zainab Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa suala hili linafanana kabisa na maeneo ya Mkoa wetu wa Lindi, hasa katika Shule ya Sekondari ya Anna Magowa, ambayo imekuwa kwa kipindi kirefu sasa haina mabweni ya kutosha; je, ni lini Serikali itatoa kipaumbele kwa shule hii ya sekondari ambayo haina mabweni ya kutosha lakini pia haina ukuta? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko shule ambazo zina mabweni lakini hayatoshelezi, kwa maana ya uhitaji wa wanafunzi. Tunafahamu kuwa Mheshimiwa Zainab Kawawa amekuwa mfuatiliaji wa mara kwa mara kuhusiana na ustawi wa wanafunzi katika Mkoa wa Lindi na kote nchini. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua kwamba ziko shule ambazo zina mabweni machache na tunahitaji kuendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kutambua shule kama hizo, zikiwemo shule ambazo amezitaja na kutenga bajeti kwa awamu ili kujenga mabweni na kusogeza huduma za bweni kwa wanafunzi wetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kiteto ni kati ya majimbo yenye mazingira magumu na sisi tulileta andiko maalumu kwa ajili ya mabweni, je, Serikali ina kauli gani kuhusu Jimbo la Kiteto?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, pia iko Halmashauri ya Ngorongoro na halmashauri nyingine zenye mazingira yanayofanana na hayo ni halmashauri ambazo zina mazingira hatarishi. Kwa maana ya kwamba wananchi walio wengi ni wafugaji na shule zinakuwa mbali sana kutoka makazi ya wananchi. Hivyo, tumeweka utaratibu, ndiyo maana kwenye sera yetu ya ujenzi wa mabweni vipo vigezo vitatu. Cha kwanza, ni kwa kidato cha tano na sita; cha pili, kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na cha tatu ni mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kauli ya Serikali ni kwamba tumeendelea kujenga mabweni katika Shule za Kiteto, Ngorongoro na maeneo mengine. Tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti kuhakikisha kwamba shule za Jimbo la Kiteto zinaendelea kujengewa mabweni ili kuwasogezea huduma wanafunzi katika shule hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ndani ya Jimbo la Momba shule nyingi ambazo zimejengwa hazina kabisa mabweni na hivyo kufanya watoto kupanga nje kwenye makazi ya watu na kuhatarisha mazingira yao ya kusoma. Je, Serikali ina mkakati gani

wa kujenga mabweni kwenye Shule za Sekondari Kapele, Kangamo, Ikana, Momba, Nzoka, Msangano, Chitete, Mkulwe, Chilulumo, Uwanda, Mkomba, Ivuna pamoja na Mpapa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Momba kwa ufuatiliaji na ninafahamu Mheshimiwa Mbunge angetamani kuona shule hizo zote alizozitaja mara moja zinakuwa na mabweni, lakini safari ni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba tutafanya tathmini na kutambua shule zenye mazingira yanayohitaji zaidi na kuendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa mabweni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, lakini kabla ya kwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, aulize swali lake.

Na. 91

**Michezo kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza michezo kwa watu wenye ulemavu pamoja na kuzalisha wachezaji wenye ulemavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa imeendelea kuhamasisha na kuendeleza ushiriki wa watu wenye ulemavu katika michezo kwa kuandaa makocha wa michezo ya watu wenye ulemavu, kuendesha matamasha ya michezo yanayowajumuisha watu wenye ulemavu, kuendesha mashindano ya ndani ya michezo mbalimbali kwa watu wenye ulemavu, pamoja na kuwezesha ushiriki wa wanamichezo wenye ulemavu katika mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vilevile Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa imeendelea kuhamasisha uanzishaji na usajili wa vyama vya michezo kwa watu wenye ulemavu ili kusaidia katika kukuza maendeleo ya michezo kwa watu wenye ulemavu, ambapo hadi Agosti, 2026, jumla ya vyama tisa (9) vya michezo mbalimbali kwa watu wenye ulemavu vimesajiliwa ikiwemo mchezo wa soka, mpira wa kikapu, tenesi, riadha na kuogelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, swali la nyongeza.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kuwezesha michezo ya watu wenye ulemavu ila kuna changamoto ndogo ikiwemo ukosefu wa makocha wanaoweza kusaidia kizazi hiki, lakini pia matamasha ya michezo kuendelea kudorora na kushindwa kulipa ada ya kushiriki mashindano ya kimataifa kutokana na kukosa usaidizi wa Serikali na wafadhili. Mfano, timu ya tenesi mwaka huu ilishindwa kushiriki mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna ukakasi wa *wheelchair basketball,* mwaka huu sidhani kama nao wataenda kushiriki kutokana na majibu ya BMT. Swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati

gani mahsusi wa kuwaandaa na kuwawezesha wanamichezo wenye ulemavu kushiriki mashindano ya kimataifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali ina mpango gani wa kuzalisha wanamichezo wenye ulemavu tukianzia ngazi ya shule ya msingi na hata wananchi ambao wana nia nzuri ya kushiriki katika michezo ya watu wenye ulemavu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia na kuongeza chachu katika kusukuma gurudumu la kuboresha mazingira ya michezo kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie katika maswali yake yote mawili ambayo ndani yake kuna maswali saba ikiwa ni pamoja na ushiriki wa mashindano ambayo yanatarajiwa kufanyika mwaka huu. Serikali kadiri inavyozidi kupata fedha inaendelea kuweka mkazo na kuboresha mazingira kuhakikisha kwamba michezo yote ikiwemo ya watu wenye ulemavu inapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mpango wa kuhakikisha tunaendelea kutengeneza vipaji vipya kupitia shule za msingi na sekondari, ni mpango mkakati ambao tunaendelea nao kati ya Wizara zetu, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira mazuri zaidi ya kuendelea kuwatambua na kuwaibua vijana katika kipindi ambacho wanakuwa katika mazingira ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, suala la makocha ni jambo ambalo si tu kwa watu wenye ulemavu ni changamoto ambayo imekuwepo kote na hata kwenye shule zetu za sekondari tuna walimu wa michezo, lakini si walimu wenye taaluma ya michezo. Kwa hiyo, bado tunaendelea na mpango kazi kuhakikisha kwamba

tunaboresha na tunawawezesha kwa *short program* na *long program* ili kuhakikisha kwamba tunapata na kuondoa ombwe lililopo la takribani ya walimu wenye uwezo zaidi ya 10,000 katika Nchi yetu ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paul Makonda, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa sasa tunaendelea na mtiririko ulioko katika *Order Paper*; Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana na sasa ninamwita Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum ili aulize swali lake.

Na. 79

**Kupitia Upya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007**

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapitia upya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007?

**MWENYEKITI:** Majibu Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007. Kabla ya mapitio hayo, Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Sera mwaka 2022 ili kubaini mafanikio, changamoto, mapungufu na masuala mapya yaliyojitokeza katika maendeleo ya vijana. Matokeo ya tathmini na maoni ya wadau yalitumika kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, Toleo la Mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera hiyo iliidhinishwa na Baraza la Mawaziri tarehe 25 Aprili, 2024 na kuzinduliwa rasmi Jijini Dodoma tarehe 12 Agosti, 2024. Kwa hiyo, Serikali haiko katika hatua ya kupanga mapitio; mapitio yamekamilika na Toleo la Mwaka 2024 linaendelea kutekelezwa. Aidha, Serikali imeandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera wa kipindi cha mwaka 2024 - 2034, unaoainisha afua, matokeo, viashiria, muda na wajibu wa wadau. Serikali itaendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake ili kuhakikisha mahitaji na changamoto za vijana zinapatiwa ufumbuzi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na ninaipongeza Serikali kwa kazi nzuri na majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa changamoto ya dhamana ni miongoni mwa vikwazo vinavyowafanya vijana wanaofanya biashara zinazoweza kuzalisha mapato, washindwe kupata mikopo katika taasisi rasmi za kifedha, je, Serikali kupitia sera hii ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana mwaka 2024 ina mpango gani wa kuanzisha au kuwezesha mfumo wa dhamana mbadala au *guarantee schemes* maalum kwa vijana ili waweze kupata mikopo hata kama hawana mali ambazo haziwezi kuhamishika kama dhamana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. kwa kuwa Sera hii itatekelezwa mpaka mwaka 2034 kama majibu ya Waziri yalivyosemwa, wakati ambao mabadiliko ya teknolojia yanaenda kwa kasi na kufanya mabadiliko katika mahitaji ya ujuzi katika sekta ya ajira; je, Serikali ina mpango gani na ina utaratibu mahususi wa kuhakikisha inahuisha ujuzi wa vijana kadri teknolojia inavyobadilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Timida Fyandomo kwa maswali yake mazuri lakini kwa uwakilishi mzuri wa vijana katika Bunge hili Tukufu. Ni kweli kama nilivyotangulia kusema kwamba Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, Toleo la 2024, imefanyiwa maboresho na hiyo ilitokana na mabadiliko mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia ambayo yanawakabili vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kwamba sera hii iendane na mazingira ya sasa na hasa kwenye fursa zinazotokana na maendeleo ya teknolojia. Kwa hiyo, miongoni mwa maeneo makuu ambayo Sera hii inalenga ni pamoja na eneo la ajira na uwezeshaji kiuchumi kwa ajili ya kuhakikisha sasa tunakuza ujasiriamali katika kundi la vijana, lakini fursa za ajira na fursa za uchumi kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujibu sasa swali lake kwa sababu Mheshimiwa Mbunge kwa muktadha wa swali lake ametaka kufahamu kikwazo kimojawapo cha vijana kuweza kujiajiri wao wenyewe ni kutokuwa na zile dhamana zisizohamishika kwa ajili ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muktadha huo Serikali imerahisisha kupitia Sera hii, lakini kupitia mkakati wa utekelezaji wa Sera hii imehakikisha kwamba masharti ya mikopo inalegezwa na hasa kwenye eneo la dhamana. Pia, ndiyo maana juzi kushinda jana Bunge hili Tukufu limepitisha Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali Zisizohamishika wa Mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sheria hii inaenda kulegeza masharti ya kutaka kuwa na dhamana pekee zile zisizohamishika na sasa kutakuwa kuna uwezo wa watu kukopa ikiwemo vijana kukopa kwa dhamana ambazo zinahamishika. Kwenye Sheria hiyo kwenye kifungu cha 8 kimeeleza kabisa bayana kwamba mali zinazoweza

kuwekwa dhamana ni pamoja na mali inayoshikika au isiyoshikika. Kwa hiyo, kile kikwazo ambacho vijana wamekuwa wakipitia cha kutakiwa kuwa na dhamana zisizohamishika kupata mikopo sasa kinaenda kwisha kupitia Sheria hii ambayo imepitishwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari ilikuwa imeshaanza kufanya maboresho mbalimbali ya kurahisisha upatikanaji wa mikopo hii kwa vijana na hasa kwenye eneo lile la masharti ya dhamana. Kwa mfano; kwenye Mfuko ule wa Maendeleo ya Vijana *(Youth Development Fund)* mwongozo mpya ulitengenezwa ambao ulilegeza masharti ya dhamana na kutoweka lile sharti la dhamana zisizohamishika pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona katika mikopo inayotolewa katika ile ahadi ya shilingi 200,000,000,000, mikopo hii inatolewa kwa namna ya vifaa. Vijana wanapewa vifaa na vile vifaa ndiyo vinatumika kama dhamana ya mkopo husika ambao vijana wanakuwa wamepatiwa. Kwa hiyo, hiyo nayo ni jitihada ambayo Serikali inafanya kuhakikisha kwamba sharti la dhamana lisiwe kikwazo kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mikopo ile inayotolewa katika halmashauri kutokana na mapato ya ndani ya 10% hivyo hivyo masharti ya dhamana yamepunguzwa. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inatengeneza masharti mazuri zaidi na mazingira mazuri zaidi kwa vijana kuweza kupata mikopo na dhamana isiwe ni kikwazo kwa vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusiana na mkakati wa Serikali wa kuhuisha elimu yetu ili ujuzi uweze kuendana na teknolojia (vijana wapate elimu ambayo inawawezesha kuwa na ujuzi unaoendana na mabadiliko ya kiteknolojia). Sasa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007, Toleo la 2024 pamoja na mkakati wa utekelezaji wa hiyo sera ambayo ni mkakati wa miaka 10, mwaka

2024 - 2034 unatambua umuhimu wa ujuzi unaoendana na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii imelenga kwamba vijana wawe wenye ujuzi, ubunifu, ufahamu na matumizi sahihi ya teknolojia. Ndiyo maana kwa wakati huu tayari Serikali imekuja na mkakati wa kitaifa wa elimu ya kidijiti kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Lengo hapa ni kwamba vijana wapate elimu wafundishwe siyo tu teknolojia zilizopo leo, lakini waweze kufundishwa pia *emerging technologies* (zile teknolojia mpya zinazoibuka kila siku) ili mfumo wa elimu yetu uweze kuendana na teknolojia mpya. Kwa hiyo, Serikali ina mkakati huo na mkakati huo unapitiwa kila mwaka, lakini una mapitio kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa miongozo mbalimbali tofauti ya matumizi ya teknolojia katika elimu ya msingi na vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vikuu lakini pia mwongozo wa matumizi ya akili unde katika elimu. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na jitihada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo pia ninaomba nitumie nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge vijana na Watanzania wote kwamba kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuna mkakati wa Taifa wa uchumi wa kidijiti wa mwaka 2024 - 2034 ambao na wenyewe unalenga kuongeza na kutengeneza umahiri katika eneo hili la masuala ya matumizi ya kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali itaendelea na jitihada hizo zote ili kuhakikisha kwamba elimu wanayoipata vijana inaendana na wakati na inaendana na mabadiliko ya kiteknolojia ili kuwawezesha katika shughuli zao na hasa za kiuchumi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, sasa ninamwita Mheshimiwa Nadra Ghulam Rashid, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 80

**Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu**

**MHE. NADRA GHULAM RASHID** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa pamoja katika utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu ambao ni nguzo ya kubadilisha uchumi wa nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Nadra Ghulam Rashid, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mbili za Muungano zinaendelea kushirikiana katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024 na Sera ya Uchumi wa Buluu ya Zanzibar ya Mwaka 2022, pamoja na mikakati na mipango yake ya utekelezaji. Aidha, katika kutekeleza Sera hizo, Serikali zote mbili zimeendelea kutekeleza mikakati ya pamoja ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na uratibu wa masuala ya Uchumi wa Buluu, kuandaa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji *(Marine Spatial Planning)*, kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Uchumi wa Buluu, pamoja na uratibu wa mikataba, itifaki na maazimio ya kimataifa na kikanda yanayohusiana na Uchumi wa Buluu. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nadra Ghulam Rashid, swali la nyongeza.

**MHE. NADRA GHULAM RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nizipongeze sana Serikali zetu mbili kwa namna wanavyoshirikiana kutekeleza huu Uchumi wa Buluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niulize swali langu la kwanza. Ili watu wetu kushiriki vizuri katika uchumi huu wanahitaji kuwezeshwa; je, Serikali imejipangaje katika kuwapatia mitaji hususan vikundi vya akina mama wanaojiendeleza katika kilimo cha mwani pamoja na uvuvi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, tangu utekelezaji huu wa mkakati wa pamoja wa wananchi, ni wananchi wangapi wa pande zote mbili wamenufaika na mpango huu wa pamoja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Nadra Ghulam amekuwa mfuatiliaji wa masuala haya ya Uchumi wa Buluu kwa karibu sana na hususan makundi ya wanawake upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia mifuko mbalimbali imekuwa ikiwasaidia wanawake kwenye vikundi vyao au mtu mmoja mmoja ili kuwawezesha kushiriki katika fursa zinazopatikana kwenye Uchumi wa Buluu. Hivi sasa pamoja na mifuko hiyo mingine, tunao mradi mkubwa wa dola milioni 150, mradi wa mabadiliko ya tabianchi, mradi wa kijamii ambao tumeutekeleza kwenye halmashauri 65 kwa nchi nzima. Katika hizo halmashauri 65, halmashauri 11 zinatokea Zanzibar na zinashiriki katika fursa hizi za Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ametaka kufahamu ni wananchi wangapi wananufaika na fursa hizi za Uchumi wa Buluu. Suala la Uchumi wa Buluu ni suala ambalo linashirikisha sekta nyingi kuanzia sekta ya uvuvi, sekta za usafirishaji, sekta za nishati na sekta za utalii. Hivyo, ni Watanzania wengi sana wanaonufaika na suala hili la Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nitolee mfano mmoja. Sekta ya uvuvi peke yake inanufaika na sehemu ya Uchumi wa Buluu karibu Watanzania 6,000,000 wananufaika na sekta hii ya uvuvi inachangia kwenye pato la Taifa kwa asilimia 2.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nitumie nafasi hii kulifahamisha Bunge lako na kuwafahamisha Watanzania kwamba nchi yetu kwenye eneo hili la Uchumi wa Buluu imepiga hatua kubwa sana kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa 2026 Tanzania ni mwenyeji wa Mkutano mkubwa wa 12 wa Mkataba wa Nairobi. Mkutano ambao utahusisha kujadili masuala ya utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za Uchumi wa Buluu kwenye Bahari yetu ya Hindi magharibi mwa Bahari ya Hindi na utahusisha Nchi 10 ikiwemo Mauritius, Madagascar, Comoro, Ufaransa, Jibut, Kenya, Somalia, South Africa pamoja na sisi Tanzania. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Imamu Vuai, swali la nyongeza.

**MHE. IMAMU MTUMWA VUAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Je, Serikali imeweka utaratibu gani kuhakikisha fursa za Uchumi wa Buluu zinawanufaisha vijana hasa wale wanaoishi visiwani na pwani?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu

mzuri wa kuhakikisha vijana wananufaika na fursa hizi za Uchumi wa Buluu na kwa kweli imefungua fursa kwa usawa kabisa kwa vijana wote wa Kitanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunahakikisha tunawapatia elimu na utoaji wa elimu umeendelea kwa maeneo yote. Vilevile vijana hawa tunaendelea kuwahamasisha kujiunga kwenye vikundi ili waweze kupata fedha hizi tulizo nazo ndani ya Serikali kupitia mifuko mbalimbali wakaweze kunufaika na fursa za uvuvi, waweze kunufaika na fursa za kilimo kwenye ukanda wote unaoguswa na eneo linalohudumiwa na Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali imeweka utaratibu mzuri na nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kusemea sekta hii ya Uchumi wa Buluu na waendelee kuwahamasisha vijana waweze kujiunga kwenye vikundi ili wafikie fursa hizi za Uchumi wa Buluu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagwila Reuben, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Afya, sasa ninamwita Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 81

**Mpango Mahsusi wa Kuhakikisha Huduma za Afya Zinawafikia Wananchi**

**MHE. ZENA M. KATAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi kikamilifu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zena Maulid Katambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Tano wa 2021 - 2026 nguzo yake kuu ni kuhakikisha upanuzi na upatikanaji wa huduma za afya na zenye ubora kwa wote kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo likiwa ni kuwafikia wananchi wote kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeongeza bajeti ya afya kutoka shilingi trilioni 1.1 mwaka wa fedha 2022/2023 na kufikia shilingi trilioni 1.8 mwaka wa fedha 2025/2026. Jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 10,153 mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia vituo 13,683 mwezi Machi, 2026 na hivyo kuwezesha takribani zaidi ya 85% ya Watanzania kupata huduma za matibabu ndani ya kilomita tano kutoka maeneo wanakoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeajiri jumla ya watumishi wa afya 53,633 wa kada mbalimbali kwa kipindi cha kuanzia 2021 hadi Machi, 2026 ambao idadi kubwa walisambazwa katika vituo vya ngazi ya afya ya msingi ili kuimarisha upatikanaji wa huduma na hivyo kufanya idadi ya watumishi wa afya kufikia 182,430.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kuhakikisha wananchi wanamudu huduma za afya, Serikali inasimamia utekelezaji wa bima ya afya kwa wote ambapo hadi Juni, 2026, jumla ya kaya 276 sawa na 100% ya kaya maskini zilizolengwa kugharimiwa na Serikali kwa awamu ya kwanza zimesajiliwa na jumla ya wanufaika milioni 1.4 wamegharamiwa bima ya afya na Serikali. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zena Maulidi Katambo, swali la nyongeza.

**MHE. ZENA M. KATAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilomita tano, lakini kwa Mkoa wa Lindi hali iko tofauti kwa sababu mkoa una kata 152, lakini kati ya kata hizo ni kata 38 pekee ndizo zina vituo vya kutolea huduma za afya. Pia kwa upande wa zahanati mkoa una vijiji 523, lakini ni vijiji 214 pekee ndiyo vina zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonesha kwamba wananchi wa Mkoa wa Lindi wanatembea zaidi ya umbali wa kilomita hizo tano ambazo Serikali inalenga. Sasa ni upi mpango mkakati mahususi wa Serikali kwa ajili ya Mkoa wa Lindi ili kuhakikisha inajenga vituo vya afya, lakini pia na zahanati ili kusudi wananchi waweze kupata huduma za afya katika umbali huu ambao Serikali unalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali imeanza kutekeleza mpango wa huduma za afya, *I mean,* bima ya afya kwa wote ambapo kwa awali umeanza kwa wananchi wanufaika wa kaya maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha unashirikisha kikamilifu wadau wote wanaohusika na utoaji wa huduma za afya na wao nao wanashiriki kwenye mpango wa bima za afya kwa wote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge Zena kwa kazi nzuri anayofanya na hata kipekee kuwapigania wananchi wa Mkoa wa Lindi ili waendelee kupata huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza la jinsi gani Serikali imejipanga kuongeza vituo vya afya na zahanati katika Mkoa wa Lindi ambapo imeonesha kwamba kati ya kata 158, kuna

vituo vya afya 38 tu. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge moja ya kazi ya Wizara ya Afya ni kutafuta pesa kwa ajili ya kujenga vituo vya afya. Tutaendelea kushirikiana na TAMISEMI ili kupata pesa na tuendelee kujenga miundombinu kwa Mkoa wa Lindi kwa maana ya vituo vya afya na zahanati na hasa vile vituo vya afya vya kimkakati ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii 15% ya wananchi ambao wanakwenda zaidi ya kilomita tano kupata huduma ya afya ni lazima tuweze kuitekeleza. Ni lengo la Serikali ni lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan huduma imfikie mwananchi na siyo mwananchi aifuate huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, sisi kama Serikali tunashirikiana na wadau wote na watoaji huduma wote wa sekta binafsi ili tuweze kutoa huduma afya kwa wote. Kwa nini? Serikali peke yake haiwezi kutoa huduma za afya kwa wananchi wake? Ndiyo maana tunashirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vituo vya afya vya *private*, Serikali za *private* nazo zote zitahusika katika kutoa huduma ya afya kwa watu wote. Kikubwa tu ziweze kutimiza vile vigezo na masharti ambavyo tumewawekea kama ambavyo tunawekea hospitali za Serikali. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa *Eng*. Johnston Johannes Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini aulize swali lake.

Na. 82

**Uhitaji wa Jengo la Mama na Mtoto - Hospitali ya Mkoa wa Kagera**

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera. Aidha, Serikali imekamilisha usanifu wa ujenzi wa jengo hilo, kwa sasa ipo katika hatua ya mwisho za kumpata mkandarasi mjenzi na ujenzi huu unatarajiwa kuanza mapema mwezi Desemba, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Eng*. Johnston Mutasingwa swali la nyongeza.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kutenga pesa kwa ajili ya kuanza kujenga jengo hilo la mama na mtoto. Niishauri Serikali sasa huo mchakato usichukue muda mrefu kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Kagera na hasa akina mama wa Jimbo la Bukoba Mjini itakuwa msaada mkubwa katika jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza, je, Serikali imefikia wapi katika mchakato wa kuanza kujenga kitengo cha magonjwa ya mlipuko katika hospitali hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Johnston Mutasingwa kwa kazi nzuri anayofanya kwa ajili ya wananchi wake

wa Kagera na ninazipokea shukrani hizi ambazo kwa kweli kwa moyo wa dhati zinamwendea Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa kupunguza vifo vya mama na mtoto nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba majengo yote ya mama na mtoto nchini yanakwisha ili tuweze kufikia lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto kufikia vifo 70 katika vizazi hai 100,000 ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mbunge, tunakwenda kusimamia hili kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kuhakikisha kwamba wananchi wa Kagera wanapata jengo hili la mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kabisa Mkoa wa Kagera ni moja ya mikoa ambayo inaathirika sana na magonjwa ya milipuko na Serikali imetenga shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kitengo cha kupunguza magonjwa ya milipuko na jengo hili litajengwa ndani ya Hospitali ya Mkoa wa Kagera kwa sababu sasa tunaenda kufanya huduma jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutazijenga ndani ya Hospitali ya Mkoa wa Kagera na siyo kama kule Kisopo ilivyokusudiwa hapo awali kwa sababu tuna mabadiliko ya utoaji wa huduma za afya unaenda kwenye huduma jumuishi na siyo huduma pekee. Kwa hivyo, tutajenga ndani ya Hospitali ya Mkoa wa Kagera na tumetenga shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha magonjwa ya milipuko. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Chipando, swali la nyongeza.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti tulipitisha hapa pesa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kanda. Hospitali ambayo inaenda kutuletea utalii wa kimatibabu katika Nchi yetu ya Tanzania pale Kigoma Mjini. Zilitengwa shilingi 8,000,000,000 na Mheshimiwa Naibu Waziri ni mtoto wa Kigoma. Tunaomba awaambie watu wa Kigoma hospitali hii inaanza kujengwa lini ili Tanzania iweze kupata wageni kutoka Congo, Burundi pamoja na Zambia, lakini pia kuongeza kipato katika Nchi yetu ya Tanzania wewe kama mtoto wa Kigoma. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayowatendea wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali imetenga shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali ya kanda katika Mkoa wa Kigoma. Tumeshapata eneo, tumeshafanya *feasibility study* na sasa kazi hii imetangazwa ili tuweze kupata mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi huu wa hospitali ya kanda katika Mkoa wa Kigoma unakwenda kuanza mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa ya Kitete ina changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa huduma katika huduma 17 zinazotakiwa na katika hospitali hiyo tuna huduma tano pekee yake. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha wanatuongezea huduma angalau zifike hata 10 au 12 ili wananchi wetu wa Mkoa wa Tabora ambao ni zaidi ya 3,000,000 waweze kupata huduma stahiki? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Tabora kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa zipo hospitali ambazo zinatoa huduma sita ikiwemo Hospitali ya Mkoa wa Tabora, Hospitali ya Ligula, Hospitali ya Songea, Hospitali ya Mbeya na Hospitali ya Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali zote hizi ambazo zinatoa chini ya huduma sita tumeweka mpango mkakati wa kuziongezea miundombinu, lakini na wataalamu, kwa sababu lengo la Serikali ifikapo 2030 tunataka hospitali zote za mkoa ziwe na huduma 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunakwenda kuyafanya yote. Kwanza kuongeza miundombinu; pili, kuongeza vifaa; lakini na tatu, kupeleka wataalamu ili tuweze kufikia malengo ya kufikia huduma 17 ifikapo 2030. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Naibu Waziri wa Afya, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Asha Hussein Saleh, Mbunge wa Fuoni, aulize swali lake.

Na. 83

**Vigezo Vinavyotumika kwa Vijana ili Kujiunga na JKT**

**MHE. ASHA HUSSEIN SALEH** aliuliza:-

Je, vigezo gani vinavyotumika kwa Vijana ili kujiunga na JKT hususani Vijana wa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Hussein Saleh, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Mwaka 1964, Kifungu cha 3(2), vijana wa Kitanzania kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wanaomaliza kidato cha sita wana wajibu wa kushiriki mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria. Hivyo, vijana wa Zanzibar wanatambuliwa kama sehemu ya vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuwapata vijana wa Zanzibar huanza visiwani, ambapo usaili huratibiwa kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote 11 za Zanzibar. Baada ya usaili, vijana wanaokidhi vigezo huchaguliwa na kupelekwa katika kambi za JKT kwa ajili ya mafunzo. Vigezo vinazingatia umri, kiwango cha elimu, uraia, vyeti na nyaraka halisi, afya njema, uwezo wa kimwili na kiakili, pamoja na tabia na nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana wa Zanzibar anaweza kujiunga na JKT kupitia makundi mawili, yaani Kundi la Kujitolea *(Volunteers)* na Kundi la Mujibu wa Sheria. Kwa ujumla, utaratibu huu unatokana na msingi wa Kikatiba na kisheria unaohusu wajibu wa vijana wa Jamhuri ya Muungano kushiriki katika ulinzi na ujenzi wa Taifa. Jeshi la Kujenga Taifa limeanzishwa kwa msingi wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa, chini ya Kifungu cha 10 na hivyo ushiriki wa vijana unalenga kuwaandaa katika uzalendo, nidhamu, utayari wa kulitumikia Taifa na kujenga mshikamano wa kitaifa. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Hussein Saleh, maswali ya nyongeza.

**MHE. ASHA HUSSEIN SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali ya kuwapa mafunzo ya uzalendo vijana wetu. Mimi sina swali la nyongeza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Yahaya, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM USI YAHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda kuuliza swali la nyongeza; pamoja na kwamba *population* ya Zanzibar ni ndogo lakini vijana wanapata shida sana kujiunga na jeshi inapokuja wakati wa *recruitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha vijana wa Zanzibar wanapata nafasi na wao ya kutosha kuingia katika jeshi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Mariam Usi Yahaya, Mbunge wa Viti Maalum kwa swali lake la nyongeza kuhusiana na suala la vijana wa JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nirekebishe kidogo maelezo ya Mbunge kwamba vijana wa Zanzibar wanapata shida. Vijana wa Zanzibar hawapati shida isipokuwa; kilichokuwepo ni kwamba katika kujitolea kuna aina mbili kama ambavyo tumejibu swali la mama. Kuna suala la kwa mujibu wa sheria na kuna suala la kujitolea kwa utaratibu ule mwingine wa ku-*volunteer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huo liko eneo ambalo wanachukuliwa vijana wa kidato cha sita wote kama

ambavyo utaratibu kwa sasa upo. Kwa hiyo, iwe kidato cha sita hicho kiko Makunduchi, kiwe Kigoma, kiwe Kwale, Lindi, Mtwara na penginepo, ukiwa kidato cha sita na umekidhi vigezo utaingia kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa pili ambao wanachukuliwa kila mwaka, kuna idadi maalum kwa mujibu wa bajeti iliyotengwa. Kwa idadi hiyo kila mwaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata sehemu ya mgao wake kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unapitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa utaratibu uliowekwa. Hatimaye Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na baadaye kila mkoa na wilaya unapata mgao wake kwa mujibu wa *ratio* iliyowekwa Kitaifa. Kwa hiyo, ninataka nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, changamoto hiyo haipo na jambo hili linakwenda vizuri. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ayoub Mohammed, Naibu Waziri, Mambo ya Ndani, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Hamis Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki aulize swali lake.

Mheshimiwa Hamisi Taletale.

Na. 84

**Ujenzi wa Barabara ya Bigwa - Kisaki**

**MHE. HAMISI S. TALETALE** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Bigwa – Kisaki ambayo imeahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami kwenye Ilani ya CCM 2020 – 2025 itaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Bigwa – Mvuha hadi Kisaki yenye urefu wa kilometa 133 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa sehemu ya Bigwa hadi Mvuha kilometa 78 ambapo Mkandarasi ameanza kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea na usanifu wa sehemu iliyobaki ya Mvuha hadi Kisaki yenye urefu wa kilometa 55. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya swali langu. Swali la kwanza, je, ni utaratibu gani ambao Serikali utautumia kuwasaidia wananchi wa Kusini na Kusini Mashariki kupata kazi kwenye eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tunafahamu *timeframe* (muda maalum wa mkataba wa kukamilika) ni mwaka 2027 kwa *delaying* ambayo imefanyika. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kumwongezea mkandarasi huyu mkataba na tujue lini barabara hii ya Bigwa – Kisaki inakwenda kukamilika yote kwa ujumla? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, moja ya taratibu zilizopo ni kwamba kule ambako barabara inapita, utaratibu upo

kuhakikisha kwamba wale vijana, wenye uwezo wa kufanya kazi, wanapatiwa kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna tatizo kwenye hiyo barabara, kwa sababu taratibu zipo kabisa, na ziko wazi, kuwatumia Mameneja wa mikoa, na wale wasimamizi wa miradi, tungetamani kule ambako barabara inapita, basi watu ambao wanahusika, wanufaika, pia wawe ndio wa kupata kazi mbalimbali zile ambazo hazihitaji utaalamu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kuhakikisha kwamba tunakamilisha mkataba kwa muda, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulichelewa kuanza hiyo kazi, kwa sababu tulimcheleweshea mkandarasi kumpa malipo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumefanya hivyo, na kwa kuwa tuna uhakika kwamba sasa mtiririko wa fedha utakuwa mzuri, tutahakikisha tunakaa naye na kumpangia muda ambao tutakubaliana kwamba, anakamilisha sasa kwa mujibu wa mkataba na kadiri tutakavyokuwa tumemwongezea muda, ili ile barabara sasa iweze kukamilika yote kwa muda ambao tutakuwa tumekubaliana naye, baada ya kuanza ile kazi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mamlaka za Utabiri wa Hali ya Hewa Nchini, imeendelea kutufahamisha kutakuwa na mvua kubwa za *El nino*. Wilaya ya Hanang ni miongoni mwa wilaya ambazo kwa kawaida huwa zinakuwa na mvua kubwa, na kwa kuwa Waziri ameshatujulisha Mfuko wa Barabara tayari umeshaanza kupokea fedha, mimi na wananchi wa Hanang tunatamani kufahamu, ni lini ujenzi utaanza kwa kipande korofi cha Barabara ya Dareda mpaka Singida? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba kweli tumepata taarifa na kama Serikali, kwa kweli tumeendelea kujipanga kukabiliana na hali ya *El Nino* ambayo imetabiriwa kwamba inakuja. Sisi tunaosimamia miundombinu ndio tunaoathirika sana; japo ni ukweli pia kwamba zile barabara ambazo zipo kwa kiwango cha lami haziathiriki sana ukilinganisha na zile barabara za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyouliza Mheshimiwa Mbunge wa Hanang ni barabara ambayo kimsingi imechoka sana, na katika barabara ambazo zimechoka ni mojawapo. Pia, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni barabara ambayo pia imeainishwa kama barabara ya ushoroba wa kiuchumi mkubwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari wataalamu wameshapita katika hiyo barabara ambayo ndiyo tunategemea tutakapoanza kupata hizo fedha za utengenezaji wa barabara *(rehabilitation),* ni moja ya barabara ambazo zitakuwa za kwanza kabisa, kuanzia hapo Dareda hadi eneo linaloitwa Gehandu, ambapo tuna kilometa kama 82 ambazo tunakwenda kutengeneza kama kuijenga upya. Barabara hiyo mwaka huu ipo kwenye mpango ambao tayari wameanza kuandaa taratibu za kuitangaza ili mkandarasi atakayepata kazi, aanze mapema sana kuirudisha hiyo barabara ambayo ni kama tunaijenga upya kwa sababu ilikuwa imeharibika sana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea Sasa ninamwita Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mbunge wa Ikungi Mashariki, aulize swali lake.

Na. 85

**Ujenzi wa Barabara ya Handeni hadi Singida kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. THOMAS M. KITIMA** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Handeni hadi Singida itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoagizwa na Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Mkoani Tanga?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mbunge wa Ikungi Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kiteto – Mrijo – Chemba hadi Singida yenye urefu wa kilometa 424.24 kwa awamu, ambapo sehemu ya kwanza ya kutoka Handeni hadi Mafuleta kilometa 20, ujenzi unaendelea. Aidha, sehemu ya pili ya Mafuleta hadi Kileguru kilometa 30 na Kibaya – Kisima kilometa 50 wakandarasi wapo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu iliyobaki, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imeitangaza ili kupata wawekezaji watakaojenga barabara hiyo kwa utaratibu wa *PPP*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, swali la nyongeza.

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ile barabara tuna mpango wa kuijenga kwa lami, na ukiangalia kutokea Singida pale njia panda, zile alama za barabarani ama zile *beacon,* yaani yale mawe yamewekwa tu kama kilometa tatu mpaka Kijiji cha Unyankanya. Maeneo mengi hayajawekwa hayo

mawe ya kuzuia ama kuonesha kingo za barabara ama hifadhi ya barabara, na wananchi wanaendelea kutumia barabara kwa shughuli mbalimbali, na wengine wanajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kwamba itafika wakati itapata mzigo mkubwa wa kulipa fidia kwa sababu wananchi wanaendelea kujishughulisha na shughuli za kiuchumi, ilhali bado hazijawekwa hizo *beacon* za kuzuia watu wasiendelee kujenga? Lini Serikali itaweka hizo alama ama hayo mawe ya kuzuia shughuli nyingine zisiendelee? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuanza kuweka mkandarasi katika Kijiji cha Unyankanya ili na yeye arudi huku, waje wakutane na hawa ambao wameanzia huku Handeni, kama alivyosema Waziri kwamba, tayari kule kuna wakandarasi, lakini na huku pia hiki kipande cha Unyankanya, Makyungu, Mungami, Sughaa nacho pia mkandarasi aanzie huko, ili kuwatoa adha hawa wananchi wa Jimbo la Ikungi Mashariki? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mbunge wa Ikungi Mashariki kwa kuona kwamba kuna haja kubwa ya kulinda barabara na hasa sharoba za barabara ikiwa ni pamoja na kuweka *beacon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na niwaagize Mtendaji wa *TANROADS* pamoja na Meneja wa Mkoa wa Singida, kwa ukubwa wa barabara hii ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna haja kubwa ya kuweka alama za kuonesha hifadhi ya barabara ambapo itapita, ili wananchi wasiendelee kufanya shughuli zao za kijamii ambapo mwisho wa siku itapelekea kulipa fidia kubwa ambayo siyo ya lazima, lakini pia kuwasumbua wananchi ambao watakuwa tayari wanaendesha maisha yao katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hilo tutalifanya na kupitia Bunge hili, ninamwagiza Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba hilo analisimamia na linafanyika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rai yake ya pili, kwamba kuna haja ya kuanza barabara upande mwingine; hii barabara ni ndefu sana na hata wakati tulikuwa na mpango wa zamani, ilikuwa tuikate kwenye vipande. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakapokuwa tumepata huyu mtu ambaye tutafanya naye kazi na hii barabara, bahati nzuri ilikuwa pia ni maagizo ya Mheshimiwa Rais kwamba tujenge kwa utaratibu wa *PPP* na taratibu zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii itakatwa kwenye vipande vipande ambapo siyo tena itatokea upande mmoja wa Tanga, nina uhakika watakuwa na vipande pengine zaidi ya vitatu ikiwepo na upande wa kuanzia Singida kuja huku. Hilo tuwaachie hawa wakandarasi ambao tutawapata na nina hakika tutaanzia pia upande wa Singida kuelekea upande wa Tanga ili tuone kwamba wanafanya kazi kwa haraka inavyowezekana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ndogo ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ambazo zimekuwa zikiunganisha wilaya kwa wilaya na vilevile, *shortcut* katika maeneo mengi ya nchi hii ni barabara ambazo ninajua kwamba Serikali inafahamu umuhimu wake. Barabara ya kutoka Igunga – Igulubi - Ukenyenge kutokea Kolandoto kwenye Jimbo langu la Kishapu ni barabara ambayo ingesaidia sana wakazi wote na wananchi wote wa Kanda ya Ziwa, kwa sababu ilikuwa ni *shortcut* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa nini Serikali licha ya kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya, Wizara haizingatii barabara hii kuiweka kwenye mpango, ili iweze kusaidia wananchi badala ya kutoka

Igunga kwenda Nzega kuja Shinyanga wananchi wanaweza wakapita *shortcut* kwa kutumia barabara hii, na umuhimu wake wanaujua? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara zote za *TANROADS* kwa kawaida kama uchumi ungekuwa umekaa sawa kabisa, lengo ni kuzifanya ziwe barabara za kiwango cha lami. Zile ambazo bado hatujaziweka kwenye mpango, tunachohakikisha ni kwamba zinatengenezwa na zinapitika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge ili Mkoa wa Shinyanga waweze kuitembelea hiyo barabara na kuitolea mapendekezo kama ni barabara ambayo inahitajika sana kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na hasa Kishapu, ili tuweze kuingiza kwenye mpango kwamba, katika mipango yetu ijayo, basi hiyo barabara iweze kuingizwa katika mipango ya kusanifiwa na kujenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nitakaowapa nafasi ya maswali ya nyongeza ninaomba tuulize kwa kifupi na Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu kwa kifupi. Mheshimiwa Ester Bulaya, jiandae Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Lengo kuu la Serikali kujenga barabara zinazounganisha mikoa ni kutanua shughuli za kiuchumi, ili wananchi waweze kufika kwenye maeneo kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejenga barabara nyingi lakini kuna changamoto ya barabara kuharibika; hizo za kimkoa kutoka hapa Dodoma kwenda Singida, kutoka Mwanza kwenda Mkoa wa Mara, kutoka Simiyu kwenda Shinyanga kupitia Lamadi, kutoka Njombe kwenda Ruvuma, na kutoka Dodoma kwenda

Iringa. Nini mkakati wa Serikali kuwa na fungu maalum la ukarabati ili kuhakikisha barabara hizi zinapitika muda wote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda kwa swali lake zuri. Katika bajeti tuliyoipitisha, moja ya ajenda kubwa ambayo Waziri wa Ujenzi alielezea, na hata Waziri wa Fedha, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ilikuwa ni uchakavu wa barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tulikuja na hoja, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, leo kati ya Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha yapo maendeleo mazuri sana ambapo tunahitaji fedha nyingi. Nina hakika ndiyo maana tulikuja na mipango mingi ambayo tunayo mpaka dakika hii, hizi barabara ziweze kujengwa na ikiwepo hata na ile barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge wa Hanang ameisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ni barabara za kiuchumi, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pengine baada ya kukamilika kwa mpango, pengine Waziri atakuja kuelezea mpango wa ku-*rehabilitate* hizo barabara zote ambazo amezitaja Mheshimiwa Ester Bulaya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Makofia Mlandizi imefungamanishwa na mradi wa ujenzi wa bandari na eneo la viwanda la Kwala, je, Serikali mpaka sasa hivi imefikia hatua gani ya maandalizi ya kulipa fidia ya wananchi wanaopitiwa na barabara hiyo wa Kata ya Yombo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Fidia ya wananchi aliowataja kama Wizara, tulishakamilisha tathmini na tulishapeleka Wizara ya Fedha. Nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo barabara sasa hivi imekuwa ni muhimu sana kwa sababu, sasa hata kule ile tunayosema Bandari ya Bagamoyo ninadhani muda siyo mrefu itakwenda kuwa *live*. Kwa hiyo, ni muhimu hiyo barabara ikajengwa. Kwa hiyo, taratibu zinaendelea, tutakapokuwa tumepata fedha, hao wananchi tutawalipa ili barabara hiyo iweze kujengwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Same – Mbaga - Mamba hadi Ndungu ni barabara ambayo iko milimani na barabara hii inachochea uchumi wa wananchi wa Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami kama ambavyo Mheshimiwa Rais ametoa ahadi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoisema ya Same – Ndungu tayari sasa hivi tuko kwenye usanifu, ilikuwa haijasanifiwa. Kwa hiyo, sasa hivi tunaendelea na usanifu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya aulize swali lake.

Na. 86

**Ujenzi ya Barabara ya Utegi - Shirati kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Utegi – Shirati kilometa 27 kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Utegi – Shirati – Kirongwe kilometa 64.96 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Mika – Utegi - Bukama kilometa 27 ambapo zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi imepangwa kutangazwa upya katika mwaka wa fedha 2026/2027 kutokana na zabuni ya awali kukosa mzabuni mwenye sifa na vigezo vya kujenga barabara hiyo. Baada ya kukamilika kwa hatua ya ununuzi, kazi za ujenzi zitaanza. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa barabara hii tayari ilishapata kibali toka mwaka wa fedha uliopita, Mheshimiwa Rais kwa mapenzi ya wananchi wa Rorya aliridhia barabara ile itangazwe na ianze ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maana ya kwamba haiombewi tena kibali, tayari kibali kilishatoka mapema mwezi wa Saba kupitia ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akiongozana na Mheshimiwa Naibu Waziri. Tuliwaahidi wananchi kupitia viwanja vile kwamba, barabara ile inatangazwa kuanzia mwezi wa Saba uliopita na ianze mara moja ujenzi kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, lakini mpaka leo ni mwezi wa Tisa barabara ile haijatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri amesema itatangazwa mwaka huu wa fedha 2026/2027 ambao kimsingi ni mrefu. Inaweza ikatangazwa 2026/2027, inaweza ikawa mwezi wa Tano mwakani au mwezi wa Saba mwakani, tofauti na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoahidi kwa wananchi wale kupitia viwanja vya shirati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate *commitment* ya Serikali, ni lipi sasa wananchi waondoke nalo? Ni hili la Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba barabara hii itatangazwa kuanzia mwezi wa Saba, mwezi wa Nane au ni ndani ya mwaka mzima kwa maana ya kwamba itakwenda mpaka mwakani mwezi wa Sita au mwezi wa Tano au mwezi wa Nne, kwa sababu imekaa kiujumla sana? Mheshimiwa Waziri, ninataka nipate *commitment* juu ya hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka nimhakikishie Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Chege, kwa uhakika kabisa kwamba ni kweli kama alivyosema kwamba mwaka wa fedha ni miezi 12. Barabara hii tunaitangaza upya mwezi huu wa Tisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Barabara ya kutoka Tarime Mjini mpaka Mugabiri, kutoka Nyamwaga mpaka Nyamongo, na kutoka Nyamongo mpaka Serengeti ina hali mbaya, na mvua zinakaribia kunyesha, na Mheshimiwa Waziri ameenda pale mara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atoe matumaini kwa wananchi wa maeneo niliyoyataja kwa ajili ya barabara yao muhimu kiuchumi, kiusalama na kiutalii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijampata vizuri sentensi yake ya mwisho Mheshimiwa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema barabara ya kutoka Tarime Mjini mpaka Mugabiri, barabara ya kutoka Nyamwaga mpaka Nyamongo na barabara ya kutoka Nyamongo mpaka Serengeti Mugumu, ni barabara ambazo zilipata wakandarasi wakaondoka *site*. Hali ya barabara hizi ni mbaya. Sasa nini kauli ya Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya wananchi wa maeneo haya kupata matumaini ya barabara yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ni barabara moja lakini ina *lot* ya Tarime hadi Mugabiri, Mugabiri – Nyamongo, na Nyamongo hadi Mugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya barabara za wakandarasi ambazo zilikuwa zimesimama, ni hizo *lots* tatu. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama Serikali tulivyosema, mwaka huu utakuwa ndiyo mwaka ambao kwa kweli wakandarasi wote ambao ama walikuwa wamesimama, ama walikuwa wanasuasua, ama hawajalipwa fedha ya awali kwa maana ya *advance*, tunakwenda kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tutalifanya katika barabara ya kutoka Tarime hadi Mugabiri, Mugabiri hadi Nyamongo na Nyamongo hadi Mugumu. Tumeshaanza kufanya hivyo na katika Mkoa wa Mara kwa sasa tayari Watu wa Sanzate – Nata tumeshawapelekea fedha kama kuanza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba Bunungu, Mbunge wa Peramiho, aulize swali lake.

Na. 87

**Ujenzi wa Barabara kutoka Likuyufusi - Mpitimbi – Mkenda**

**MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kutoka Likuyufusi – Mpitimbi – Mkenda kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba Bunungu, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Likuyufusi – Mpitimbi hadi Mkenda yenye urefu wa kilometa 122.5 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza ya Likuyufusi – Muhukuru, urefu wa kilometa 60, taratibu za malipo ya awali kwa mkandarasi zinaendelea ili kumwezesha kuanza kazi za ujenzi. Kwa sehemu iliyobaki ya Muhukuru – Mkenda kilometa 62.5, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa tena nafasi. Ujenzi wa barabara hii unahusisha barabara ya zamani kwa maana ya *existing center line,* lakini kandokando ya barabara hii kuna makazi ya wananchi, pia na miundombinu mingine. Sasa, miundombinu hii ilifanyiwa tathmini kwa ajili ya maandalizi ya ulipaji wa fidia ili kabla ya ujenzi huu kuanza, wananchi wale wawe wameshalipwa fidia. Hivyo kupisha eneo lile kwa ajili ya ujenzi kuanza na kupunguza malalamiko ya

wananchi dhidi ya Serikali yao. Je, ni lini sasa Serikali itaanza ulipaji wa fidia katika kipande hiki cha kwanza ili kuruhusu ujenzi uweze kufanyika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kwamba tunapokwenda kujenga barabara na hasa kama kuna wananchi ambao wanapisha barabara, mali zao pamoja na miundombinu kama ipo, iwe ya Serikali, tunatakiwa tuifidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna mambo mawili tunafanya. Kama fedha ya ujenzi itaanza, tutaanza maeneo yale ambayo hayahitaji fidia wakati tunatafuta fidia. Pia, tunatafuta fidia ili tuweze kuwalipa ili ikiwezekana tuanze barabara yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia hatutamwondoa mwananchi kabla hatujamlipa fidia lakini pia tukipata fedha ya kuanza, tutaanza maeneo yale ambayo hayahitaji fidia ili wale wananchi wakati wanaondoka wawe tayari wameshalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Likuyufusi – Muhukuru ni kati ya barabara ambazo ninajua zinaunganisha nchi na nchi, na Wanaruvuma wanasema, ndiyo barabara pekee ambayo inaunganisha nchi na nchi, lakini bado ni ya vumbi. Kwa hiyo, tunalizingatia sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Ujenzi, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, sasa ninamwita Mheshimiwa Mohamed Khalfan Issa, Mbunge wa Pandani, aulize swali lake.

Na. 88

**Kuachana na Matumizi ya Mbwa katika Ukaguzi wa Meli za Usiku**

**MHE. MOHAMED KHALFAN ISSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaachana na matumizi ya mbwa katika ukaguzi wa abiria na meli za usiku Bandari ya Dar es Salaam kwa kuwa unakiuka misingi ya baadhi ya dini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Khalfan Issa, Mbunge wa Pandani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*, inalo jukumu la msingi la kufanya ukaguzi wa kina wa watu, mizigo na vifurushi vinavyopita katika maeneo ya gati za abiria *(Passenger Terminal)*, *Azam Sea Link*, na *Lighter Quay* kwa ajili ya kudhibiti usafirishaji wa bidhaa haramu zikiwemo dawa za kulevya kupitia maeneo hayo na masuala ya usalama wa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi unaofanywa ni wa kawaida kwa kutumia midaki *(Scanners)* na pale kunapojitokeza mizigo na vifurushi vinavyotiliwa mashaka, ndipo mbwa wa ukaguzi huombwa kutumika na ukaguzi unaofanywa hauhusishi watu na mizigo/vifurushi vyenye chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, jitihada zinafanywa ili kuongeza idadi ya midaki zaidi ya ile mitatu iliyokwishanunuliwa ambapo, midaki miwili imefungwa eneo la *Passenger Terminal* na mdaki mmoja katika eneo la *Lighter Quay*. Midaki mingine miwili

zaidi inatarajiwa kufungwa katika eneo la *Azam Sea Link* kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi wa watu na mizigo. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Khalfan, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED KHALFAN ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu ya Serikali ya swali langu la msingi, ninakushukuru sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bandari ya Dar es Salaam, wasafiri wengi wanaotumia meli za *Azam Sea Link* ni ndugu zetu Watanzania wa Unguja na Pemba, ambao mizigo yao ikinuswa na mbwa inaondoa tohara ambapo ni kinyume na imani ya Dini ya Kiislamu. Sasa, utaratibu huu wa ukaguzi kwa njia hiyo unaofanywa na Serikali, utaendelea hadi lini, kwa kuwa utaratibu huu unakiuka misingi ya imani ya dini na pia wananchi wanalalamikia sana mtindo huu? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ikiwa tatizo ni uwezo wa kununua *scanner* na uwekaji, je, anaweza kuliambia Bunge hili kwamba *scanner* inayohitajika pale inagharimu kiasi gani cha fedha za Kitanzania kwa kununuliwa kwake? Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mohamed Khalfan Issa kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya Bandari yetu ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na usafirishaji na usafiri, akiwa amejikita kwenye upande wa mfumo bora tunaotumia katika ukaguzi wa mizigo na abiria katika Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba kipaumbele chetu cha kwanza katika Bandari ya Dar es Salaam na bandari zote ni usalama. Utaratibu unaotumika kwa sasa ni kutumia *scanners* katika kufanya ukaguzi. Tunatumia

mbwa pale inapojitokeza mashaka kwenye mizigo fulani fulani. Hiyo ni kwa mujibu pia wa sheria *(PGO)* kwa maana ya Sera ya Jeshi la Polisi, inayoruhusu kutumia mbwa kufanya ukaguzi pale ambapo mnaona kuna mashaka, na kwenye utaratibu wa kawaida usingeweza pengine kung'amua changamoto iliyopo. Tunafanya hivyo katika kufanya ukaguzi katika masuala ya doria na kutambua milipuko. Lengo ni kuimarisha usalama kwenye bandari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamkumbusha Mheshimiwa Mbunge, kwamba ukaguzi huu unaofanyika siyo tu Tanzania, ni duniani kote. Nchi zote zinafanya hivyo, kwenye viwanja vya ndege, bandari, mipaka, mikusanyiko mikubwa na hata kwenye viwanja vya michezo kama mipira. Lengo ni kudhibiti usalama. Pale tunapohisi kwamba kuna mashaka, tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa mashaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita haishindwi kununua *scanners* kwa ajili ya ukaguzi. Ndiyo maana tumeeleza hapo awali kwamba tumeshafunga midaki miwili eneo la *Passenger Terminal* pamoja na mdaki mmoja eneo la *Lighter Quay*. Pia, tunakwenda kuongeza midaki miwili, au tuseme *scanners* mbili, kwa ajili ya eneo la *Azam Sea Link*. Hivyo, hiyo siyo changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, awaelimishe pia wananchi wenzetu waelewe dhamira ya kufanya hivyo. Aidha, ninatoa pia wito kwa wenzetu wa bandari kwamba, kukagua kwa kutumia mbwa siyo utaratibu wa kawaida wa kila siku, ni pale tu kunapokuwa na mashaka. Kwenye utaratibu wa kawaida ukaguzi wa kawaida uendelee. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, Mbunge wa Butiama, aulize swali lake.

Na. 89

**Ukarabati wa Skimu ya Umwagiliaji ya Buswahili**

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati au kujenga upya Skimu ya Umwagiliaji ya Buswahili yenye ekari 500 ili wakulima waendelee na kilimo cha mpunga katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba sasa nijibu swali Na. 89 kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, Mbunge wa Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kilimo kinaendelea kwa mwaka mzima kwenye Skimu ya Umwagiliaji ya Buswahili iliyopo Wilaya ya Butiama, Kata ya Buswahili, yenye eneo la ukubwa wa ekari 500 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa Skimu ya Buswahili ambapo utekelezaji wake umefikia 35% na kuendelea kunufaisha wakulima 292 katika Kijiji cha Buswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaofanyika utawezesha kutambua gharama za ukarabati. Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa skimu hiyo ili wananchi waendelee na kilimo cha mpunga kwa lengo la kujipatia kipato. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Mahera, maswali ya nyongeza.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ninaishukuru Serikali na Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo tumeyapata. Ninaendelea kuishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu hasa ya masuala ya kilimo na umwagiliaji. Pia, ninaishukuru Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kazi nzuri inayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina swali la ziada, lakini ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, kama itawezekana ni vizuri pia akafika kwenye eneo hilo ili aweze kujionea jinsi ambavyo matope yamejaa kwenye bwawa hilo kwa sababu lilijengwa mwaka 1998. Japo sasa tunashukuru sana kwamba upembuzi yakinifu na usanifu umeanza, nina imani kubwa kwamba Serikali hii sikivu inakwenda kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa skimu hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru. Nina imani maoni hayo umeyapokea. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyapokea na ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Maji. Sasa ninamwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, aweze kuuliza swali lake.

Na. 90

**Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kwa Vijiji 33 vya Tarafa ya Chamriho**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini utekelezaji wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria katika Vijiji 33 vya Tarafa ya Chamriho utaanza ambapo tathmini na usanifu umeshafanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea kote nchini ili ianze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi kabla ya kuanza ujenzi wa miradi mipya. Kwa upande wa Wilaya ya Bunda, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi nane ikiwemo miradi inayojengwa katika Maeneo ya Hunyari, Nyamuswa, Kabainja – Ragata, Kinyambwiga, Mariwanda Awamu ya II sanjari na ukarabati wa Skimu ya Maji ya Mugeta – Nyangaranga. Utekelezaji wa miradi hii utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 12.4 na kukamilika kwake kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wapatao 67,282.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika vijiji 33 vya Tarafa ya Chamriho tathmini na usanifu umekamilika, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali inaendelea na jitihada za utafutaji wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 104 ili kuendelea na hatua za kuanza ujenzi wa mradi huo mkubwa. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninawapongeza Wizara ya Maji kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu, wamehangaika sana na Jimbo la Bunda. Sasa mimi nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amekuja sana kwenye jimbo lile. Kuna mradi wa shilingi bilioni nane wa kutoka Butiama kuja Nyamuswa. Mradi ule ilikuwa umalizike mwezi wa 12

mwaka 2025, haukumalizika. Mwezi wa Pili haujamalizika, mpaka sasa umegota. Pia kuna mradi wa Hunyari wa shilingi milioni 830, nao umegota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba kujua yuko tayari sasa kuita wataalamu wake wa mkoa na wilaya na sisi Watu wa Bunda tukakutana naye na Wizara ili tuone miradi ya Bunda itaishaje kwa sababu kuna uhaba mkubwa wa maji kwenye Jimbo la Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Boniphace Getere kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Wanabunda na kwa namna ambavyo anazidi kufuatilia utekelezaji wa mradi huu ambao ni uwekezaji mkubwa ambao unatokana na maombi yake mwenyewe kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndiyo maana tukaidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 8.3 kama alivyosema, ambapo ni kuyatoa maji kutoka Butiama kuja mpaka pale Nyamuswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunao mradi mwingine wa shilingi milioni 830 ambao unaendelea kama alivyosema, ambapo ni juhudi zake mwenyewe ambazo ameendelea kuwasemea wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kweli kabisa utekelezaji wa mradi huu unaendelea vizuri na sasa umefikia 60%. Tunayo matanki mawili, tanki la lita 300 na tanki la lita 200,000, yanaendelea na yapo katika hatua nzuri. Pia, tuna ile *gravity main* ambayo tayari imeshajengwa kilometa 16.7 ambapo bado meta 200 kufikia kwenye tanki lenyewe. Sambamba na hilo, tuna kilometa 16.1 kwa ajili ya *distribution network*, ambapo tunaamini kabisa kwamba tunaenda kuukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyokuwa imejitokeza ni kwamba mradi haujakamilika kama ilivyotarajiwa, na tunatambua

kwamba ndiyo kiu ya Mheshimiwa Mbunge. Hii ni kwa sababu ya *supplier* wa mabomba ambapo uzalishaji wa mabomba umekuwa na changamoto kwa sababu ya *material* yanayotumika katika kuzalisha haya mabomba. Kwa hiyo, kumekuwa na *delay* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewapa *extension* ambapo tunatarajia Desemba, 2026, tutahakikisha kwamba mradi huo unaanza kutoa huduma iliyokusudiwa, lakini ninakubaliana na ombi la Mheshimiwa Mbunge, tutawaita. Kwanza kabisa, tutamwita mkandarasi ambaye ni *GAT Engineering,* na *supplier* ambaye ni MOLI, pamoja na *DM* na *RM* kwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunda ambao wanaguswa na mradi huu ili tuweze kuweka mkakati ili na *supplier* na yeye atoe *commitment* kwa maandishi kwamba ataweza ku-*supply* mabomba kwa wakati ili mradi uweze kwenda kukamilika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wambura, swali la nyongeza. Mheshimiwa Chacha Wambura, hayupo. Mheshimiwa Kafiti Kafiti, swali la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Mwanza na Wilaya ya Ilemela ni moja ya maeneo ambayo yamebarikiwa kuwa na vyanzo vya maji kupitia Ziwa Victoria, lakini ukiangalia leo Wilaya ya Ilemela, licha ya kuwa imezungukwa na maji kwa 75% bado ina shida ya maji. Tuna mgao mkubwa sana wa maji na ni aibu kwa Mkoa wetu wa Mwanza. Nini kauli ya Serikali kuhusu kuondoa mgao huu wa maji katika Wilaya ya Ilemela na Mkoa wa Mwanza kwa ujumla? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kafiti Kafiti, Mbunge mahiri kutoka Jimbo la Ilemela. Kimsingi, Jiji la Mwanza kwa ujumla wake kwa majimbo ya Ilemela pamoja na Nyamagana ni kitovu cha uchumi wa Kanda ya Ziwa. Tunafahamu kabisa kwamba kuwepo kwa mgao inakuwa ni

changamoto katika kuhakikisha kwamba tunachochea uchumi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ameliomba na amelifuatilia sana, Mheshimiwa Rais ametoa idhini ya kuanza kufanya *extension* ya chanzo chetu cha *Capri Point* ambapo kwa maombi ya Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela na Mbunge wa Nyamagana, tumeweza kupata shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kuanza. Kwanza, ni kuongeza uwezo wa uzalishaji wa chanzo kile lakini pia kuongeza mtandao ili ufike mpaka Ilemela kwa wananchi ambao wanatarajia kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, huu ni utatuzi wa muda mfupi. Kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Jiji la Mwanza pamoja na Mbunge Mheshimiwa Kafiti, tumekubaliana tuanze kufanya *feasibility study* ili tukaangalie namna ya kutumia maji kutokana na chanzo cha Kabangaja, ambapo tunaamini kwamba hilo ndilo litakuwa suluhisho la kudumu katika Jimbo la Ilemela, Jimbo la Nyamagana na viunga vyote katika Jiji la Mwanza. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imetatua changamoto hiyo na uchumi wa Mwanza utaendelea kukua bila kuwa na changamoto yoyote. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. *ENG.* CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuwa na mradi wa miji 28 pale Geita, ambapo mradi ule ni mkubwa na utaenda kuondoa tatizo la maji pale Geita. Sasa swali langu ni kwamba, ninataka *commitment* ya Serikali, ni lini hasa mradi huu utakamilika ili watu wa Geita waweze kupata yale maji yaliyokusudiwa, hasa ikijulikana kabisa kwamba Geita *water table* yake ipo mbali, kiasi kwamba visima vingi vinavyochimbwa huwa havipati maji na kuna tatizo kubwa la maji? Sasa Serikali inawaambiaje watu wa Geita, ni lini hasa huu mradi utakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Chacha, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Chacha kwa kuendelea kuwasemea wananchi wa Jimbo lake la Geita. Pia, sisi Wizara ya Maji tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza mradi mkubwa wa kimkakati katika Wilaya na Mkoa wa Geita ambao unatoka Geita unaenda mpaka Chato, lakini tunafahamu kwamba utasaidia mpaka kule kwenye jimbo la Mheshimiwa Musukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ni kwamba mradi huu, tumeshamaliza *civil works*, upande wa *intake* iko katika hatua nzuri, upande wa *WTP (Water Treatment Plant)* iko katika hatua nzuri, sasa kilichobaki tuko kwenye *electromechanical installation*. Tunaamini kwamba baada ya kukamilisha *electromechanical installation* sasa tutaenda kwenye *testing* ili tuweze kuona maji yanaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, maelekezo ya Serikali ni kwamba, hatutasubiri kila kipengele kikamilike. Pale ambapo inawezekana maji kuanza kutumika yaanze kutumika, wananchi waanze kupata maji bila kusubiri mradi uweze kukamilika kwa ukamilifu zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Copriano, swali la nyongeza.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza ninaishukuru sana Wizara ya Maji kwa ule mradi mkubwa ambao ni wa vijiji 13 na vijiji saba, unaendelea vizuri. Nilikuwa na swali dogo tu kwamba, ni lini sasa Wizara itakwenda kufanya ukarabati kwenye Bwawa la Naalarami, Moita, Ngoisusi na Nguvukazi yaliyopo Mswakini ili angalau basi mvua itakaponyesha wananchi wapate maji kwanza kwa kupitia mabwawa hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Copriano Kadogoo, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Copriano kwa sababu jana tumeweza kuwasiliana, tumeongea, lakini ameongelea kuhusu ule mradi na uzalishaji wa mabomba kutoka kwenye kiwanda cha *Pipe Industry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, tumeshalipokea, tumeanza kulifanyia kazi ili mabomba yaweze kukamilika. Kwenye suala hili kulingana na taarifa tulizonazo za utabiri wa hali ya hewa, kwamba inawezekana kukawepo na mvua ambazo zitakuwa na madhara makubwa sana, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninamwelekeza Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji ambaye anahusika na masuala ya mabwawa yote, akafanye tathmini na kuchukua hatua haraka kabla ya fedha ambazo zimeshawekezwa pale kupotea kabisa, kwa sababu tunaamini kwamba kila uwekezaji lazima uwe na tija na kila uwekezaji lazima ulindwe kwa sababu ni fedha za Watanzania ambazo wamezitoa. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninatambua uwekezaji wa Serikali kwenye mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria wa Tarime – Rorya wa takribani shilingi bilioni 134. Kwa kuwa zaidi ya 55% ya wananchi wa Tarime Mjini hawana maji na mradi huu ulitarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026 lakini hadi sasa upo 18% tu na fedha ambazo zimetolewa ni shilingi bilioni 27; Na kwa kuwa mkandarasi alisha-*raise* fedha shilingi bilioni nane mpaka sasa hivi hajapelekewa ili arudi *site* na Bunge lililopita la bajeti; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, ninafahamu sasa hivi tumebadilisha fedha zinatoka Hazina zinakuja moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kujua, Serikali inawaambia nini wananchi wa Jimbo la Rorya, Tarime Mjini na Tarime Vijijini, kwamba mradi huo unaenda kukamilika lini? Kwa sababu ni mradi wa miji 28, wenzetu wako 78%, mpaka 80%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini. Nimwambie tu kwamba dhamira ya Serikali kwanza ni kuwaona watu wake wanapata majisafi na salama. Baada ya hapo tunafanya *needs assessment* kuona kuna mahitaji gani katika eneo husika ili tuweze kupata mradi. Haya yote yameshafanyika na ndiyo tukaja na suala la kuwekeza zaidi ya shilingi bilioni 134.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunafahamu kwamba mradi huu umechelewa kwa sababu ya fedha. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge amesema vizuri sana kwamba sasa tumepatiwa dirisha la kupata fedha za tozo za moja kwa moja kutoka kwenye makusanyo ya tozo ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu na nimtoe wasiwasi kabisa pamoja na wananchi wake wa Tarime Mjini kwamba dhamira ya Serikali iko pale pale kuhakikisha wanapata haya maji. Tutaenda kutekeleza hatua kwa hatua kwa sababu miradi inayoendelea ni mingi na mahitaji ya fedha ni makubwa, lakini lazima tukubaliane kwamba tutakuwa tunaweka awamu kwa awamu mpaka utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kabla ya kusubiri mradi huu mkubwa wa shilingi bilioni 134 kukamilika, tutachukua hatua za dharura katika Jimbo la Mheshimiwa Esther Matiko ili tuweze kuangalia vyanzo ambavyo vinaweza kutusaidia katika maeneo mengine na kata nyingine ambazo hazina maji kwa kuchimba visima vya dharura ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wa Jimbo la Tarime Mjini, jimbo la watu makini kabisa,

wanapata huduma ya maji safi na salama kwa sababu sauti yao imesikika na sisi tutaweka kipaumbele kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Andrea Kundo, Naibu Waziri wa Maji, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Sasa ninamwita Mheshimiwa Devota Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake, Mheshimiwa Kiza Mayeye.

Na. 92

**Kufufua Viwanda Vilivyokufa Morogoro**

**MHE. KIZA H. MAYEYE K.n.y. MHE. DEVOTA M. MINJA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda vilivyokufa Mkoani Morogoro ili kutoa ajira kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Devota Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kufufua viwanda vilivyokufa nchini ambapo kwa sasa inaendelea kufanya tathmini na ufuatiliaji wa viwanda vyote vilivyokufa vikiwemo viwanda vya Mkoa wa Morogoro. Aidha, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, viwanda ambavyo vimeshindwa

kuendelezwa, vinaendelea kupatiwa wawekezaji wapya au taasisi zenye uwezo wa kuviendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kiwanda cha *Mang'ula Mechanical & Machine Tools* kilichopo Wilayani Kilombero Mkoani Morogoro kimekabidhiwa kwa Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* ili kifufuliwe na kuendelezwa. Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi kuwekeza kwenye viwanda vipya na kufufua vya zamani. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiza Mayeye, swali la nyongeza.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Katika Mkoa wa Morogoro viko viwanda ambavyo mpaka sasa vimetelekezwa na watu wamefikia mahali wanafugia mbuzi katika viwanda hivyo. Ninataka kauli ya Mheshimiwa Waziri, ni lini Serikali itachukua hatua kwa watu wote ambao wanahujumu viwanda ambavyo vingeweza kuwasaidia vijana katika ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ndani ya Jimbo la Kigoma Kaskazini tuna fursa nyingi sana kama kilimo, ambapo tungeweza kuanzisha viwanda ambavyo vingetoa ajira kwa vijana, lakini mpaka sasa hatuna viwanda kabisa. Nini kauli ya Serikali kwa Wanakigoma Kaskazini kuhakikisha tunapata viwanda ili vijana waweze kutoka katika dimbwi la umasikini na kupata ajira? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilibinafsisha viwanda hivi kwa nia njema na lengo lilikuwa ni kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa Taifa katika sekta ya uzalishaji kupitia viwanda. Nia hii njema ya Serikali ina mafanikio makubwa kwenye baadhi ya maeneo, lakini ninakiri kwamba kuna baadhi ya maeneo kuna changamoto za uendeshaji wa viwanda hivyo, ikiwemo Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali kupitia Msajili wa Hazina imefanya zoezi la tathmini kupitia viwanda vyote vile ambavyo vimesimamisha uzalishaji na vile ambavyo vinaendelea na uzalishaji na vile ambavyo vina changamoto ya kiuendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto ambazo tumeziona kupitia tathmini hiyo ni ukosefu wa mitaji ya kuendesha viwanda hivyo; teknolojia duni ya mitambo na mashine kwenye viwanda hivyo; kutokuwepo usimamizi madhubuti wa uendeshaji wa viwanda hivyo; na pia kutokuwepo kwa malighafi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kukaa na hao ambao wana changamoto ya uzalishaji kuona Serikali inawasaidia vipi kuendesha viwanda hivyo, lakini wale ambao wameshindwa kabisa, nia ya Serikali ni kuvirejesha viwanda hivyo na kuvitangaza upya kupitia *TanTrade*, Balozi zetu na *NDC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kutafuta wawekezaji wapya ili viwanda hivyo virudi kwenye mfumo wa uzalishaji kuongeza tija na pia kutekeleza Dira ya Maendeleo ya 2020 – 2050, ambayo inajikita kwenye kuongeza thamani ya mazao yetu na pia kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuhusiana na Kigoma. Mkoa wa Kigoma ni mkoa wa kimkakati na Serikali inauangalia Mkoa wa Kigoma kama mboni ya jicho lake. Moja ya mikoa ya kipaumbele kwetu Serikali ni Mkoa wa Kigoma na ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge anaweza kuwa shahidi, uwekezaji ambao tumeufanya au tunaoendelea kuufanya kupitia barabara ya lami kwenda Kigoma, upanuzi wa bandari ya Kigoma, ongezeko la idadi ya meli na ufunguzi wa kiwanda cha *cement* pale Kigoma, unaonyesha *commitment* ya Serikali kuwa Mkoa wa Kigoma ni mkoa wa kimkakati katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumaini yetu ni kwamba vitaongeza ajira kwa vijana, na pia vinaenda kuongeza thamani ya malighafi ambazo zinapatikana Kigoma. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lazaro Londo, Naibu Waziri Viwanda na Biashara, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunamalizia swali la mwisho, linaelekezwa Wizara ya Nishati. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 93

**Umeme Toshelevu kwenye Maeneo ya Wachimbaji Wadogo**

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakuja na mpango mkakati wa kupeleka umeme toshelevu maeneo ya wachimbaji wadogo ili kupunguza gharama za uzalishaji?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa shughuli zote za uchimbaji mdogo wa madini nchini zinahitaji umeme wa uhakika, wenye ubora na toshelevu ili kuendesha mitambo ya uchimbaji, usagaji na uchenjuaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imetekeleza mradi wa kusambaza umeme katika maeneo 582 ya migodi midogo, kilimo na viwanda Tanzania Bara kwa gharama ya shilingi bilioni 115. Mradi huu ulianza Aprili, 2023 na kwa sasa upo katika hatua ya umaliziaji. Aidha, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Madini inaendelea kuainisha maeneo

ya kipaumbele ambayo yataendelea kupelekewa umeme kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali kupitia *TANESCO* kwa kutumia fedha za ndani inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme katika mikoa mbalimbali nchini hususan katika maeneo ambayo yana *low voltage*. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha maeneo yote ya uzalishaji ikiwemo wachimbaji wadogo wanapata huduma ya umeme iliyo toshelevu na ya uhakika wakati wote. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na mipango mikakati ambayo Serikali imeiweka kwa ajili ya kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana kwa wachimbaji wadogo na hasa wachimbaji wanawake ambao wamepatiwa mitaji na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampongeza kwa majibu mazuri na jitihada kubwa ya *investment* ya Serikali ya zaidi ya shilingi bilioni 115 iliyotumika kufikisha maeneo haya. Hata hivyo, wahakikishe kwamba changamoto ya *low voltage* hasa kwenye maeneo ya Mwakitolyo na Nyandole yanafanyiwa kazi. Ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Mwanahamisi Munkunda, Mbunge mwenzangu kutoka Mkoa wa Shinyanga. Nami ninamwahidi kwamba katika maeneo haya ya wachimbaji hasa wa Mwakitolyo na wachimbaji wote wa mkoa mzima wa Shinyanga, tunafahamu kwamba mkoa wetu, kitega uchumi kikubwa kinatokana na

upatikanaji wa madini, kwa hiyo, ni jukumu la Serikali hasa Wizara ya Nishati kuwapelekea umeme wa uhakika ili uzalishaji uwe na tija na Mkoa wa Shinyanga uendelee kung'ara katika uzalishaji na uchangiaji katika pato la Taifa. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Ninaomba niwatambulishe wageni walioko Bungeni siku hii ya leo.

Tukianza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Spika kutoka Bunge la Jamhuri ya Watu wa Kongo yupo *Honourable* Aimé Boji Sangara Bamanyirue, *President of the National Assembly of Democratic Republic of Congo*; *Honourable* Mishiki Suhini Willy, *Member of Parliament*; *Mr*. Chiribagula Ntwali Jean, *Advisor to the President; Mr*. N'shokano Balola Ruphin, *Coordinator of the Communication Department; and Mr*. Anzoli Momem Axel, *cameraman in the Office of the President of the National Assembly*.

Wengine ni *Mr*. Malongo Kimana Didier, *photographer in the Office of the President of the National Assembly*; Ndg. Msafiri Marwa, Mkuu wa Utawala, Ubalozi wa Tanzania, Kinshasa; na Ndg. David Fupi, Afisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika kutoka Bunge la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pamoja na msafara wako, karibuni sana hapa Bungeni, Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Babati Vijijini Mkoani Manyara. Yupo Ndugu Ally Juma,

Ndugu Samweli Gwahara, pia Ndugu Salma Ramadhani. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni mgeni mmoja wa Mheshimiwa Hamza Said Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye ni Ndugu Neema Grace Johari, Mke wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Karibu sana Ndugu Neema na tunakushukuru kwa kuendelea kumtunza Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Vile vile wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, ambaye ni Padre Emanuel Gembuya wa Jimbo Katoliki Meatu kutoka mkoani Simiyu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Fratern Mdaku ambao ni Makatibu wa Ofisi ya Mbunge kutoka Malinyi Mkoani Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, wadau wa maendeleo kutoka Wilaya ya Ikungi Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, ambao ni wafanyakazi kutoka Chuo Kikuu Huria. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, ambao ni marafiki zake kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Nadra Ghulam Rashid, ambao ni familia yake kutoka Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 13 wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ambao ni viongozi wa Chama cha Wafugaji Tanzania kutoka Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly ambao ni wanafunzi na walimu wa Chuo cha Biblia kutoka Sumbawanga Mkoani Rukwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 21 wa Mheshimiwa John Stephano Luhende ambao ni *Ex- DARUSO Leaders* mwaka 2013/2014, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 33 wa Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka ambao ni Ndugu, jamaa na marafiki kutoka Mkoa wa Ruvuma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 41 wa Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, ambao ni Kikundi cha Gombani *Fitness Club* kutoka Chakechake Pemba, Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni Ndugu Sophia Ibrahimu Hamza, Mkurugenzi Mkuu *SM* Tanzania *Foundation* ya Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Fahadi Shabani Hamisi, Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaos washiriki 36 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Kigoda cha Mwalimu Nyerere kwa kushirikiana na Taasisi ya Rosa Luxemburg Afrika Mashariki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 92 na walimu sita wa Shule ya Sekondari ya wasichana Aman kutoka Manyoni Mkoani Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni wote waliopata fursa ya kututembelea siku ya leo hapa Bungeni.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.02) Bill, 2026]*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.02) wa mwaka 2026, *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill,* 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu, kuendelea kumwombea Mheshimiwa Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu ili amjalie afya njema na kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwa mara nyingine tena, kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Louis Pankras Mtemi Ndejembi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru na kukupongeza kwa namna ambavyo umeongoza kikao chetu hadi sasa. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa namna ambavyo mnaliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee pia ninapenda kuishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaonipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, inayoongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, na Makamu wake Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta jedwali la marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie pia fursa hii kuwapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Ndugu Samwel Maneno, kwa jinsi wanavyojituma na kutekeleza majukumu kwa umahiri na weledi. Kipekee pia ninaomba kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wakiongozwa na Ndugu Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa msaada waliotoa kwangu kipindi chote cha kushughulikia Muswada huu na kuhakikisha kuwa ninatekeleza majukumu yangu kwa ubora na kiwango stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninaomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mke wangu na rafiki yangu, mpenzi wangu, ambaye leo yupo nasi katika Jukwaa la Spika, kwa mapenzi yake, kwa upendo wake, kwa ushauri wake, ambavyo vinanifanya niweze kutekeleza majukumu yangu na kunipa amani ya roho. Ahsante sana Mke wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijielekeze katika maudhui ya Muswada ulio mbele yetu. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill,* 2026) kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria Kuu Saba (7) zifuatazo:-

(1) Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116;
(2) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287;
(3) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
(4) Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61;
(5) Sheria ya Mamlaka ya Nchi katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449;
(6) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138; na
(7) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya sheria yanapendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi yaani Sura ya 116. Sheria hii ilitungwa mwaka 2007 kwa lengo la kuweka taratibu za uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Kufuta Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 1984; na kuweka masharti kwa masuala yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kutungwa kwake, sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha mfumo wa kisheria ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hivyo marekebisho yanakusudia kubainisha muda wa kushika madaraka kwa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kuongeza vyanzo vya mapato ya Tume na kuimarisha ushirikiano kati ya Tume na mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kuhusu muda wa Wajumbe wa Tume kushika madaraka. Inapendekezwa kuwa muda wa kushika madaraka uwe miaka mitatu ili kuimarisha utawala bora na kutoa fursa kwa Waziri kuteua Wajumbe kutoka miongoni mwa kada mbalimbali zilizoainishwa kwenye Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushauriana na Kamati ninapendekeza, kupitia Jedwali la Marekebisho, kurekebisha Kifungu hicho cha sita ili kuweka masharti kwamba uteuzi wa Wajumbe wa Tume utazingatia umahiri wa kitaaluma, ujuzi na uzoefu uliothibitika katika sekta wanazohudumia. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha uteuzi wa wajumbe unazingatia sifa na uwezo unaohitajika ili kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 7(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Tume kuwekeza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuiwezesha Tume kuongeza mapato kupitia uwekezaji, hivyo, kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, baada ya mashauriano na Kamati ninapendekeza, kupitia jedwali la marekebisho, marekebisho ya Kifungu cha 14 ili kujumuisha fedha zitokanazo na uwekezaji unaofanywa na Tume kuwa miongoni mwa vyanzo vya fedha vya Tume kufuatia pendekezo la kuipa Tume mamlaka ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Tume mamlaka ya kutoa maelekezo kwa mamlaka nyingine za upangaji kuhusu masuala yanayohusu mipango ya matumizi ya ardhi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utaratibu na usimamizi wa masuala ya mipango ya matumizi ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 25 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka sharti la mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi kushauriana na Tume kabla ya kutangaza eneo kuwa eneo la mpango. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ushirikiano na utaratibu kati ya mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi na Tume katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 61 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha adhabu kwa mtu anayekiuka masharti na vigezo vya mpango wa matumizi ya ardhi ulioidhinishwa. Aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati napendekeza, kupitia Jedwali la Marekebisho, kufanya marekebisho ya Vifungu vya 61 na 62 ili kutenganisha adhabu ya jumla kwenye makosa mahsusi pamoja na kuhuisha viwango vya adhabu kwa makosa hayo. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha uzingatiaji wa masharti ya Sheria na kuhakikisha kuwa adhabu zinazotolewa kwa ukiukwaji wa masharti ya sheria zinaendana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekezwa kurekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287. Sheria hii ilitungwa mwaka 1982 kwa lengo la kuweka masharti yanayosimamia Mamlaka za Wilaya. Sheria hii imerekebishwa mara kadhaa ili kuendana na mahitaji na mazingira ya wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza muda wa Makamu Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya kushika madaraka. Kwa sasa sheria inaelekeza kuwa Makamu Mwenyekiti atashika madaraka kwa mwaka mmoja. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni

kuoanisha muda huo wa Wenyeviti kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji wa viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza kupitia Jedwali la Marekebisho, kurekebisha Kifungu hicho cha 38 ili kubainisha kuwa katika mazingira maalumu yaliyoelezwa katika Kifungu cha (5), Baraza la Madiwani linaweza kuazimia kuwa viongozi hao washike wadhifa wao kwa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Sheria hii ilitungwa mwaka 1982 kwa lengo la kuweka masharti yanayosimamia Mamlaka za Miji. Kama ilivyo kwa Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, Sheria hii imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa Mamlaka za Miji na kuziwezesha kuendana na kasi ya ukuaji wa miji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu vya 25 na 27 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza muda wa kushika wadhifa wa Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji na Manispaa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha muda huo na muda wa Meya katika Halmashauri ya Jiji na Manispaa na Mwenyekiti katika Halmashauri ya Mji ili kuimarisha uwajibikaji wa Viongozi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 27 kupitia jedwali la marekebisho ili kuweka sharti kuwa pale ambapo wagombea wa nafasi ya Meya, Mwenyekiti, Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti wanapokuwa wamelingana kura, Wajumbe wa Baraza waweze kuazimia kufupisha kipindi cha kushika wadhifa ili wagombea hao wagawane muda huo wa kushika wadhifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa,

Sura ya 61. Sheria hii ilitungwa mwaka 2010 kwa lengo la kuanzisha Baraza la Usalama la Taifa na Kamati za Usalama katika ngazi mbalimbali za kiutawala kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu masuala ya usalama wa Taifa. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Nne kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha idadi ya vikao vya baraza vinavyopaswa kufanyika kisheria kwa mwaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha utekelezaji wenye tija wa majukumu ya Baraza la Usalama la Taifa na uendeshaji bora wa shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Nchi (katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia), Sura ya 449. Sheria hii ilitungwa mwaka 2017 kwa lengo la kulinda rasilimali asilia za nchi. Tangu kutungwa kwake, sheria hii imefanyiwa marekebisho mara tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa matumizi ya vyombo vya utoaji haki sehemu ya utatuzi wa migogoro na mamlaka ya utatuzi wa migogoro inayotokana na shughuli za uziduaji, uvunaji, na upatikanaji na utumiaji wa mali na rasilimali asilia kama itakavyokubaliwa na pande husika za makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini. Kwa sasa sheria inataka migogoro ya aina hiyo itatuliwe nchini na vyombo vya Kimahakama pekee au vyombo vingine kwa kutumia Sheria za Tanzania hali inayoweza kuathiri mazingira ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138. Sheria hii ilitungwa mwaka 2016 kwa lengo la kuainisha Mamlaka na Majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali,

kuanzisha Bodi ya Usajili wa Wathamini, kuweka masharti kuhusu majukumu ya uendeshaji wa Bodi, kuweka masharti ya udhibiti na usimamizi wa taaluma na shughuli za uthamini. Tangu kutungwa kwake sheria hii haijawahi kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Tatu kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza na kuboresha fasili ya misamiati iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa misamiati iliyotumika katika sheria inatafsiriwa ili kuiwezesha kueleweka kwa kadri ilivyotumika katika masharti mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Sita kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa idhini ya Mheshimiwa Waziri mamlaka ya kutoa msamaha wa ada zinazohusu huduma zinazotolewa na mthamini kwa taasisi ya Serikali. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha utoaji wa msamaha wa ada kwa taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, ninapendekeza marekebisho ya kifungu hicho kupitia jedwali la marekebisho ili kuweka sharti la Mthamini Mkuu wa Serikali kuzingatia sheria nyingine itakayokuwa imeweka masharti yoyote kuhusu uthamini wa mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu vya 49 na 50 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka usahihi wa masharti kuhusu dhumuni la uthamini katika Kifungu cha 49 na vigezo vya msingi wa uthamini katika Kifungu cha 50. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka misingi sahihi ya uthamini na kuongeza uwazi katika utekelezaji wa shughuli za uthamini kwa kuhakikisha ulinganifu na matumizi sahihi ya kanuni za uthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 62 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuzuia watu ambao hawajasajiliwa au kuorodheshwa kufanya shughuli za uthamini. Lengo la marekebisho

yanayopendekezwa ni kuhakikisha taaluma ya uthamini inadhibitiwa ipasavyo na Bodi ya Usajili wa Wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 70 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha kutengenezwa kwa kanuni zitakazoweka vigezo na utaratibu wa utoaji wa msamaha. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka mfumo na utaratibu wa wazi wa utekelezaji wa mamlaka ya kutoa msamaha wa ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283. Kwa faida ya wafugaji ninaomba nirudie. Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283. Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 kwa lengo la kuweka masharti kuhusu uhifadhi, usimamizi, ulinzi na matumizi endelevu ya wanyamapori na bidhaa za wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kutungwa kwake Sheria hii imerekebishwa mara kadhaa kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa masharti mbalimbali ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu vya 111 na 116 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa mifugo kuwa miongoni mwa vitu ambavyo vinaweza kutaifishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuondoa mifugo kuwa miongoni mwa vitu ambavyo vinaweza kutaifishwa baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka uwiano kati ya kosa na adhabu inayotolewa ili kuimarisha misingi ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naomba kwa niaba ya Serikali niliahidi Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kufanya maboresho ya sheria ili kuhakikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu inatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka, 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026)* ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**MAELEZO YA MHESHIMIWA HAMZA SAID JOHARI (MB), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 2) WA MWAKA 2026 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 02) BILL, 2026) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuingoza Nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie nafasi hii kwa mara nyingine tena kumpongeza Mhe. Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Vile vile, napenda kuwapongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuliongoza Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa shukurani kama nisipo kushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya pekee napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bw. Baraka Ildiphonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee niishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.) na Makamu wake Mhe. Edwin Enosy Swalle (Mb.) pamoja na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kuishauri Serikali kuuboresha Muswada. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie pia fursa hii kuwapongeza pia watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Ndg. Samwel Maneno kwa jinsi wanavyojituma na kutekeleza majukumu kwa umahiri na weledi. Kipekee pia naomba kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wakiongozwa na Ndg. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa msaada waliotoa kwangu kipindi chote cha

kushughulikia Muswada huu na kuhakikisha kuwa ninatekeleza majukumu yangu kwa ubora na kiwango stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nijielekeze katika maudhui ya Muswada ulio mbele yetu. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026) kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria Kuu Saba (7) zifuatazo:

1. Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116;
2. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287;
3. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
4. Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61;
5. Sheria ya Mamlaka ya Nchi Katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449;
6. Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138; na
7. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya Sheria yanapendekezwa kurekebishwa katika Sehemu zake.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116. Sheria hii ilitungwa mwaka 2007 kwa lengo la kuweka taratibu za uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi; kufuta Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 1984; na kuweka masharti kwa masuala yanayohusiana na hayo. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha mfumo wa kisheria ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hivyo, marekebisho yanakusudia kubainisha muda wa kushika madaraka kwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi,

kuongeza vyanzo vya mapato ya Tume, na kuimarisha ushirikiano kati ya Tume na mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi.

Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti kuhusu muda wa wajumbe wa Tume kushika madaraka. Inapendekezwa kuwa muda wa kushika madaraka uwe miaka mitatu ili kuimarisha utawala bora na kutoa fursa kwa Waziri kuteua wajumbe kutoka miongoni mwa kada mbalimbali zilizoainishwa kwenye Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Serikali kushauriana na Kamati napendekeza, kupitia Jedwali la Marekebisho, kurekebisha kifungu hicho cha 6 ili kuweka masharti kwamba uteuzi wa wajumbe wa Tume utazingatia umahiri wa kitaaluma, ujuzi na uzoefu uliothibitika katika sekta wanazohudumia. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha uteuzi wa wajumbe unazingatia sifa na uwezo unaohitajika ili kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa Tume.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiwezesha Tume kuwekeza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuiwezesha Tume kuongeza mapato kupitia uwekezaji hivyo, kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake. Vile vile, baada ya mashauriano na Kamati napendekeza, kupitia Jedwali la Marekebisho, marekebisho ya Kifungu cha 14 ili kujumuisha fedha zitokanazo na uwekezaji unaofanywa na Tume kuwa miongoni mwa vyanzo vya fedha vya Tume kufuatia pendekezo la kuipa Tume mamlaka ya kuwekeza. Vile vile, kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Tume mamlaka ya kutoa maelekezo kwa mamlaka nyingine za upangaji kuhusu masuala yanayohusu mipango ya matumizi ya ardhi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya mipango ya matumizi ya ardhi nchini.

Kifungu cha 25 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka sharti la mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi kushauriana na Tume kabla ya kutangaza eneo kuwa eneo la mpango. Lengo la

marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha ushirikiano na uratibu kati ya mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi na Tume katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kifungu cha 61 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha adhabu kwa mtu anayekiuka masharti na vigezo vya mpango wa matumizi ya ardhi ulioidhinishwa. Aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati napendekeza, kupitia Jedwali la Marekebisho, kufanya marekebisho ya vifungu vya 61 na 62 ili kutenganisha adhabu ya jumla kwenye makosa mahsusi pamoja na kuhuisha viwango vya adhabu kwa makosa hayo. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha uzingatiaji wa masharti ya Sheria na kuhakikisha kuwa adhabu zinazotolewa kwa ukiukaji wa masharti ya Sheria zinaendana na mazingira ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287. Sheria hii ilitungwa Mwaka 1982 kwa lengo la kuweka masharti yanayosimamia mamlaka za wilaya. Sheria hii imerekebishwa mara kadhaa ili kuendana na mahitaji na mazingira ya wakati husika.

Kifungu cha 38 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza muda wa Makamu Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya kushika madaraka. Kwa sasa Sheria inaelekeza kuwa Makamu Mwenyekiti atashika madaraka kwa mwaka mmoja. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha muda huo na muda wa Wenyeviti kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji wa viongozi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza kupitia Jedwali la Marekebisho, kurekebisha kifungu hicho cha 38 ili kubainisha kuwa katika mazingira maalumu yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (5), Baraza la Madiwani linaweza kuazimia kuwa viongozi hao washike wadhifa wao kwa muda mfupi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Sheria hii ilitungwa mwaka 1982 kwa lengo la kuweka masharti yanayosimamia mamlaka za miji. Kama ilivyo kwa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, Sheria hii imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa mamlaka za miji na kuziwezesha kuendana na kasi ya ukuaji wa miji nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Vifungu vya 25 na 27 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza muda wa kushika wadhifa wa Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji na Manispaa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanisha muda huo na muda wa Meya katika Halmashauri ya Jiji na Manispaa na Mwenyekiti katika Halmashauri ya Mji ili kuimarisha uwajibikaji wa uongozi. Baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza marekebisho ya kifungu cha 27 kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuweka sharti kuwa pale ambapo wagombea wa nafasi ya Meya, Mwenyekiti, Naibu Meya au Makamu Mwenyekiti wanapokuwa wamelingana kura, wajumbe wa baraza waweze kuazimia kufupisha kipindi cha kushika wadhifa ili wagombea hao wagawane muda huo wa kushika wadhifa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61. Sheria hii ilitungwa mwaka 2010 kwa lengo la kuanzisha Baraza la Usalama la Taifa na kamati za usalama katika ngazi mbalimbali za kiutawala kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu masuala ya usalama wa Taifa. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara moja.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha idadi ya vikao vya Baraza vinavyopaswa kufanyika kisheria kwa mwaka. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha utekelezaji wenye tija wa majukumu ya Baraza la Usalama la Taifa na uendeshaji bora wa shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Nchi Katika Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449. Sheria hii ilitungwa mwaka 2017 kwa lengo la kulinda rasilimali asilia za nchi. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara tatu.

Kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa matumizi ya vyombo vya utoaji haki, sehemu ya utatuzi wa migogoro na mamlaka ya utatuzi wa migogoro inayotokana na shughuli za uziduaji, uvunaji au upatikanaji na utumiaji wa mali na rasilimali asilia, kama itakavyokubaliwa na pande husika za makubaliano. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka mazingira bora ya uwekezaji nchini. Kwa sasa Sheria inataka migogoro ya aina hiyo itatuliwe nchini na vyombo vya kimahakama au vyombo vingine kwa kutumia Sheria za Tanzania, hali inayoweza kuathiri mazingira ya uwekezaji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138. Sheria hii ilitungwa mwaka 2016 kwa lengo la kuainisha mamlaka na majukumu ya Mthamini Mkuu wa Serikali, kuanzisha Bodi ya Usajili wa Wathamini, kuweka masharti kuhusu majukumu na uendeshaji wa Bodi, kuweka masharti ya udhibiti na usimamizi wa taaluma na shughuli za uthamini. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii haijawahi kurekebishwa.

Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza na kuboresha fasili ya misamiati iliyotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa misamiati iliyotumika katika Sheria inatafsiriwa ili kuiwezesha kueleweka kwa kadri ilivyotumika katika masharti mbalimbali ya Sheria.

Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Mthamini Mkuu wa Serikali, kwa idhini ya Waziri, mamlaka ya kutoa msamaha wa ada zinazohusu huduma zinazotolewa na mthamini kwa taasisi ya Serikali. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha utoaji wa msamaha wa ada kwa taasisi za Serikali.

Aidha, baada ya Serikali kushauriana na Kamati, napendekeza marekebisho ya kifungu hicho kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuweka sharti la Mthamini Mkuu wa Serikali kuzingatia sheria nyingine itakayokuwa imeweka masharti yoyote kuhusu uthamini wa mali.

**Mheshimiwa Spika,** Vifungu vya 49 na 50 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka usahihi wa masharti kuhusu dhumuni la uthamini katika kifungu cha 49 na vigezo vya msingi wa uthamini katika kifungu cha 50. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka misingi sahihi ya uthamini na kuongeza uwazi katika utekelezaji wa shughuli za uthamini kwa kuhakikisha ulinganifu na matumizi sahihi ya kanuni za uthamini.

Kifungu cha 62 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuzuia watu ambao hawajasajiliwa au kuorodheshwa kufanya shughuli za uthamini. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha taaluma ya uthamini inadhibitiwa ipasavyo na Bodi ya Usajili wa Wathamini. Kifungu cha 70 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha kutengenezwa kwa kanuni zitakazoweka vigezo na utaratibu wa utoaji wa msamaha. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka mfumo na utaratibu wa wazi wa utekelezaji wa mamlaka ya kutoa msamaha wa ada.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283. Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 kwa lengo la kuweka masharti kuhusu uhifadhi, usimamizi, ulinzi na matumizi endelevu ya wanyamapori na bidhaa za wanyamapori. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imerekebishwa mara kadhaa kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa masharti mbalimbali ya Sheria.

Vifungu vya 111 na 116 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiondoa mifugo miongoni mwa vitu ambavyo vinaweza kutaifishwa baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka uwiano kati ya kosa na adhabu inayotolewa ili kuimarisha misingi ya haki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine naomba, kwa niaba ya Serikali, niliahidi Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kufanya maboresho ya sheria ili kuhakikisha kuwa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu inatekekelezwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, NAOMBA KUTOA HOJA.

Hamza S. Johari (Mb.),
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
2 Septemba, 2026

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote na kwa mujibu wa Kanuni ya 102 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha maoni ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 02 ya Mwaka, 2026 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 02) Bill, 2026)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa iliyobeba maoni ya Kamati iwekwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge yaani Hansard kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 26 Juni, 2026 katika Kikao cha 58 cha Mkutano wa Tatu, Muswada huo ulisomwa mara ya kwanza kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Baada ya hatua hiyo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 100 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 139 (14) ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1b) Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili maelekezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Hamza Saidi Johari siku ya Jumanne Tarehe 11 Agosti, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni yao *(public hearing)* kuhusu Muswada huu na jumla ya wadau 32 walifika kwenye kikao hicho kutoka katika asasi za kiraia Saba. Kwa upekee Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote kama walivyotajwa katika ukurasa wa pili wa taarifa ya Kamati kwa kutoa maoni yao ambayo yalitoa mchango mkubwa kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Muswada. Kamati ilifanya kazi ya kuchambua Muswada wote wenye jumla ya Ibara 26 zinazolenga kurekebisha sheria saba ambazo ni:

(i) Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura 116;

(ii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
(iii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
(iv) Sheria ya Baraza la Usalama wa Taifa, Sura ya 61;
(v) Sheria ya Mamlaka za Nchi (Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia), Sura ya 449.
(vi) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138; na
(vii) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua Ibara zote 26 za Muswada huu. Katika uchambuzi huu, Kamati ilikubaliana na mapendekezo yaliyopendekezwa isipokuwa kwa baadhi ya Ibara ambazo Kamati ilipendekeza maboresho ambayo yalikubaliwa na Serikali. Uchambuzi kuhusu Sehemu za Muswada huu na Ibara zake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moja, marekebisho ya Sheria ya Mipango na ya Matumizi ya Ardhi Sura 116. Uchambuzi wa Kamati umebaini mapungufu katika Ibara ya Nne, Tano na Sita. Ibara ya Nne imependekeza kuweka muda wa miaka mitatu kwa Wajumbe wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi pamoja na uwezekano wa kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Kamati imebaini kuwa Sheria haijaweka sifa za wajumbe hali inayoweza kusababisha kuteuliwa kwa watu wasio na uzoefu na utaalamu unaohitajika kwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ibara ya Tano imependekeza kuipa Tume mamlaka ya kuwezesha kuwekeza fedha ili kuongeza vyanzo vya mapato lakini Kifungu cha 14 hakijatambua mapato yatokanayo na uwekezaji kama chanzo cha fedha za Tume hivyo kuna haja ya kuoanisha vifungu hivyo viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya Sita inapendekeza mamlaka ya upangaji wa matumizi ya ardhi kushauriana na Tume kabla ya

kutangaza eneo kuwa eneo la mpango. Kamati inaona kuwa hatua hii ni muhimu katika kuimarisha ushirikishwaji wa Tume. Hata hivyo, ushauri pekee hauipi Tume mamlaka ya kuhakikisha ushauri wake unazingatiwa. Mamlaka za upangaji bado zinaweza kuamua kutofuata ushauri huo jambo ambalo linaweza kusababisha mipango ya matumizi ya ardhi kutokidhi vigezo au kutotekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba lengo la marekebisho ni kubadili muda wa kushika madaraka wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya kuwa miaka mitano badala ya mwaka mmoja. Baada ya marekebisho haya kuridhiwa na kuwa sheria, muda wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri utaendana na muda wa kushika madaraka wa Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia Sheria yote na kubaini kuwa bado kuna maeneo yanahitaji marekebisho. Mojawapo ni Kifungu cha 38 (8) kinacholipa Baraza la Halmashauri ya Wilaya mamlaka ya kumuondoa madarakani Mwenyekiti wa Halmashauri kwa azimio linaloungwa mkono na theluthi mbili ya Wajumbe wote bila kumtaja Makamu wake licha ya kuongezewa muda wa kukaa madarakani kuwa miaka mitano kama ilivyo kwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokumjumuisha Makamu Mwenyekiti kunalinyima Baraza mamlaka ya kumuondoa madarakani kwa azimio la wajumbe wa baraza. Hali hii haileti usawa wa kisheria kwa Mwenyekiti na Makamu wake, tatizo ambalo linapaswa kurekebishwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Ibara ya 12 una lengo la kuboresha Sheria hii kuhusu muda wa kukaa madarakani viongozi wa Baraza la Halmashauri ya Manispaa na Halmashauri ya Miji. Hata hivyo, Kamati imebaini baadhi ya maeneo yanayohitaji maboresho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mosi, Kifungu cha 27 (6) kinalipa Baraza mamlaka ya kumuondoa madarakani Meya wa Halmashauri ya Mji au Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji kwa azimio linaloungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe. Kifungu hicho hakijamtaja Naibu Meya au Makamu Mwenyekiti licha ya viongozi hao kuongezewa muda wa kukaa madarakani kwa miaka mitano kama ilivyo kwa Meya na kwa Mwenyekiti, usawa wa madaraka kwa kipindi cha miaka mitano. Hali hii haileti usawa wa kisheria kwa viongozi hao na hivyo inapaswa kurekebishwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, marekebisho ya Kifungu cha 27 (4) yanayoweka muda wa miaka mitano kwa Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti yanahitaji kuzingatia zaidi mpangilio wa viongozi kwa mji wa itifaki. Kamati pia imebaini kuwa Kifungu cha 27 (4) baada ya marekebisho kitaliwezesha Baraza kufupisha muda wa madaraka wa Meya, Mwenyekiti, Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti kabla ya kutimiza miaka mitano. Hata hivyo, Muswada haujaainisha mazingira au vigezo vitakavyoruhusu Baraza kufanya uamuzi huo hali inayoweza kuleta utata katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi (Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasimali Asilia), Sura ya 449. Ibara ya 16 inarekebisha Kifungu cha 11 ili kutambua makubaliano ya pande za mkataba katika sekta ya uzinduaji kuhusu utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba iliyoidhinishwa na Baraza la Mawaziri na yenye masharti hayo itaweza kuruhusu migogoro kutatuliwa na vyombo vinavyokubaliwa na wahusika ikiwemo vyombo vilivyo nje ya Tanzania na kwa kutumia sheria walizokubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa marekebisho hayo yanaweza kusaidia kuvutia wawekezaji wa kimkakati katika sekta ya uzinduaji na kuheshimu makubaliano halali ya kimikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138. Ibara ya 18 inaongeza fasili ya neno *asset* na kupanua fasili ya neno *valuation* ili kujumuisha mali zenye thamani ya kiuchumi ikiwemo hisa, mitaji, hakimiliki na bunifu. Hata hivyo, Kamati imebaini fasili hii ni pana na inaweza kuingiliana na sheria na mamlaka nyingine zinazosimamia mali za kifedha, hisa, hakimiliki na sekta nyingine maalum, hivyo kusababisha mgongano wa kisheria na mwingiliano wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19 inapendekeza kumpa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa idhini ya Mheshimiwa Waziri, mamlaka ya kusamehe ada zinazolipwa kwa huduma za uthamini zinazotolewa na Wathamini wa Serikali. Kamati inaona kuwa pendekezo hili ni zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Muswada haujaweka wazi aina ya huduma zinazoweza kusamehewa, vigezo vya kutoa au kukataa msamaha wala mipaka ya mamlaka hayo. Hali inayoweza kuruhusu misamaha kutolewa kwa kazi binafsi zinazofanywa na wathamini wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283. Ibara ya 25 na 26 zinafuta neno *livestock* katika vifungu husika kwa lengo la kuiondoa mifugo katika orodha ya mali zinazoweza kutaifishwa kutokana na makosa chini ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori. Kamati imeona kuwa hatua hii ni nzuri katika kulinda haki za wafugaji, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa licha ya kurekebishwa kwa Sheria hii bado zipo sheria nyingine zinazowezesha mifugo kushikiliwa, kutaifishwa au kuuzwa na hivyo marekebisho haya pekee yanaweza yasimalize changamoto hii kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati ni kuwa kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada huu isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Kamati ilipendekeza maboresho na Serikali imeyazingatia. Moja, maboresho kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria haijaweka sifa na uzoefu unaohitajika kwa Wajumbe wa Tume ya Mipango ya Ardhi hali inayoweza kusababisha kuteuliwa kwa wajumbe wasiokuwa na utaalamu na uzoefu wa kutosha. Kwa hiyo, Kamati ilishauri Ibara ya 4 iboreshwe kwa kuweka sifa za watu wanaoweza kuteuliwa. Serikali imekubaliana na ushauri huo na imeboresha Ibara ya 4 kupitia jedwali la marekebisho ya Serikali;

(b) Ibara ya 5, inaongeza Kifungu cha 7A ili kuipa Tume mamlaka ya kuwezesha kuwekeza fedha zake wakati Kifungu cha 14 hakitambui mapato yatokanayo na uwekezaji kama chanzo cha mapato ya Tume. Kamati ilishauri Kifungu cha 14 kirekebishwe ili kutambua mapato ya Serikali, mapato hayo na Serikali imekubaliana na ushauri huo kwa kuongeza Ibara Mpya baada ya Ibara ya 5, kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali; na

(c) Ibara ya 6, inaweka wajibu wa Tume kushauriana na mamlaka za upangaji kabla ya kutangaza kwa eneo kuwa eneo la mpango. Hata hivyo mamlaka hizo zinaweza kuamua kuzingatia au kutokuzingatia ushauri wa Tume. Kamati ilishauri Tume ipewe mamlaka ya kauli ya mwisho kwa masuala yasiyohitaji ushauri ili kuimarisha utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Serikali imekubaliana na ushauri huo kwa kuongeza Ibara Mpya kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Kifungu cha 38, Kifungu Kidogo cha Nane kinacholipa Baraza mamlaka ya kumuondoa madarakani Mwenyekiti kwa azimio linaloungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe kirekebishwe ili kujumuisha Makamu Mwenyekiti na hivyo kuweka usawa wa kisheria. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuleta marekebisho ya Ibara ya 9. Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Miji.

(a) Kamati ilishauri Ibara ya 12 iboreshwe ili ilete uwiano wa viongozi waliotajwa ukizingatia itifaki na kuenzi misingi ya utawala bora. Serikali imeridhia ushauri huo na kuboresha Ibara ya 12 kupitia jedwali lake la marekebisho; na

(b) Kamati ilishauri Ibara ya 12 iboreshwe kwa kurekebisha Kifungu cha 27 Kifungu Kidogo cha Sita cha Sheria ili kujumuisha Naibu Meya wa Manispaa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji kuwa na uwezekano wa kuondolewa madarakani kama ilivyo kwa Meya wa Manispaa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji. Serikali imekubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 12 kupitia jedwali lake la marekebisho ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 27 Kifungu Kidogo cha Nne cha Sheria kinachorekebishwa na Ibara ya 12 kitawezesha Baraza la Halmashauri ya Manispaa ya Mji, Halmashauri ya Wilaya kufanya uamuzi wa kufupisha muda wa Meya, Mwenyekiti, Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti kushikilia madaraka chini ya muda wa miaka mitano. Kifungu hicho kiboreshwe ili kiweze kuainisha mazingira ambayo yanaweza kupelekea baraza kufikia uamuzi huo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 12 kupitia jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini. Kamati ilishauri kuwa fasiri ya neno *asset* iliyopo kwenye Ibara ya 18 ni pana na inaweza kukinzana na Sheria za mamlaka nyingine zinazosimamia mali zisizoshikika na ingefaa fasiri hiyo iwekewe mipaka ili kuondoa mgongano huo. Serikali imeukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 19 kupitia jedwali lake la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilishauri Ibara ya 19 iboreshwe kwa kuwekea Mthamini Mkuu wa Serikali aina ya kazi, huduma zinazoweza kusamehewa ada, vigezo vya kutoa au kukataa msamaha. Vilevile Ibara hiyo iboreshwe ili kutenganisha kazi binafsi ya uthamini inayoweza kufanywa na wathamini wa Serikali na kazi za Serikali zinazoweza kufanywa na wathamini hao hao wa

Serikali. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 19 na 23 ya Muswada huu kupitia jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Ibara ya 25 na 26 Kamati ilishauri kuwa zipo Sheria nyingine zenye vifungu vinavyoruhusu mifugo kutaifishwa ikiwemo Sheria ya Misitu, Sheria ya *TANAPA* na Ngorongoro. Kamati iliishauri Serikali ilete marekebisho ya sheria hizi, Serikali mbele ya Kamati kupitia jedwali la hoja za Kamati imeeleza kuwa marekebisho ya sheria hizo yatawasilishwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati inashauri watu wanaokamata mifugo pasipo kuipatia mifugo hiyo haki zake kama vile chakula, maji, matibabu stahiki, sehemu salama na kuwekwa kwenye eneo lenye nafasi na hewa ya kutosha kadri ya haki hizo zinavyotambuliwa na Sheria ya Ustawi wa Wanyama wachukuliwe hatua binafsi kwa kukiuka masharti ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia. Marekebisho ya sheria hii yatawezesha wadau katika mikataba ya kisekta ya uzinduaji *(extractive industry)* iliyokidhi masharti yanayopendekezwa katika Muswada kwenda kutatua migogoro yao katika vyombo mbalimbali walivyochagua wao ikiwemo vyombo vya nje ya nchi na kwa kutumia sheria walizochagua wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kwamba jambo hili linavutia uwekezaji, Kamati inaamini endapo kungeanzishwa kituo cha usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji chenye hadhi ya kimataifa hapa nchini, migogoro hiyo ingetatuliwa hapa nchini kama ilivyokusudiwa hapo awali na sheria hii. Hivyo basi, Serikali ianzishe kituo cha usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji hapa nchini chenye hadhi ya kimataifa ikiwa ni pamoja na kuwaandaa wataalamu wetu wa kutosha waliobobea katika masuala ya usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru Spika, kwa dhati akisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vyema Bunge hili na kwa namna ambayo ameipatia Kamati ushirikiano, ushauri na maelekezo yake imekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Juma Zuber Homera, Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba, kwa ushirikiano wao mzuri wa kipekee waliotupatia Kamati wakati wa kuchambua Muswada huu. Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali *(CPD)* Ndugu Onorius Njole, kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa umahiri wao, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua Muswada huu na hatimaye kukamilisha taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa hii za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu ninamshukuru sana Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini kwa ushirikiano wanaonipatia kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge kwa neema ya Mungu sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria inaliomba Bunge lako Tukufu kujadili, kukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Mbili wa Mwaka 2026 *(The Laws*

*Miscellaneous Amendments Bill (No. 02) Bill, 2026)* pamoja na marekebisho yake kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 2 WA MWAKA 2026 (*THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 2) BILL, 2026*) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 102 (5)** na **Kanuni ya 139 (11)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 Wa Mwaka 2026 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026*)**.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 26 Juni, 2026 katika Kikao cha Hamsini na Nane cha Mkutano wa Tatu, Muswada huu ulisomwa Mara ya Kwanza kwa mujibu wa kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 100 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 139 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Saidi Johari, (Mb.), siku ya Jumanne tarehe 11 Agosti, 2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 100 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni *(Public Hearing)* kuhusu Muswada huu kwa njia ya kielekroniki au kufika kwenye kikao cha kamati kilichofanyika siku ya Jumatano tarehe 12 Agosti, 2026. Kwa upekee Kamati inapenda kuwashukuru wadau wote kwa kutoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

**Aidha,** Katika Mkutano huo, jumla ya wadau 32 kutoka katika vyama na asasi za kiraia 7 walifika na kutoa maoni yao.
Vyama na asasi hizo ni: -

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS);
(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
(iii) Jukwaa la Ardhi;
(iv) LANDESA;
(v) Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT);
(vi) Anti-Corruption Voices Foundation; na (vii) Haki Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kuchambua maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya mtoa hoja na maoni ya wadau. Kupitia uchambuzi huo, Kamati iliandaa jedwali la maoni na kuliwasilisha Serikalini ili kupata ufafanuzi wa maboresho mbalimbali ya Muswada ikiwa ni uzingatiaji wa Kanuni ya 100(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

Aidha**,** tarehe 18 Agosti, 2026 Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mashauriano kuhusu Ibara mbalimbali za

Muswada huu. Baada ya hatua hiyo na kwa kuzingatia Kanuni ya 101 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, Kamati kupitia Mwenyekiti wake ilikujulisha rasmi kwamba imekamilisha kazi ya uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2026 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2026*) umegawanyika katika sehemu Nane (08) na unapendekeza kurekebisha sheria Saba (7) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi ya Nane zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kurekebisha Sheria Saba ambazo ni: -

a) Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116;
b) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
c) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
d) Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura ya 61;
e) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449;
f) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138; na
g) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilichambua Ibara zote ishirini na sita (26) za Muswada huu. Katika uchambuzi huo, Kamati ilikubaliana na marekebisho yanayopendekezwa isipokuwa kwa baadhi ya Ibara ambazo Kamati ilipendekeza maboresho ambayo yalikubaliwa na

Serikali. Uchambuzi kuhusu sehemu za Muswada huo na Ibara zake ni kama ifuatavyo: -

## 2.2 Ibara za Muswada wa Sheria Zilizofanyiwa Maboresho na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ilibaini mapungufu katika marekebisho ya sheria Sita kati ya sheria Saba zinazopendekezwa kurekebishwa. Sheria hizo ni: -

(i) Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116;
(ii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
(iii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
(iv) Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449;
(v) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138; na
(vi) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

### 2.2.1 **Marekebisho ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Pili ya Muswada kuanzia Ibara ya 3 hadi ya 7. Uchambuzi wa Kamati ulibaini mapungufu katika Ibara tatu ambazo ni Ibara ya 4, 5 na 6. Ufafanuzi wa Ibara hizo ni kama ifuatavyo: -

(a) Ibara ya 4 ya Muswada inarekebisha **Kifungu cha 6** cha Sheria hii ili kuweka muda wa wajumbe wa Tume ya Mipango ya Ardhi kushika madaraka kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu na kuwa na uwezekano wa kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ilivyo sasa, Kifungu cha 6 hakitoi sharti la ukomo wa muda wa kushika Madaraka kwa wajumbe wa Tume ya

Mipango ya Matumizi ya Ardhi,na hivyo marekebisho haya yanalenga kutatua jambo hilo kwa kuweka muda.

Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, sheria ilivyo sasa, inaainisha sekta ambazo wajumbe wanaweza kuteuliwa, pasipokutaja sifa za wajumbe watakaoteuliwa. Hali hii inaweza kusababisha kuteuliwa kwa wajumbe wasiokuwa na uzoefu au utalaamu wa kutosha, ilimradi tu wanatokea katika sekta zilizoainishwa kwenye sheria.

(b) Ibara ya 5 inarekebisha **Kifungu cha 7** cha Sheria kwa kuongeza **Kifungu Kipya cha 7A** ili kuipatia Tume ya Mipango ya Ardhi mamlaka ya kuwekeza. Kabla ya marekebisho yanayopendekezwa, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, haijatoa mamlaka kwa Tume kuwekeza fedha zake. Kamati ilielezwa kuwa, lengo la maboresho haya ni kuongeza vyanzo vya mapato ya Tume.

Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, kifungu cha 14 cha sheria hiyo kinachotaja vyanzo vya fedha za Tume, hakijaweka chanzo cha fedha zinazotokana na uwekezaji na vilevile si sehemu ya maboresho yanayopendekezwa. Hali hii inaweza kusababisha mapato ya Tume yanayoweza kupatikana kutokana na shughuli za uwekezaji yasitambulike kisheria kama chanzo cha mapato ya Tume.

(c) Ibara ya 6 inapendekeza kurekebisha **Kifungu cha 25(1)** cha sheria ili kuweka sharti la mamlaka za upangaji wa matumizi ya ardhi kushauriana na Tume ya Mipango ya Ardhi kabla ya kutangaza sehemu kuwa eneo la mpango. Sheria ilivyo sasa, inaziruhusu mamlaka hizo kutangaza eneo la mpango bila kushauriana na Tume. Marekebisho yaliyoletwa, yanaweka sharti la mamlaka za upangaji kushauriana na Tume, na hivyo kutatua changamoto iliyokuwepo. Licha ya hatua hii kubwa iliyochukuliwa na serikali, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, kushauriana pekee hakuipi Tume uwezo wa kutoa maelekezo yatakayopaswa kufuatwa na mamlaka za upangaji wa ardhi. Mamlaka za upangaji zina hiyari ya

kuzingatia ushauri wa Tume. Hali hii inaweza kusababisha mipango ya ardhi inayoandaliwa na mamlaka za upangaji isikidhi vigezo au isifuatwe.

### 2.2.2 Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika **sehemu ya Tatu** ya Muswada kuanzia **Ibara ya 8** hadi **Ibara ya 9**. Katika sheria hii, Kamati ilipendekeza maboresho kwenye Ibara ya 9 inayorekebisha **Kifungu cha 38 cha sheria.**

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, lengo la marekebisho ni kubadili muda wa kushika madaraka wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya kuwa miaka mitano badala ya mwaka mmoja. Baada ya marekebisho haya kuridhiwa na kuwa sheria, muda wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri utaendana na muda wa kushika madaraka wa Mwenyekiti wa Halmashauri.

Kamati inatoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa hatua hii za kuleta Muswada huu ili kurekebisha hali iliyokuwepo kwani italeta ufanisi ikiwa ni pamoja na kuondoa migogoro ya kisiasa iliyokuwa inasababishwa na uwepo wa uchaguzi wa Makamu mwenyekiti kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuunga mkono hatua zilizochukuliwa na Serikali, Kamati ilipitia sheria yote ikiwa ni vifungu vinavyorekebishwa na ambavyo havirekibishwi. Katika kazi hiyo, Kamati ilibaini kwamba bado maeneo mbalimbali yanahitaji kurekebishwa.

Mojawapo ya kifungu kinachopaswa kurekebishwa mapema ni kifungu cha 38(8). Kifungu hicho kinalipatia mamlaka Baraza la Halmashauri la wilaya kumuondoa madarakani Mwenyekiti wa Halmashauri kwa azimio linaloungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe. Sharti hilo halimtaji Makamu Mwenyekiti licha ya kuongezewa muda wa kushikilia madaraka kuwa miaka mitano kama ilivyo kwa Mwenyekiti. Hali hii haiweki usawa wa kisheria kwa

viongozi wa Baraza licha ya kwamba wote kwa sasa watakaa madarakani kwa kipindi cha muda unaolingana wa miaka mitano.

### 2.2.3 Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika Sehemu ya Nne ya Muswada, kuanzia Ibara ya 10 hadi 12. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Ibara ya 12 inaboresha sheria kuhusu suala la muda wa viongozi wa Baraza la Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Manispaa. Uchambuzi wa Kamati uliangazia masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

(a) Kama ilivyokuwa kwa sheria ya Serikali za Mitaa (Halmashuri za Wliaya), vilevile sheria ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Mji) bado inahitaji kutazamwa zaidi katika maeneo mengine ili yaboreshwe kuendana na wakati. Mojawapo ya kifungu kinachopaswa kurekebishwa mapema ni kifungu cha 27(6). Kifungu hicho kinalipatia mamlaka Baraza la Halmashauri ya manispaa au hamlashauri ya mji kumuondoa madarakani Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri ya mji kwa azimio linaloungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe. Sharti hilo halimtaji Naibu Meya au Makamu Mwenyekiti licha ya kuongezewa muda wa kushika madaraka kuwa miaka mitano kama ilivyo kwa Meya au Mwenyekiti, na hivyo kukosekana kwa usawa wa ksheria kwa viongozi hao.

(b) Ibara ya 12 inarekebisha kifungu cha 27(4) cha sheria ili Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa au Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji ashike madaraka kwa muda wa miaka mitano kama ilivyo kwa Meya na Mwenyekiti. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, baada ya marekebisho hayo, mpangilio wa viongozi haujazingatia itifaki ya viongozi, jambo linaloweza kukiuka misingi ya utawala bora; na

(c) Kifungu cha 27(4) kinachorekebishwa na Ibara ya 12 kitawezesha Baraza la Halmashauri ya Manispaa, mji au Halmashauri ya wilaya kufanya uamuzi wa kufupisha muda wa Meya,

Mwenyekiti, Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti kushika madaraka chini ya muda wa miaka mitano. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, marekebisho hayo hayaja ainisha mazingira ambayo yanaweza kuruhusu Baraza kufikia uamuzi huo, na hivyo kuleta utata katika utekelezaji.

### 2.2.4 Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Sita ya Muswada na yanahusu Ibara ya 15 na 16. **Ibara ya 16** inarekebisha **Kifungu cha 11** cha sheria kwa lengo la kutambua makubaliano ya pande mbili za mkataba katika sekta ya uziduaji (extractive industry) kuhusu utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza. Mkataba utakaokidhi vigezo vya masharti yake kutambuliwa ni ule ulioidhinishwa na Baraza la mawaziri na wenye masharti ya aina hiyo.

Kwa wale ambao mikataba yao imekidhi masharti haya, wanaruhusiwa kwenda kutatua migogoro yao katika vyombo mbalimbali walivyochagua wao ikiwemo vyombo vya nje ya nchi na kwa kutumia sheria nyingine walizochagua. Kwa sababu hiyo, hawatafungwa na masharti ya Kifungu cha 11(3) cha sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11(3) cha sheria kilivyo sasa, kimeweka sharti kuwa migogoro yote inayohusu sekta ya uziduaji kwa rasilimali asilia zinazopapatikana nchini Tanzania itaamuliwa na vyombo vilivyopo nchini Tanzania kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, marekebisho yanayopendekezwa yanaweka mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji mkubwa katika sekta ya uziduaji. Aidha, marekebisho yanalenga kuheshimu makubaliano halali yaliyofikiwa baina ya pande mbili (*sanctity of contract*) ikiwa ni pamoja na kuendana na mabadiliko ya kidunia.

Licha ya hatua hii muhimu, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba masharti yanayotaka migogoro inayotokana na sekta ya uziduaji kwa rasilimali asilia zinazopatikana nchini kutatuliwa nchini yangeweza kutekelezeka bila ya changamoto yoyote endapo kungeanzishwa hapa nchini vyombo vyenye hadhi ya Kimataifa vya utatuzi wa migogoro ya uwekezaji. **Kamati inashauri Serikali kuanzisha vyombo hivyo mapema iwezekanavyo ili kuwezesha migogoro hiyo kutatuliwa hapa nchini**.

### 2.2.5 Marekebisho ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138

**Mheshimiwa Spika;** marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Saba ya Muswada kuanzia Ibara ya 18 hadi 23. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba marekebisho ya sheria hii yanahusu masuala mbalimbali katika sekta ya uthaminishaji. Baadhi ya masuala hayo ni: -

(a) Ibara ya 18 inaongeza fasili ya neno **"asset"** na kurekebisha fasili ya neno **"valuation"** kwa kuongeza maneno "***or asset***". Mapendekezo haya yanaongeza wigo wa shughuli za uthamini kutoka kwenye mali (*property*) pekee na kujumuisha mali zote zenye thamani ya kiuchumi (*assets*) ikiwemo na mali nyingine zisizoshikika kama vile hisa, mitaji, hakimiliki na bunifu mbalimbali.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, fasili inayopendekezwa ni pana na inaweza kusababisha Sheria ya Uthamini ionekane kugusa aina za mali zinazodhibitiwa na sheria na mamlaka nyingine, ikiwemo mali za kifedha, hisa/mitaji, haki miliki na sekta maalumu nyingine. Jambo hili linaweza kuleta mgongano wa kisheria na mwingiliano wa kazi kati ya taasisi moja na nyingine.

(b) Ibara ya 19 inarekebisha **Kifungu cha 6** cha Sheria kwa kuongeza **Kifungu kipya cha 6(3)** ili kumpa Mthamini Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa msamaha wa ada zinazolipwa kwa huduma zinazotolewa na Wathamini wa Serikali baada ya kupata idhini ya Waziri.

Sheria ilivyo sasa, Mthamini Mkuu wa Serikali ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za uthamini nchini mwenye jukumu la kuratibu, kusimamia na kuhakikisha huduma za uthamini zinatolewa kwa kuzingatia Sheria na viwango vya kitaaluma. Hata hivyo, Sheria haimpi mamlaka ya kusamehe ada zinazotozwa kwa huduma zinazotolewa na Wathamini wa Serikali. Jambo hilo husababisha huduma zote za uthamini kutozwa ada kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa.

Licha ya pendekezo hili kuwa zuri, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Ibara haijaweka aina ya kazi/huduma zinazoweza kusamehewa, vigezo vya kutoa au kukataa msamaha. Aidha, kwa kuwa mthamini wa serikali anaweza pia kufanya kazi ya uthamini kama mthamini binafsi, marekebisho yalivyo sasa yanaweza kutafsiriwa kuruhusu msamaha hata kwa kazi binafsi zinazofanywa na wathamini wa serikali.

Hali hii inaweza kuwa na athari za kuinyima serikali mapato, pamoja na kutokuwa na ushindani wenye usawa baina ya wathamini binafsi na wathamini wa serikali pindi wanapofanya kazi binafsi.

### 2.2.6 **Marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283**

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho ya sheria hii yanapatikana katika sehemu ya Nane ya Muswada kuanzia Ibara ya 24 hadi 26. **Ibara ya 25** inarekebisha **Kifungu cha 111(1)(a) na (3)** cha Sheria kwa kufuta neno "**livestock".** Vilevile, **Ibara ya 26** inarekebisha **Kifungu cha 116(3)(b)** cha Sheria hiyo kwa kufuta neno “**livestock**”.

Marekebisho haya yanalengo la kuiondoa mifugo katika orodha ya mali zinazoweza kutaifishwa baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya Sheria ya uhifahi wa wanyamapori. Sheria ilivyo sasa, Mahakama ina mamlaka ya kuamuru kutaifishwa kwa mifugo endapo imekuwa ni sehemu ya ukiukwaji wa sheria ya Wanyamapori. Vilevile, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Wanyamapori anaweza kutaifisha mali mbalimbali ikiwemo mifugo endapo

amefifilisha kosa lililokiuka masharti ya sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, licha ya hatua hii nzuri inayolenga kulinda haki za wafugaji na mifugo, na kuhakikisha nchi inakuwa na hifadhi za wanyamapori na misitu endelevu, uchambuzi wa Kamati ikiwa ni pamoja na kupitia hukumu mbalimbali za mahakama zilizohusu mifugo umebaini kwamba bado zipo sheria nyingine zinazoruhusu mifugo kutaifishwa, kushikiliwa na kuuzwa ambazo si sehemu ya marekebisho haya. Hali hii inaweza kusababisha changamoto ya mifugo kutaifishwa kuendelea kwa kutumia sheria nyingine licha ya marekebisho haya.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mbali na mifugo kutaifishwa, mojawapo ya changamoto zinazosababisha wafugaji kutokurejeshewa mifugo yao mara baada ya mahakama kutowakuta na hatia ni mifugo yao kufa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo magonjwa, kukosa chakula, kurundikana kwenye sehemu isiyokuwa na nafasi na kujeruhiwa na Wanyama wakali.

Aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba, zipo sheria ikiwemo sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 na kanuni zake zinaainisha haki za mifugo pindi inaposhikiliwa kutokana na makosa ya wafugaji.

Haki hizo ni kupewa chakula cha kutosha, maji ya kunywa, matibabu na kuwekwa kwenye sehemu yenye nafasi ya kutosha. Endapo masharti ya sheria na kanuni hizo yatazingatiwa, ni vigumu wafugaji ambao hawajakutwa na hatia kushindwa kupata mifugo yao iliyokuwa inashikiliwa pindi shauri linapohitimishwa mahakamani.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada huu isipokuwa kwa baadhi ya maeneo

ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya maboresho mbalimbali katika Muswada huu. Maoni hayo yanafafanuliwa katika kama ifuatavyo: -

### 3.1 Maboresho kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116

(a) Sheria haijataja uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Mipango ya Ardhi wawe na sifa na uzoefu gani. Hali hii inaweza kusababisha uteuzi wa wajumbe wa Tume wasiokuwa na utalaamu na uzoefu wa kutosha. Hivyo basi, Kamati iliishauri Ibara ya 4 ya Muswada iboreshwe ili kuweka sifa hizo. Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati na kuboresha Ibara ya 4 kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(b) **Ibara ya 5** ya Muswada inaongeza **Kifungu cha 7A** ili kuipa Tume mamlaka ya kuwekeza fedha zake kwa kuzingatia maelekezo ya "mamlaka husika". Kifungu cha 14 cha sheria hii kinataja vyanzo vya mapato vya Tume, ambapo mapato kutokana na uwekezaji hayajatajwa. Kamati imeshauri kifungu cha 14 kirekeishwe ili kutambua mapato yatokanayo na uwekezaji. Serikali imekubali ushauri wa Kamati kwa kuongeza Ibara ya 6 mara baada ya Ibara ya 5 kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la serikali.

(c) Ibara ya 6 ya Muswada inatoa wajibu kwa Tume ya Mipango ya Ardhi kushauriana na mamlaka za upangaji kabla ya mamlaka kutangaza sehemu kuwa eneo la mpango. Hata hivyo, suala la kushauriana ni la hiyari na mamlaka za upangaji zina uhiyari wa kuzingatia ushaueri au la. Kamati imependekeza Tume iwe na mamlaka yanayowezesha mbali na ushauri kwa masuala yanayohitaji ushauri, mamlaka ya kutoa maelekezo kwa masuala ambayo hayahitaji ushauri.

Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuongeza Ibara ya 7 mara baada ya Ibara ya 5 kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la serikali.

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287

(a) Mara baada ya sheria hii kurekebishwa ili kuruhusu Makamu Mwenyekiti wa Halmsahuri ya wilaya kushikilia madaraka kwa kipindi cha muda wa miaka mitano kama ilivyo kwa Mwenyekiti, Kifungu cha 38(8) cha Sheria kinacholipatia Baraza mamlaka ya kumuondoa madarakani Mwenyekiti kwa azimio linaloungwa mkono na theluthi mbili ya wajumbe kirekebishwe ili kumjumuisha Makamu Mwenyekiti na hivyo kuleta usawa wa kisheria. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho ya Ibara ya 9 kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288

(a) Ibara ya 12 inarekebisha sheria ili kuwajumuisha Meya, Mwenyekiti, Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya manipaa, mji na wilaya mtawalia wote kukaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano. Ibara hiyo Iboreshwe ili uainishaji wa viongozi hao uzingatie itifaki. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 12 kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(b) Ibara ya 12 iboreshwe kwa kurekebisha Kifungu cha 27(6) cha Sheria ili kumjumuisha Naibu Meya wa Manispaa na Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Mji kuwa na uwezekano wa kuondolewa madarakani kama ilivyo kwa Meya wa Manispaa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 12 kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(c) Kifungu cha 27(4) chas heria kinachorekebishwa na Ibara ya 12 kitawezesha Baraza la Halmashauri ya Manispaa, mji au Halmashauri ya wilaya kufanya uamuzi wa kufupisha muda wa Meya,

Mwenyekiti, Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti kushikilia madaraka chini ya muda wa miaka mitano. Kifungu hicho kiboreshwe ili kiweze kuainisha mazingira ambayo yanaweza kupelekea Baraza kufikia uamuzi huo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 12 kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### 3.4 Marekebisho ya Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138

(a) **Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 18 inayoweka fasili ya neno **"asset**" inongeza wigo wa shughuli za uthamini kutoka kwenye mali (*property*) pekee na kujumuisha mali zote zenye thamani ya kiuchumi (*assets*) ikiwemo mali zisizoshikika ikiwemo hisa, mitaji na hakimiliki na bunifu. Fasili hiyo ni pana, na inaweza kukinzana na sheria za mamlaka nyingine zinazosimamiwa mali zisizoshikika. Ibara iboreshwe kwa kuongeza maneno "**subject to other written laws**" katika matumizi ya fasili ya neno "asset" ili kuzuia mgongano huo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 19 kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

(b) katika Ibara ya 19 inarekebisha **Kifungu cha 6** cha Sheria ili kumpa Mthamini Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa msamaha wa ada zinazolipwa kwa huduma zinazotolewa na Wathamini wa Serikali baada ya kupata idhini ya Waziri.

Ibara iboreshwe kuwa kuweka aina ya kazi/huduma zinazoweza kusamehewa, vigezo vya kutoa au kukataa msamaha. Vilevile, Ibara hiyo iboreshwe ili kutenganisha kazi binafsi ya uthamini inayoweza kufanywa na wathamini wa serikali na kazi za serikali zinazoweza kufanywa na wathamini wa serikali.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri huo na kuboresha Ibara ya 19 na 23 ya Muswada kupitia jedwali la marekebisho la Serikali.

### 3.5 Marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283

(a) Ibara ya 25 na 26 ya Muswada inarekebisha sheria hii ili kuzuia mifugo ya wafugaji kutaifishwa. Hata hivyo, zipo sheria nyingine zenye vifungu vinavyoruhusu mifugo kutaifishwa, ikiwemo sheria ya misitu, TANAPA na Ngorongoro. Kamati ilishauri Serikali ilete marekebisho ya sheria hizo, na serikali mbele ya Kamati kupitia Jedwali la hoja za Kamati imeeleza kuwa marekebisho ya Sheria hizo yatawasilishwa katika Mkutano wa Tano wa Bunge la 13.

(b) Pamoja na marekebisho ya sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori na sheria nyingine ambazo serikali imeahidi kuzileta hapa Bungeni, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za kuwawajibisha binafsi watendaji wote wanaoshikilia mifugo huku wakikiuka masharti ya sheria nyingine ikiwemo sheria ya Ustawi wa Wanyama na Kanuni zake kwa kutoipatia mifugo haki zake pindi wanaipoishikiliwa kwa sababu mbalimbali.

#### 3.5.1 Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 449

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho ya sheria hii yanalengo la kutambua makubaliano ya pande mbili za mkataba katika sekta ya uziduaji kuhusu utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza. Kwa pande ambazo mikataba yao imekidhi masharti haya ikiwa ni pamoja na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri, wanaruhusiwa kwenda kutatua migogoro yao katika vyombo mbalimbali walivyochagua wao ikiwemo vyombo vya nje ya nchi na kwa kutumia sheria **walizochagua.**

Kamati inaamini kwamba endapo kungeanzishwa kituo cha usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji chenye hadhi ya Kimataifa hapa nchini, migogoro hiyo ingetatuliwa hapa nchini kama ilivyokusudiwa hapo awali na sheria hii. **Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba Serikali ianzishe kituo cha usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji hapa nchini chenye hadhi ya Kimataifa ikiwa ni pamoja**

**na kuandaa watalaamu wa kutosha waliobobea katika masuala ya usuluhishi wa migogoro ya uwekezaji mkubwa.**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Wajumbe
4. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Wajumbe
5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb - Wajumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Wajumbe
7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb - Wajumbe
8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb - Wajumbe
9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb - Wajumbe
10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb - Wajumbe
11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb - Wajumbe
12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb - Wajumbe
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb -Wajumbe
14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb - Wajumbe
15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb - Wajumbe
16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb - Wajumbe
17. Mhe. Dkt. Yahaya Esmail Nawanda, Mb - Wajumbe
18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb - Wajumbe
19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb - Wajumbe
20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb - Wajumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Juma Zuberi Homera, Mb, na Naibu Waziri wake Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb kwa ushirikiano wao mzuri na wa kipekee walioipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Kamati pia inampongeza kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari, Mb akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali ***(CPD)*** Ndg. Onorius Njole kwa kuandaa Muswada huu baada ya kubaini makosa mbalimbali katika Sheria wakati wa utekelezaji wake.

**Aidha**, Kamati inawashukuru pia watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wote kutoka taasisi mbalimbali zinazohusika na usimamizi na utekelezaji wa Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii; na kwa upekee niishukuru sekretarieti ya Kamati iliyohusika na uratibu wa vikao vya uchambuzi wa Muswada hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2026 (*The***

***Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026*)** Pamoja na Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Dkt. Damas Daniel Ndumbaro Mb.

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA,**
**KATIBA NA SHERIA**
2 SEPTEMBA, 2026

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo tunakushukuru kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati. Sasa tunaingia katika hatua ya uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, ajiandae Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ajiandae Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na ninamshukuru Mwenyezi Mungu ametupa afya njema na tumeamka salama leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda niseme jambo moja hapa, Bungeni hapa kuna watu wengi sana wanakuwa wananiita Daktari, Daktari, sasa kwa sababu nilikuwa naitwa kwenye *corridor,* huko sikujali sana, lakini alivyokuja Waziri wa TAMISEMI, Profesa Shemdoe wakati anajibu swali akasema Dkt. Olelekaita! Sasa mimi siyo Daktari kwa hiyo, hilo ieleweke.

**MBUNGE FULANI:** *Material* zako za kidaktari!*(Kicheko)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwanza ninakupongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kweli, kama siyo umejichanganya tu kumleta shemeji

yetu hapa, wafugaji leo wangekupa mke, kwa sababu ya kifungu hiki cha wanyamapori. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Wanyamapori kile kimetesa watu na nimefurahi sana kwa sababu unajua umezungumza wazi kabisa kwamba haikuwa na *proportionality test* kuwepo pale, sasa unajua wakati naangalia ilibidi niangalie *the legal history* ya hicho kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kuchukua sheria ile ya Fauna kuanzia 1951 haikuwepo, 1974 haikuwepo *somehow* ikaja tu ikaingia kwenye Sheria hii ya 2009 lakini pamoja na kwamba ni kweli hai-*met* ile *proportionate test* ambayo ni jambo kubwa la kisheria. *In fact,* ningekuwa mahakamani ningesema hii imewekwa ki-*mathematics,* ki-*engineering*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma soma hicho kifungu hicho hata sijui imeingizwaje lakini *thank you*. Wewe kwa kweli utaingia kwenye historia ya kwamba wakati fulani tunaendelea kubadilisha sheria zetu ili ziendelee ku-*meet standards* za kisheria. Kwa hiyo, kwa kweli nikushukuru sana na shemeji yetu tuendelee kumwambia akutunze sana, kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuandika sheria siyo jambo jepesi sana, kuandika sheria ni jambo gumu sana kwa sababu inahitaji kutabiri tabia za watu, kwamba baada ya muda gani lakini pia una-*balance* maslahi na maslahi ya jamii zinazokinzana huku ukizingatia usahihi wa sheria. Kwa hiyo, siyo kazi ndogo sana ni kazi nzito, kubwa, wewe kwa kweli na *Parliamentary Drafts Person* yule mna kazi kubwa sana ya kizalendo kwa kweli, kwa hiyo, muendelee hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa namwangalia Mwalimu Nyerere, hivi Mwalimu Nyerere alionaje sheria? ali-*view* sheria namna gani? Mwalimu Nyerere ali-*view* sheria, nitanukuu: "*laws are not merely as tools for punishment or control but as instruments for social justice, equity and collective welfare of the community*". Rais wa

Marekani anaitwa Rosevelt anasema hivi: "*It is difficult to make our material condition better by the best law, but it's easy enough to ruin it by a bad law*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli marekebisho ya sheria hii ya wanyamapori ilivyoandikwa na watu walivyokuwa wanatekeleza ilikuwa inaleta aibu kubwa sana. Kwa hiyo, kwa kweli Mheshimiwa *Attorney General* na Serikali mbarikiwe sana kwa kuona hili. Kwa kweli Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa inataka watanzania baada ya miaka 25 wawe na Dola 7,000. Kwa hiyo, *intention* ya Serikali ni kufanya watanzania hawa wawe matajiri siyo kuwa-*impoverish*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli kama walivyosema Kamati *this is a very good start, very good*. Wafugaji leo nchini watakuwa wamefurahi sana, Mwenyezi Mungu akubariki sana na tuendelee hivyo hivyo kwa sababu dira yetu inasema tuangalie sheria zetu kama alivyosema rafiki yangu Mheshimiwa Mwinyi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi sisi tunaangalia, tunachukua Dira hii ya Taifa ya 2050 halafu tunaangalia kupitia kwenye sheria tunaona ina *balance perfectly*, kwa hiyo, *well-done*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Sheria hii inaitwa *Natural Wealth and Permanent Sovereignty*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Alaa! Muda umekwisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nawapongeza wote na majirani zangu hapa tuendelee, hii kazi imekwenda vizuri na wote hapa tunakubaliana na chote walichosema Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilimtaja Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ajiandae Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji wetu ni dakika tano tukizingatia kwamba Saa Nane tuna ratiba nyingine muhimu.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa wakati mwingine mzuri mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwanza, moja kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kufanya mapitio ya sheria mbalimbali ambapo kama watanzania tunapata fursa ya kujisahihisha kwenye baadhi ya mienendo ambayo tumekuwa tukiishi kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nijielekeze moja kwa moja kwenye marekebisho ya Sheria Kifungu kile cha Ibara 25 ambacho kinazungumzia masuala ya kufuta ile Sheria ya Utaifishaji wa Mifugo. Kwanza nikiri kwamba Serikali imeona haja kubwa ya kutengeneza usawa na kutengeneza haki ya usimamizi wa rasilimali ambazo zinazalisha na kuleta maendeleo kwa watanzania, moja kati ya maeneo hayo ni eneo la wafugaji na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwa sababu imetazamwa haki vizuri kabisa inayomhusu mfugaji. Sambamba na kazi hii nzuri iliyofanyika ya kufuta Sheria ya Utaifishaji wa Mifugo nafikiri tumetazama maeneo kadhaa na eneo la kwanza hata katika nyongeza ya Kamati katika pendekezo la sheria inayopaswa

kuja kutazamwa vizuri wameitazama eneo la *TANAPA*, wameitazama Ngorongoro na wametazama na maeneo mengine yanayohusiana na uhifadhi. Kama kuna eneo tunapaswa kulitazama katika misingi ya usawa kwenye haki ya makundi, eneo mojawapo ni eneo la wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba ipo Mikoa ambako sheria hii kabla haijapendekezwa kufuta bado Mikoa hii ilikuwa kwenye taharuki, shida na matatizo makubwa sana ya mifugo kuingia kwenye mashamba ya wakulima. Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Songwe na Pwani ni wahanga wa mifugo kuingizwa kwenye mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mwelekeo wangu? Sina haja ya kupingana na mabadiliko na marekebisho ya sheria hii. Hata hivyo, napenda kujua Mwanasheria Mkuu atakapokuja aniambie kama sheria hii ya kuondoa utaifishaji wa mifugo haitakuwa kichaka, narudia tena haitakuwa kichaka kwa baadhi ya wafugaji kuitumia sheria hii mpya kwamba hawataifishiwi mifugo yao na kwenda kudhuru pia kwenda kuharibu mazao ya wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya sheria hii, imetamkwa neno "haki" na "haki" iliyotamkwa hapa, mimi ninafahamu kwamba, moja, mifugo isiporwe ili wafugaji wawe matajiri; pili, mifugo hii iendelee kuchangia pato la Taifa kwa wale wafugaji kuishi kwa usalama na amani; na tatu, tulete hoja ya kuondoa umaskini kwa mfugaji kupata kipato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sheria hii imelenga mwono huo kwa wafugaji, basi Mwanasheria Mkuu atuambie, ni sheria ipi itakwenda sasa ku-*cover* ili kumsaidia mkulima mwenye mbaazi, ili mbaazi yake impe fedha na awe tajiri, imsaidie mkulima wa Nachingwea, ili anapokuwa shambani awe na hakika hatapigwa na kuondolewa utu wake na mfugaji kwa kosa la kumpiga, kumdhuru na kumfanyia *humiliation*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu huko kwetu Mheshimiwa Olelekaita hapa *Advocate* ninayempenda sana na kumwamini, ametamani kumpa mke kaka yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninataka nimhakikishie Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sheria hii kama haitafafanuliwa sehemu gani itawasaidia wakulima, kama shemeji yetu ni wa kusini, tunamchukua, atakuwa wa kwetu, tunaondoka naye, kwa sababu tunataka tuone eneo ambalo wakulima watanufaika na kufutwa kwa Sheria ya Utaifishaji wa Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, sheria hii wakati inatekelezwa, kule kwetu haikuwaki kufanya kazi ipasavyo kwa wafugaji hawa kutaifishiwa mifugo yao, ila bado iliendelea kuleta zahama kubwa. Hata hiyo *penalty* tunayoitamani iwe, kama ndiyo kifichio cha sheria hii, bado utekelezaji wake utaumiza wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect*, ninawaheshimu wafugaji na ninawapenda, tunaomba Mwanasheria Mkuu atusaidie namna atakavyoweza kuilinda sheria iliyofutwa iendelee kuwasaidia wakulima wanaolima mazao yao. Ahsante sana ninaunga mkono hoja.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ameshamaliza Mheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, ajiandae Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kupata baraka ya kusimama katika Bunge hili. Pamoja na kumshukuru Mungu, pia ninaomba nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya na mabadiliko ya Sheria mbalimbali ambayo ameyaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Tumepitia hizo sheria na kutoa mapendekezo yetu. Leo ninaomba nizungumzie Sheria ya Serikali za Mitaa, mamlaka zile za ngazi za wilaya na hasa kwenye eneo lile la kumpata Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Bahati nzuri na mimi nimeshakuwa Diwani kwa vipindi vitano, lakini nikiwa Diwani, pia nilibahatika kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati tumekubaliana moja kwa moja na haya mabadiliko, na sababu mbalimbali zilitolewa kwenye Kamati yetu, kwanza, kufanya uchaguzi katika kila mwaka ni usumbufu sana. Sisi tukakubali moja kwa moja mapendekezo ya Serikali kwamba ni vizuri tupate Makamu Mwenyekiti na yeye pia akae katika kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wanasiasa pia tunafahamu, kunapokuwa na uchaguzi, pia kunakuwa na mipasuko. Ni lazima watu kila mmoja anakuwa na matamanio yake. Kwa hiyo, kwa pendekezo hili kwa mwaka mmoja, mtu anakuwa hajashusha pumzi, lakini kwa miaka mitano vile anavyokwenda kama anavyochaguliwa Mwenyekiti wa Halmashauri, sisi tumekubaliana moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamoja na kukubali, tumeendelea kusema kwenye Kamati kwamba ziko sheria nyingine zinatakiwa zipitiwe upya. Kwa nafasi hii pia ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa *ALAT*. Ninafahamu kwenye kikao cha *ALAT* ambacho kilifanyika Arusha, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa hii hoja na awamu iliyopita wakati anaahirisha Bunge alisema pia matamanio yake ya kuona tunamchagua Makamu Mwenyekiti kama vile tunavyochagua Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati, bila kigugumizi, tulikubaliana, na mimi niwashawishi Wabunge wenzangu, twendeni

tukubaliane kwa sababu na sisi ni sehemu ya Madiwani, tukiwa kwenye Mabaraza ya Madiwani, tunaona usumbufu wa kufanya uchaguzi kila mwaka. Ni vizuri tukae miaka mitano, na baada ya miaka mitano apatikane Makamu Mwenyekiti mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nitumie fursa hii, kama vile ambavyo tumeongea kwenye Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria. Tumemwomba Mwanasheria aende akapitie sheria nyingine ambazo tunahisi kwa sasa zimepitwa na wakati. Tunapozungumzia Madiwani, ukija kwenye Halmashauri, kuna Madiwani wa Kata, na pia kuna Madiwani wa Viti Maalum, kama tulivyo sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukija kwenye zile sheria, Diwani wa Viti Maalum haruhusiwi kugombea kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri. Mimi kwangu bado naona ni sheria kandamizi. Inawezekana Madiwani wenzie watampenda, lakini kwa sababu tu sheria haimruhusu, hawezi kugombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, hata sisi Wabunge wa Viti Maalum humu ndani tunafanya kazi kubwa ya kupitisha mambo mbalimbali katika hili Bunge, lakini ukirudi kwenye halmashauri, wewe sio Mjumbe wa Kamati ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu, ukiwa kwenye Kamati ya Fedha, unapata nafasi ya kujadili mambo mbalimbali, utazungumzia masuala ya mikopo, ni tofauti na unavyokaa kwenye Baraza la Madiwani, kwa sababu Baraza la Madiwani lina ukomo wa kuchangia. Huwezi kupata nafasi ya kuchangia mara mbili kwenye ajenda moja, lakini ukiwa kwenye Kamati ya Fedha utapata nafasi ya kuchangia kwa kina masuala yanayohusu akina mama wenzetu, na masuala yanayohusu afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia Kamati hii nilishauri, na bahati nzuri sisi Wajumbe wa Kamati, lakini pamoja na hizi sheria ambazo tunapitisha, na kwa kweli ni sahihi kabisa kupitisha, tunamwomba Mwanasheria arudi akapitie na hizo sheria nyingine

ambazo sisi tunahisi hatutendewi haki. Mimi nimeona niyaseme hayo kwa kuthamini mchango mzuri ambao unatolewa na Wabunge wanawake na Madiwani wanawake kwenye Bunge hili lakini pia kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti tunafahamu sana kazi nzuri inayofanyika na Mwanasheria wetu na bahati nzuri Mwanasheria huyu ni msikivu, hivi hapa ninavyosema anaandika pale anaenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, mchango wangu ulikuwa huo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, ajiandae Mheshimiwa Isack Joseph Copriano.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwanza ninaunga mkono hoja, nisije nikajisahau huko mbele, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utashi huu kwa kuleta huu Muswada hapa. Imekuja Miswada mbalimbali, lakini hasa ninazungumzia upande wa wafugaji na matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi ni chama cha wakulima na wafanyakazi, na hili halijabadilika. Kwa hiyo, Muswada huu kwa kweli una-*address* ile *core* ya chama chetu, kwamba tunajali wakulima na wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri mwenye dhamana na vilevile Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwani jana nilikuwa ninamsikiliza vizuri sana, na leo anafanya kazi nzuri sana na anatuhakikishia kwamba yale ambayo tunatamani kuyaona mwaka 2050, yatatimia, kwa sababu kubadilisha sheria na sera ni kitu kimoja

*core,* pengine 50% ya mabadiliko ambayo tunataka tuyaone. Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni mali kama mali nyingine na inalindwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1997, Ibara ya 24(1) na ningependa ninukuu "*Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria*." Mwisho wa kunukuu. Hii tu siyo tu kwamba inasaidia wafugaji wetu, lakini vilevile ni dalili tosha kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inaheshimu Katiba ya Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina-*declare interest,* ninatokana na wafugaji, na vilevile ninatoka katika Jimbo. Wapiga kura wangu asilimia karibu mia moja, aidha ni wafugaji au ni wakulima, na sisi kwetu kule tunafuga na kulima *at the same time*. Kwa hiyo, huu Muswada unanihusu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 14 iliyopita, wakati sheria ilipotungwa mwaka 2009 kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, tulianza harakati mwaka 2013/2014, tukatengeneza chama cha wafugaji. Hiki chama unachokiona cha wafugaji, tulikitengeneza wakati huo. Lengo lake kubwa kwanza ilikuwa ni sauti ya wafugaji isikike nchini; na pili, ni kutengeneza mahusiano bora kati ya Chama cha Wafugaji na Serikali kutokana na yaliyotokea kwa miaka karibu mitatu baada ya kutungwa ile sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na mimi nilikuwa mlezi wakati huo, nikapotea kidogo pale, lakini umenirudisha tena kuwa mlezi. Kwa hiyo, hili jambo kwangu kwa kweli linanihusu sana na ndani ya Bunge lako hili, tuna *caucus* yetu kwa Wabunge tunaotokea katika maeneo ya wafugaji. Nami nimebahatika, wameniamini kuwa Mwenyekiti wao. Vilevile nafikiri Mheshimiwa Olelekaita ni katibu wetu na Makamu wetu ni Mheshimiwa Getere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii sheria kwa kweli sisi tulikuwa tunaisubiri sana, na hili vilevile tusisahau kumshukuru sana

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninafikiri alilizungumzia hapa kwa utashi wake huo na kusema kwamba atakuwa sehemu ya kusukuma hili liweze kutokea. Kwa hiyo, hapa ninapozungumza, tunaishukuru sana Serikali kwa usikivu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa sheria nzuri sisi wafugaji imetutesa kwa muda mrefu. Kwa hiyo, hili nataka nirudie tena kwamba tunaishukuru sana Serikali yetu kwa usikivu huu, na nina imani kwamba zile sheria ambazo zimezungumzwa hapa zitatakiwa zibadilishwe ili tuondokane kabisa na hili suala kwamba wanataifisha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo kwetu ni maisha, na maisha kwetu ni mifugo. Kutaifisha mifugo ni kutaifisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba tena kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, ajiandae Mheshimiwa Arif Suleiman Premji.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Ninasimama hapa kuunga mkono hoja na ninataka niseme tu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan imeandika historia. Nimpongeze sana *AG*, ameandika historia. Hata siku moja akikaa huko nyumbani kwake atakuwa ana historia ameandika kwa Watanzania, hususan wafugaji wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sizungumzii tu nikasema labda wafugaji ni wengi. Hakika amewatendea haki wafugaji. Niseme tu, sitaki kumjibu rafiki yangu Mheshimiwa Fadhili, ni ndugu yangu, lakini kuna vitu viwili hapa lazima avitofautishe. Sheria hii na jambo ambalo tunalizungumza, ni vitu viwili tofauti. Haviingii kwenye suala la mashamba na kitu kingine. Hii inakwenda ku-*stick* kwenye maeneo yale ya Serikali hususan hifadhi za Taifa. Kwa hiyo, ni vitu

viwili tofauti. Kama kuna jambo, ni vyema alete tu kama kuna mahali anafikiri inatakiwa ifanyiwe marekebisho, lakini siyo kwenye upande huu.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu kumpa taarifa rafiki yangu Mheshimiwa Copriano *(Copricorn)* kwamba sheria hii ni nzuri, itakapoondolewa kutokutaifishwa, siyo tu kwenye hifadhi, ni mpaka kwenye mashamba ya mbaazi pia hayatataifishwa. Nilitaka tu kumpa hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea na ninamheshimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuishukuru Serikali katika vitu ambavyo vimewaumiza wafugaji wengi nchini. Hii ni juu ya utaifishaji wa mifugo. Leo jambo ambalo limefanyika ni jambo la kihistoria. Miaka ya nyuma wananchi wengi walikuwa (na hili mwelewe kabisa) hawapendi kufanya hiyo mnayofikiria labda *sometimes* ng'ombe wanatoroka wanaingia kwenye hifadhi, hujui wamekwenda; labda kijana aliyekuwepo amekuwa mzembe, sasa ng'ombe wanataifishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunasimama hapa kuishukuru Serikali ya mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Jambo hili ni zuri, ambapo *AG* na Serikali wamekaa na kuifanya. Pia niipongeze sana Kamati hii, imefanya kazi ambayo imetukuka. Binafsi ninawiwa kusema, leo ukipita kwa wafugaji hususan kwenye Jimbo langu la Monduli, Jimbo la Simanjiro, Jimbo la Kiteto, Jimbo la Ngorongoro, na maeneo mengine, kila mmoja anafurahia jambo hili

ambalo Serikali imekwenda kulifanya. Ni jambo ambalo ni la kimiujiza. Hakika…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita na hiyo itakuwa ni taarifa ya mwisho.

**TAARIFA**

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa tu taarifa nzuri sana na tuweke rekodi sawa. Hapa tunabadilisha Sheria ya Wanyamapori inayo-*govern* maeneo ya hifadhi, *(reserved lands)*. Mashamba siyo *reserved lands*. Mashamba ni kitu kingine kabisa. Ahsante, endelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa ya Mheshimiwa Olelekaita, Mwanasheria, kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kweli ninatamani kulia. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ni jambo ambalo liliwagusa wananchi wangu wa Monduli. Kwa hiyo, wamefanya jambo ambalo amekwenda kutafsiri hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 14/11/2025 kwamba anapotaka kuondoka 2030, anatamani kuacha tabasamu kwa Watanzania. Sasa ameanza kuacha tabasamu kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amepita kwenye njia yake ile anayoitaka. Alisema, "sitamani kuacha magorofa, sitamani kufanya nini, natamani niwaachie Watanzania tabasamu." Leo AG amekwenda kuwaachia Wanamonduli na Watanzania hususan wafugaji wa Tanzania, tabasamu ambalo halina mfano. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimepata bahati ya kuwa Diwani kwa miaka 15, na nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri miaka 10. Sheria hii na yenyewe inaenda kupunguza usumbufu ya watu kutokufanya uchaguzi wa kila mara. Inaenda kuondoa *loophole* nzuri ambayo wananchi wanakwenda kuwa hawarudiirudii kwenye uchaguzi. Ninaishukuru sana Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme, ninaunga mkono hoja, nimefurahishwa sana mpaka nimeshindwa kusema juu ya hii sheria iliyofanyiwa marekebisho ya kutokutaifisha mifugo ya Watanzania. Hii ndiyo ilikuwa benki ya wafugaji wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, ajiandae Mheshimiwa Dickson Lutevele.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninashukuru kwa fursa niliyopewa ya kuchangia. Kuna *philosopher* mkubwa tu Marekani aliwahi kusema, "*The law is a living thing, it must grow*." Huyu alikuwa ni *Oliver Wendell Holmes Jr.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* ambayo tunaenda kufanya ni kwenye Sheria ya Uthamini Sura 138, Kifungu cha 51(1)(a) na (e) na Kifungu cha 52(2). Vifungu hivi kwenye Sheria hiyo ya Uthamini Sura 138, ni moja ya chanzo cha umaskini kwa wananchi wa vijijini. Ninasema hivyo kwa nini? Kifungu cha 51(1)(a) kinasema *Direct Market Comparative Method* na kifungu hicho hicho 51(1)(e) kinasema *Residual Method*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu hivi viwili na ukienda kwenye uhalisia wa maisha ya Mtanzania, anayeishi kijijini, uki-*apply* unaona kabisa kwamba kuna changamoto ya kunyimwa haki yake, na hususan kwenye fidia. *Practically*, halmashauri inatwaa kwa mwananchi eneo, hekari moja kwa shilingi 1,200,000, ambayo ni *square meter* moja. Thamani yake ilikuwa ni shilingi 296, inaenda

kumuuzia mwananchi huyo huyo. *Square meter* moja kwa shilingi 3,000 ambayo ukiweka thamani hapo inakuwa ni shilingi 12,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji maboresho na hata ukiangalia hii, yaani *factor* ya *residual method* ni lazima uchukue *gross development value*. Ndiyo ukichukua *factors* hizo mbili unaweza ukaona kwamba sehemu hiyo anapata changamoto. Kwa hiyo, niishauri Serikali na pia Kamati, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya, lakini waangalie kwenye jicho hilo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine; Kifungu cha 52 (2)2 ndicho kinaonesha *validity,* kusema kwamba tathmini inayofanyika na Serikali au ya *valuer,* inaishi kwa muda gani? Nayo ni miaka miwili. Baada ya miaka miwili, ile *report* ya *valuation* inakuwa siyo *valid.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka nitoe mfano mmoja ambao upo kwenye Jimbo la Mtwara Vijijini, Kata ya Mbawala Shamba la Ludipe. Wananchi walifanyiwa tathmini Novemba, 2021. Tathmini hiyo ikaisha 2022 Machi, lakini mpaka leo hawajalipwa hiyo fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia muda, sasa hivi ni 2026, maana yake ni miaka minne imeshapita. Ile ripoti wakati inaandaliwa palikuwa na mashamba ambayo yana korosho, mashamba mazuri; na mwananchi akishaambiwa kwamba usiingie tena kwenda kufanya au kuendeleza shamba lako lile, basi linaachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya miaka minne, miaka mingapi, unakuja tena unataka kufanya *valuation* shamba lile limeshageuka kuwa pori, utampa thamani ipi? Kwa hiyo, *practically* bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Kamati na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mambo ambayo ameyafanya

kama vile kwenye Kifungu cha 50 kuongeza neno *"market"*, ni jambo jema, lakini vifungu hivi bado vinahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, *"Martin Luther King Junior* alisema: *"The law is not a monument, it is a movement."* Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dickson Lutevele, ajiandae Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada ulioletwa na Tume ya Kurekebisha Sheria na Mapendekezo. Kwanza kabisa, ninaomba nichukue nafasi hii kuipongeza Tume na niipongeze Wizara kwa kazi hii nzuri ya marekebisho ya sheria ambazo zimeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, ninaomba nijikite katika maeneo mawili kwenye marekebisho ya sheria yaliyofanyika kwenye Wakala wa Kusimamia Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze sana Serikali katika kurekebisha Sheria ya Leseni za Biashara *(Business License Act cap 208)* iliyoanzisha Fungu la 14(a) na kuleta amri ya Serikali katika kusimamia kuzuia wageni (raia wa kigeni) kufanya biashara fulani fulani (biashara 15).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii kwanza ninaiunga mkono na ninaipongeza sana kwa sababu katika nyakati tofauti tofauti, humu ndani tumetoa mchango na mawazo ya kuhakikisha Serikali inaendelea kulinda biashara wanazofanya wajasiriamali, vijana, akina mama na wananchi katika maeneo mbalimbali wale ambao wamewezeshwa na Serikali. Sheria hii inakwenda kuondoa wafanyabiashara wa kigeni wanaofanya biashara zinazofanywa na wazawa bila kuathiri diplomasia tuliyonayo baina yetu na Mataifa

ya jirani. Ninaipongeza Serikali kwa kuleta sheria hii kwa sababu imeonesha ni namna gani inazingatia yale ambayo Bunge linashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini katika Jimbo langu la Mafinga Mjini. Marekebisho haya yanayokwenda kufanyika, siyo tu yatalinda biashara za wajasiriamali, lakini yanakwenda kulinda biashara za wale wanaofanya biashara ya mazao. Tunaona kwamba biashara ya mazao kwa wakulima wetu na viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani kwa sasa kabla ya sheria hii, wako raia wa kigeni walikuwa wanazifanya kwa kwenda kununua moja kwa moja shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia sheria hii maana yake tutaongeza mnyororo wa thamani kwa wafanyabiashara wenyeji. Ninaunga mkono sheria hii na ninaiomba Serikali isimamie sana jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba nizungumzie suala la *BRELA* kufanya marekebisho. Sasa hivi *BRELA* imefanya marekebisho makubwa kupitia Mfumo wake wa *BRELA Online* ambapo wajasiriamali na wafanyabiashara wanajisajili kimtandao. Sasa ninaomba niishauri Serikali, jambo hili ni nzuri lakini limekumbwa na changamoto ya kimtandao kwenye maeneo hasa ya majimbo yaliyoko mbali sana na maeneo ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukulie mfano Jimbo langu la Mafinga. Wako wajasiriamali ambao wanachelewa sana kujisajili kwenye mfumo huu kwa ajili ya utaratibu wa kimfumo. Wengi hawajui elimu ya mfumo, lakini hawana vifaa vya kutosha, lakini wakati mwingine mtandao unakuwa *slow* sana. Kwa hiyo, unamwona mjasiriamali anachukua siku tatu mpaka nne kufanya zoezi moja la kujisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuko kwenye *Vision 2050,* ninashauri suala la kimtandao ni muhimu sana kuhakikisha kwamba

mitandao yetu inakuwa na *speed* sana kwa sababu tunaanzisha mfumo mzuri, lakini unakwenda kushindwa *field* kwa ajili ya kukosa mtandao wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia jambo moja tu. Ninaomba Mamlaka za Kiserikali katika jambo hili jema ziunganishe, mfanyabiashara anapokwenda kusajili *BRELA,* asajiliwe *TRA* kwa maana ya *TIN* na apate leseni ya halmashauri ili kuepusha usumbufu kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wale wanaokwenda kuchukua leseni. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, Mheshimiwa Agnesta Lambert na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi wajiandae, na tutamalizia na mtoa hoja.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Nami kama wenzangu waliotangulia kusema, kwa kweli niipongeze sana Serikali kwa kuleta Miswada hii mbalimbali ambayo tunaijadili sasa hivi Mezani kwetu. Kiuhalisia kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, na leo Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu hii Miswada kwa kweli ni mizuri na ni ya wakati huu na hasa ile ya mifugo na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo tafsiri sahihi na halisi ya Serikali inayosikiliza, kwa sababu wafugaji wengi sana wametaifishiwa mifugo na wamekuwa maskini kwa sababu hiyo. Leo kuleta Muswada wa aina hii ni kuwarejeshea matumaini na hasa kile alichokisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuhakikisha

kwamba haki inaonekana na inatendeka. Kwa kweli, tunawashukuru sana na sisi tutaiunga mkono na wananchi wenzangu kule Ngorongoro ambao leo wanaifuatilia kwa *television* mjadala huu watakuwa wamefurahi sana na mimi binafsi nimefurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitatumia muda mrefu sana kuchangia. Kuna kipengele ambacho kwa kweli na chenyewe kinatakiwa tukitazame kule mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kipengele cha 116 (2)(a) kinachompa mamlaka Mkurugenzi wa Wanyamapori kutoza *fine,* wanaita *compound offense* ya shilingi 200,000 mpaka karibu shilingi 10,000,000 kwa aidha kundi la ng'ombe au kundi la kosa. Kwa kweli hiyo ni sawasawa tu na kufilisi, kwa sababu...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningefurahi huko mbeleni tunapoelekea tujadili na hicho kipengele ili tutafute namna ya kumwelekeza Mkurugenzi wa Wanyamapori namna ya kutoza ile *fine,* kwa sababu na yeye ni binadamu kama sisi.…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** …Mara nyingine anasukumwa na ushawishi, mara nyingine anasukumwa na hasira iliyoko katika kipindi hicho...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutazame na hicho kipengele namna ya kukirekebisha ili tumpe ushauri na maelekezo ya namna ya kutoza *compound offense* kwa sababu mara nyingi sana wanaishia kwa kiwango cha juu cha shilingi 10,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kweli ninakushukuru na ninaendelea kuwapongeza na kuwaunga mkono hiyo hoja ipite. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, tutamaliza na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa machache kuhusiana na hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 25 Julai, 2026 ndani ya Bunge lako hili Tukufu wakati wa kipindi cha maswali ya papo kwa hapo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilileta hoja au swali kwa Mheshimiwa Waziri nikiiomba na kuishauri Serikali iweze kufanya marekebisho katika sheria mbili. Sheria ambazo zilikuwa zinapelekea uchaguzi wa Naibu Meya na Wenyeviti wa Halmashauri kufanyika kila baada ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anajibu swali langu la papo kwa hapo, kwanza kabisa alikiri kwamba na yeye katika ziara zake anazozifanya amegundua kwamba hii ni changamoto kubwa sana ya kufanya uchaguzi kila baada ya mwaka mmoja, na akakiri mbele ya Bunge lako Tukufu akasema anaiona hoja kubwa ndani ya swali langu na hivyo akaahidi kwamba katika udharura wake wataleta marekebisho ya sheria hapa Bungeni kupitia Mwanasheria ya Mkuu wa Serikali. Hivi nilivyosimama mbele yako, ninapenda kuipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo wameahidi na sasa wametenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa AG amefanya kazi kubwa sana na nzuri pamoja na Kamati. Nikiri na niseme kwamba anakwenda kuweka historia kwa sababu halmashauri zetu zinapokwenda kutulia, kufanya na kupanga maendeleo kwa ajili ya wananchi, ile kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais ya kuwaacha na

tabasamu Watanzania inakamilika na inaonekana kwa matendo, na hiyo ni kwa sababu halmashauri zetu zinakwenda kutulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nimesema ninaipongeza Kamati na Waziri wa TAMISEMI ambapo kwa pamoja wameshirikiana kuhakikisha kwamba mambo haya yanafanyika. Nikiri kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita imekubaliana na mapendekezo ya Mbunge anayetokana na chama cha upinzani na ni kwa sababu imeona kuna tija kubwa sana. Awamu hii ya Sita haijajikita katika uchama, bali imejikita katika kuwaletea wananchi maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mheshimiwa, wakati ninaelekea mwisho kwa ajili ya muda, ninaomba niseme kwamba Serikali imeona mbali sana. Waheshimiwa Wabunge, wote ni mashahidi, humu ndani katika halmashauri zetu vikumbo havijawahi kuziacha salama halmashauri zetu. Madiwani na sisi wenyewe Wabunge tumekuwa tukihusishwa moja kwa moja na migogoro inayotokana na chaguzi za kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba kwa kusema kwamba kupitia marekebisho haya Mheshimiwa *AG* huko nje katika halmashauri na kwa wananchi, kwa sababu ambao walikuwa wakiumia ni wananchi, wala siyo Madiwani kwa sababu pale halmashauri zinapozorota, ina maana maendeleo hayaendi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa siyo mtu wa shukrani ikiwa sitampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tunafahamu kwamba Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani, na sheria zote zinazobadilishwa lazima zipite mikononi mwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba Mheshimiwa Rais katika hili ameonesha kwa uwazi kabisa kuwa yeye ni muumini wa hoja zinazoleta maendeleo kwa wananchi wake bila kujali hoja imeletwa na Mbunge wa chama gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kumwomba Mheshimiwa *AG,* wakati anakuja hapa ku-*wind up* ningependa kufahamu tumepitisha au tunakwenda kupitisha mabadiliko haya ya sheria? Je, wale Manaibu Meya walioko kwa sasa, na wale Makamu Wenyeviti walioko kwa sasa katika sheria hii, wataendelea na nafasi zao, au tena tutaingia katika mchakato wa uchaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi na kwa kuishauri Serikali sioni kama kuna haja wala tija ya kuingia tena katika uchaguzi wakati Manaibu Meya waliopo na Wenyeviti wanachapa kazi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ABDULLAH A. MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami ninatoa shukrani za dhati kwa kunipa wasaa wa kuchangia maneno mawili matatu kwenye Muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia sheria moja mahususi ambayo haikuzungumzwa sana. Nayo ni Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Mali na Raslimali Asilia, Sura ya 449.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa kuwa msikivu. Hoja ya kurekebisha haya ilitoka kwa wakili msomi, Mheshimiwa Edward Olelekaita na Serikali ikaiona ina mashiko na hatimaye wakachakata na kuileta hapa na kufanya haya mabadiliko ya msingi kabisa. Mabadiliko haya yanaendana sambamba na utekelezaji na kufika kwenye *Vision 2050.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vision 2050* inataka uwekezaji na fedha nyingi sana ziingizwe kwenye uchumi. Sehemu kubwa ya

*Vision 2050* kama tulivyozungumza hapo awali ni sehemu ya sekta binafsi; Sekta binafsi ya ndani na sekta binafsi ya nje. Sasa uwekezaji mkubwa kama wa *LNG,* kama tunavyotaka kuweka *refinery* pale Tanga, kwenye migodi ya hali ya juu yenye thamani kubwa sana wawekezaji, lazima wawe na imani na amani kwamba pakitokea mgogoro, kutakuwa kuna *tribunal,* kutakuwa kuna taasisi *neutral* ambayo inaweza ikakaa ikatazama na ikatatua ile migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha uwekezaji mkubwa kama hivi dola bilioni; *LNG* peke yake ni zaidi ya dola bilioni 42. *Refinery* inaweza kufika dola bilioni 20. Ulimwenguni kote nchi zilizoendelea na zisizoendelea haiwezekani watu wakaweka fedha ndani ya nchi za kiwango hicho halafu wasiwe na *tribunal* ya wabobezi ambao ukitokea ugomvi wa aina yoyote au kutokuelewana wakakaa wakafanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi haya yanaakisi sheria. Katika sheria, katika Jumuiya ya Madola *(Common Law)* kuna *concept* ya *privity of contract*. Yaani wale ambao wameingia kwenye mkataba wao wenyewe wana haki ya kuamua mambo ya ndani ya ule mkataba bila mtu mwingine kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la *arbitration* ni mkataba ndani ya mkataba. Mkataba mmoja wa uwekezaji, mkataba wa pili ni wa makubaliano kwamba tunafanya nini kama likitokea tatizo lolote; na *advantages* zake ni nyingi. Moja, tunapata sehemu *neutral* baina ya watu wawili ya kufanya maamuzi, kila mtu hatakwenda kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ulimwenguni ikitokea hukumu, kukazia ile hukumu kwenye *arbitral award* ya namna hii, inakuwa rahisi. Nchi zaidi ya 200 zinaafikiana na mfumo huo, lakini *in country award* siyo rahisi ku-*enforce* nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wakati mwingine mikataba ile ina *trade secrets*; kuna siri ndani yake ambayo watu hao wawili wasingependa zitoke. Sasa *arbitration* ni *private*, mikutano inakuwa

ya faragha baina ya pande mbili, wanaletwa wabobezi; kila mtu anamleta mbobezi wake halafu maamuzi yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, muda wa hukumu. Kwa kuwa wabobezi wanatoka sehemu mbalimbali na kwa sababu wameletwa kwa kazi ile tu, muda wa hukumu unakuwa mapema na haraka. Haiwezekani tukawa na jambo la msingi, likaingia katika Mahakama za kawaida ambazo muda wake hatuna uhakika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mfumo huu na mantiki hii hata ndani ya nchi upo. Masuala ya kikodi kwa mfano, yanakwenda kuhukumiwa kwenye wabobezi wa kodi. Ndani ya nchi hapa hayaendi kwenye Mahakama za kawaida, kuna *TRAB* na *TRAT* mnakumbuka? Masuala ya *procurement* vilevile kuna mahakama zake, kwa sababu inahitaji utaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, ninapenda kumaliza kwa kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa kuleta marekebisho ya msingi kabisa ambayo yataweza kutuendeleza na kukuza uchumi wetu. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho wa Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.02) Bill, 2026]*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 10 wamechangia Muswada huu. Waheshimiwa Wabunge hao wote 10 wamechangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge, na hakuna Mbunge ambaye amechangia kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Fadhili Liwaka, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, Mheshimiwa

Isack Copriano, Mheshimiwa Arif Premji (huyu ni Mbunge wangu huyu katika Jimbo letu la Mtwara Vijijini), Mheshimiwa Dickson Lutevele, Mheshimiwa Yanick Ndoinyo, Mheshimiwa Agnesta Kaiza na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia wameunga mkono hoja, lakini na kuendelea kutoa maoni yao katika maeneo mbalimbali katika Muswada huu ambayo nayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa katika Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, labda nianze na kuzungumzia suala ambalo Mheshimiwa Fadhili Liwaka alitaka kupata majibu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu namna ambavyo mkulima na mazao yake yatakavyoweza kulindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tufahamu kwamba Sheria hii ya Wanyamapori inaondoa suala zima la utaifishaji wa mifugo inapoingia ndani ya hifadhi. Kwa hiyo, tunaondoa ule utaratibu wa kutaifisha mifugo hiyo, kwa sababu, utekelezaji wake kwa utaratibu ule tuliokuwa tunaufanya, tulikuwa tunakwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nitawasomea Ibara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa kwa kuigusa Ibara hiyo ingawa yeye alikomea ile ya kwanza. Ibara ya 24(1), na Ibara ya 24(2) na nitaisoma, “bila ya kuathiri masharti ya Ibara ndogo ya kwanza, ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha, au madhumuni mengineyo bila ya idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia.” Kwa hiyo, huwezi kuinyang'anya. Hilo haliwezekani, ni kinyume na Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Ibara hii inazungumzia mtu kutaifishiwa mali yake. Anaweza kuwa mfugaji, anaweza kuwa mkulima, anaweza kuwa mfanyabiashara, anaweza kuwa mvuvi,

anaweza kuwa mchimbaji na makundi hayo yote yamelindwa na Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa mfugaji, kuanzia mfugaji mdogo, mfugaji wa kati au mfugaji mkubwa, utalindwa. Ukiwa mkulima, mkulima mdogo au wa kati utalindwa; mchimbaji madini na kadhalika. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Fadhili Liwaka; lakini, aliniuliza kwamba sasa mkulima na mazao yake analindwa na sheria gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima na mazao yake analindwa na Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16, imeweka wazi kabisa ni kosa kwa mujibu wa sheria kuharibu mali za watu. Kwa hiyo, mazao yakiharibiwa ni kosa kwa mujibu wa sheria. *The Penal Code,* Kifungu cha 325 kimeweka hilo ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo lisimtie wasiwasi na sheria ile inaenda kuondoa ile changamoto ambayo wafugaji walikuwa nayo pale mifugo yao ilipokuwa ikiingia kwenye hifadhi inataifishwa. Kwa hiyo hilo tumeliweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zile ambazo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wananipa ni za Mheshimiwa Rais. Ninashukuru sana kwa pongezi, lakini sisi tunafanya kazi kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambapo yeye lengo lake anataka kutoa tabasamu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tutahakikisha kwamba sheria hizi tunazioanisha na lengo hilo kwamba akiwa mkulima awe na tabasamu, akiwa ni mfanyabiashara apate tabasamu, akiwa ni mchimbaji wa madini apate tabasamu, akiwa ni mvuvi apate tabasamu, na wote katika makundi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashukuru sana kwa pongezi, lakini pongezi hizi kwa kweli tumpatie Mheshimiwa Rais kwa

maono yake na maelekezo yake mbalimbali anayotupatia ili kuhakikisha kwamba tunatimiza malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nikiwa ninajibu yote kwa ujumla, ni kwamba, zoezi hili la kuendelea kurekebisha sheria ili ziendane na Dira, ni endelevu. Jana nimeyataja makundi ya sheria zote ambazo tutazirekebisha, na nilisema jana kwamba, sisi tunataka tukifika mwaka 2050, pato liwe Dola za Kimarekani trilioni moja ambayo mimi huwa ninapenda kuongea kwa fedha ya Kitanzania, naona ndiyo inaeleweka vizuri, kwamba shilingi trilioni 2,600 kwa *exchange rate* ya jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, pato la mtu mmoja mmoja liwe Dola za Kimarekani 7,000, kwa *exchange rate* ya leo, ni sawa sawa na shilingi milioni 18.2 pato la kila Mtanzania. Kwa hiyo, akiwa mfugaji, awe mkulima, wote. Huko ndiyo tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kwa dhamira ya dhati, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuchapa kazi na kuhakikisha kwamba sheria hizi zote tunazioanisha, zenye vikwazo tunaviondoa ili wananchi wapate tabasamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanazuoni mashuhuri wa sheria anaitwa *Roscoe Pound* aliwahi kusema, "*Law must be stable and yet cannot stand still.*" Kwamba, pamoja na umuhimu wa sheria kuwa na uthabiti na kutoa uhakika, ni lazima pia ziendelee kuhuishwa ili kukidhi mahitaji ya jamii na kuondoa changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wake Abraham Lincoln ambaye alikuwa Rais wa 16 wa Marekani, aliwahi kusema, "*The world is moving on, and we must move with it. The doctrines of the past are inadequate to the storm of the present.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, ulimwengu unaendelea kubadilika, ni lazima na sisi tubadilikenao au kwa lugha ile nyingine, tunyumbulikenao. Sheria nazo lazima zinyumbulike hivyo hivyo. Nadharia za zamani hazitoshelezi tena kuhimili mawimbi ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hizi zinaonyesha umuhimu mkubwa wa kufanya mabadiliko katika sheria na taasisi kadri mahitaji ya kimaendeleo yanavyojitokeza. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hizi kazi na kuhakikisha kwamba sheria zetu tunazihuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango iliyotolewa, mingi ilikuwa ni ya kuunga mkono, na kama nilivyosema, tunashukuru na tutaendelea kuboresha. Maoni mengi yaliyotolewa tumeyachukua, na utaenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa Mheshimiwa Arif Premji kuna maoni mazuri ambayo ameyatoa na wengine. Yote tutaenda kuyafanyia kazi kwa sababu zoezi hili ni endelevu. Bunge la mwezi wa Novemba tunaingia na mabadiliko mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana niliahidi leo tunaingia tena na Muswada mwingine na tumefanya hivyo. Mwezi wa 11 tutaingia na mabadiliko mengine. Kwa hiyo, tutaendelea. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Kaiza, waendelee, wao waliopo wanaendelea tu, sisi tumeweka mifumo ya kisheria sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itatoa msukumo wa kipekee ili kuhakikisha malengo ya Dira 2050 yanafikiwa, lakini mbali na sheria, katika kufikisha azma hii, nimeelekeza kuimarisha pia usimamizi wa mikataba, majadiliano na uwekezaji, na sasa hivi tumeondoa ile changamoto iliyokuwa kwenye Sheria ya *Natural Work* ili mikataba ya kimkakati iwe nyenzo ya kufikia malengo ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema kwamba, ule mpango wetu wa kuanzisha Kituo cha Usuluhishi *(Arbitration Center)* chenye hadhi ya Kimataifa, unaendelea na tunausimamia kwa karibu ili tuwe na Kituo cha Usuluhishi hapa nchini ambacho kina hadhi ya Kimataifa hata mtu kutoka *Hong Kong* atake kuja kufanya usuluhishi hapa. Yaani Tanzania iwe *Famous City of Arbitration,* na hilo tutalisimamia kuweza kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha hoja yangu, ninapenda kuwashukuru sana sana, Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na maoni yao tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kazi nzuri. Kama nilivyosema jana, kazi ya kutunga sheria katika nchi ya kidemokrasia ni ya wananchi, mamlaka ni ya wananchi, lakini wananchi wanafanya kazi hiyo kutumia Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ya utungaji sheria katika Bunge iko kwenye ngazi ya Kamati, kwa sababu wana nafasi ya kuita wadau na wana nafasi ya kujadiliana na Serikali. Sisi kama Serikali tutasikiliza sana maoni ya Kamati kwa sababu ndiyo wananchi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo anavyotuongoza katika Bunge letu, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na ninawashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole; na watendaji wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hili tumelifanikisha vizuri na limetokana na maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya kipekee ninaomba kumshukuru kwa maelekezo yake mazuri ambayo leo yametuwezesha kuweka tabasamu kwa wafugaji. Tutaendelea kuweka tabasamu kwa makundi mengine ya kijamii ili kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais ya kuwapa tabasamu Watanzania. Mheshimiwa Rais, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.02) Bill, 2026]***

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kifungu kipya cha 6
Kifungu kipya cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu kipya cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya Mabadiliko yoyote)*

Mpangilio mpya wa Ibara ya 6 – 26 kuwa Ibara ya 8 – 29

*(Mpangilio wa ibara tajwa hapo juu ulipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 105 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninapenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 02) Bill, 2026)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 02) Bill, 2026)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na sasa nitawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo Saba kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamebainika Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria Hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Sasa natamka rasmi kwamba Muswada huu umepitishwa kwa hatua zote za Kibunge na sasa mamlaka ya Mheshimiwa Rais itafuata kwa ajili ya hatua nyingine. Ninachukua nafasi hii kukupongeza sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na ofisi yako kwa kazi kubwa mliyoifanya.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujahitimisha shughuli za leo, ninaomba nilete kwenu matangazo. Kwanza tuna tangazo la wageni walioko Bungeni mchana huu. Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo kutoka Kiwanja cha Ndege Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanawake 74 wa Kanisa la *Pentecost City* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, anaomba kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kagera, Simiyu, Kigoma, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Njombe na Mbeya kesho siku ya Alhamis, tarehe 3 Septemba, 2026 kuanzia saa saba mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Ajenda ya kikao hiki ni uelewa wa mikopo inayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa vijana hususan ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba. Waheshimiwa Wabunge wa mikoa tajwa mnaomba kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, tunakumbushwa pia kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Ndani kwamba Idara ya Uhamiaji watakuwepo hapa kesho kwa ajili ya kutoa *Passport* za kusafiria kwa Waheshimiwa Wabunge ambao walishawasilisha maombi yao, na endapo kuna changamoto yoyote, basi tunaomba tumwone Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, ninarudia tena kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na timu yake kubwa kwa kuwasilisha mapendekezo haya ya mabadiliko ya sheria mbalimbali. Pia ninaipongeza Kamati yetu ya Bunge kwa kutoa maoni na kuboresha Muswada. Vilevile ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia Muswada huu ambao tumeupitisha muda siyo mrefu. Hongereni sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kwa hakika lile ambalo limekuwa ni kero ya muda mrefu kuhusiana na mifugo, mnayaishi na kuyatenda kwa dhati maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hasa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Basi tunawatakia utekelezaji mwema na kama ambavyo Mheshimiwa AG umesema, tutaendelea kupata maboresho mbalimbali au marekebisho mbalimbali ya sheria mbalimbali. Ni matumaini yetu kwamba matamanio ya wananchi wetu wote yatafikiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho Alhamis saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.25 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 3 Septemba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*